<sup>25</sup>Kuna na mambo yangine menji ya Yesu ahendeyeyo. Ela ṭambere yonse ni kworegwa, naṭara haṭa huju lumwengu jwenye ntajundeewa na pfantu pfa kuviweka hivi vyuo vya kwamba vindekworegwa.

## Mahendo

### Mahendo 1

- <sup>1</sup>Kwa Muhilwa Tofilo: Kuzimuni mwa chuo changu cha dura nyora dzuu ya mambo yonse ya Yesu ahendeyeyo na kuyongweeza, hangu nsiku adabviyeyo kaziye
- <sup>2</sup>haṭa nsiku adzeyoakihwajwa dzuu mbinguni. Asidzahwajwa dzuu mbinguni, kawaḍama kwa nguvu za Ruhu Mudheru hawa wantu atsaniyeo dza ntumi wakwe.
- <sup>3</sup>Kwa nsiku miyongo mine ḅaada ya kupfatsikwakwe, Yesu kawaṭupukia ntumiwe mweedha kwa mweedha kwa namuna isiyokajeleka kwamba ka moja. Wamuona na kanena nao dzuu ya Uhaju wa Muungu.
- <sup>4</sup>Epfokuwa pfamodza nao amaale, kawaamuru kawamba, “Namutsenuka Yerusalemi, ela indani ṭola ya Baba amuahidiyeyo, niyomwambia.
- <sup>5</sup>Yohana kaṭopya wantu na madzi, kenge nywinywi mudzaṭopyegwa na Ruhu Mudheru ḅaada ya nsiku kachuchu.”
- <sup>6</sup>Hawa ntumi wepfoṭuṭaa pfamodza na Yesu, wamuuza wamwamba, “Ḃwana, munamba ujwakuwagalichia uhaju wantu wa Isiraeli mahafufini?”
- <sup>7</sup>Yesu kawambukuya kawamba, “Ngera na nsiku vinawekwa ni Baba jeje hekeṭu, ela si dzuu yenu kumanya ya kwamba vinawa ari.
- <sup>8</sup>Ela Ruhu Mudheru adzefomusukia, munadzazwa nguvu. Munawa mashaahidi wangu hangu Yerusalemi na nsi yonse ya Yuḍaya, Samaria, na haṭa yukungo jwa lumwengu.”
- <sup>9</sup>Epfokwisa kunena hivi, huku wakiwa kumuyowani, kahwajwa kwenda mbinguni. Kwa dzambo ḍya wingu ḍimufinikiziyeyo ntawakumuona kawii.
- <sup>10</sup>Yesu epfoakipfaa mbinguni, hawa ntumi wewa kumakiani gu yuwinguni. Iyo saa, wantu wawii wawwaiyeo nguo nyeupe wasumama hafufi nao.
- <sup>11</sup>Wawauza wawamba, “Wantu wa Galilaya, kuṭi musumama hapfa mukwakudabvani ndulu yuwinguni dzuu? Huyu Yesu ahwajwe kwenu kwenda mbinguni, anauja dza viviḍe mumuoneyeyo akiwa kwendani mbinguni.”
- <sup>12</sup>Makisa hawa ntumi wauja Yerusalemi kuyawa Murima wa mihi ya Mizeituni, wiwokuwa haṭuwa mfufi nze ya hu mudzi.
- <sup>13</sup>Wanjia Yerusalemi na wenda haṭa chumba cha ḍarini dzuu wemowakikaa. Wewa ni Peṭero, Yohana, Yakobo na Anḍerea, Filipo na Tomasi, Baṭolomayo na Matayo, Yakobo mwana jwa Alifayo, Simioni Muziloti na Yuḍa mwana jwa Yakobo.



<sup>14</sup>Wekiṭuṭaa kuyombani mweedha kwa mweedha pfamodza na wake wangine, na Maria mamajwe Yesu, na wanduguzwe Yesu.

<sup>15</sup>Hizihiziḍe nsiku, kwiiṭuṭaa wantu wamuhikiziyeo Kiristo chima cha gana modza na miyongo miwii. Peṭero kasumama kunena kahi yao.

<sup>16</sup>Kamba, “Wandugu zangu, haya yorejweyo kuzimuni mwa haya matsoro madheru yewa ni haḍi yaṭimiye. Ruhu Mudheru kamuhendeza Ḍauḍi kunena dzuu ya Yuḍa. Kayavya unabii wa haya ya Yuḍa andeyohenda, huyu ayongoweyee wantu wadzeowakimugija Yesu.

<sup>17</sup>Kwa kwamba Yuḍa ewa katsanwa kumuhumikia Muungu pfamodza naswi, ewa mumodza jwa kiṭaro chehu.”

<sup>18</sup>Yuḍa kaguya nkonde na hizi fwedha aipfijwezo kwa hendo ḍyakwe zuka. Nae kagwa pfapfaḍe, kaḅaika na kahi na ntumboze zonse ziyawa nze.

<sup>19</sup>Kula muntu jwa Yerusalemi kasikia haya yamuhendekeeyo Yuḍa. Ndookomu kwa lugha yao wenye waihana hiḍe nkonde “Hakelidama,” yani “Nkonde ihikiyeyo mwazi.”

<sup>20</sup>Peṭero kongeza kunena kamba, “Koro vyoregwa chuoni mwa Zaburi, ‘Nyumbaye naiwe ntupfu, nakutseewa yuḍejwone jwa kuishi humo humo.’ Na kawii vyoregwa, ‘Pfantupfe pfa uhumisi napfahwajwe ni muntu yungine.’

<sup>21</sup>Ḍubva ni haḍi hutsane muntu mumodza jwa kuungana naswi kuwambia wantu kwamba Ḍwana Yesu kafufuka kuyawa kwa wafu. Ni awe mumodza jwa hichi kiṭaro chehu chichochikigijana na Ḍwana Yesu ngera zonse, hangu ngera aṭopyejweyo ni Yohana haṭa nsiku adzeyoakihwajwa kwenda mbinguni.”

<sup>23</sup>Ndookomu wahadza wantu wawii: Yusufu, eyehanwa Barisaba (pia ekihanwa Yusto) na Matia.

<sup>24</sup>Makisa wayomba wamba, “Ḍwana, kumanya myojo ya wantu wonse. Ḍubva, huyange huyu umutsaniyee kahi ya hawa wantu wowii,

<sup>25</sup>ahwae pfantu pfa uhumisi dza ntumi. Hu ni uhumisi wa Yuḍa ayatsiyeo kwenda ekonamala kuwa.”

<sup>26</sup>Makisa wabiga kura, na kura imugwiya Matia. Nae wamungiza hichi kiṭaro cha hawa ntumi kumi na mumodza.

## Mahendo 2

<sup>1</sup>Nsiku ya Pentekoste ipfofika, hawaḍe wonse wamuhikiziyeo Kiristo waṭuṭaa pfantu pfamodza.

<sup>2</sup>Ḍwikira, wadzawasikia sauti kuyawa yuwinguni iyokuwa dza sauti ya vuṭo kali, na idzaa humu nyumbani mwonse wemokaa chihako.

- <sup>3</sup>Makisa waona vija vivyo dza vibilibili vya moho vikwakuḡdachaani na kuhama dzuu ya kula mumodza jwao.
- <sup>4</sup>Wonse wadzajwa ni Ruhu Mudheru na waḡabva kunena na lugha garagara, dza vya Ruhu awapfiyevyo kunena.
- <sup>5</sup>Kwiwa Wayahuḡi weowakikaa Yerusalemi. Wewa wantu wamuhiliyeo Muungu, wayawiyeo kula nsi ya lumwengu.
- <sup>6</sup>Wepfosikia hiyo hoisa, tuḡa nkuu ya wantu idziana hapfaḡe. Wamaka, koro kula mumodza kawasikia hawa wamuhikiziyeo Kiristo wakiwa kunenani na hi lugha yakwe mwenye
- <sup>7</sup>Wamaka muno haḡa wamba, “Dzaambia awa weokunenani na lugha garagara si Wagalilaya tswee?”
- <sup>8</sup>Viiwadze ḡubva, kwamba hwonse hwakuwasikiani wakiwa kunenani na lugha zehu wenye?”
- <sup>9</sup>Huyawa Pathia, Midia na Elami, na wangine wayawa Mesopotamia, Yuḡaya, Kapadokia, Ponto, Asia,
- <sup>10</sup>Furugia, Pamufilia, Rumi, Misiri na ḡanda za nsi ya Libiya ziizo hafufi na Ukirene,
- <sup>11</sup>hangu Wayahuḡi na haḡa wantu wa vyeeti vingine waubiyeyo ḡini ya Kiyahuḡi. Na wangine wehu wayawa Kirete na Arabuni. Ela hwonse hwakuwasikiani wakiwa kunenani na lugha zehu wenye dzuu ya haya mambo makuu ya Muungu ahendeeyo!”
- <sup>12</sup>Kwa dzambo ḡya kimako na kipapo wechokuwa nacho, waḡabva kuuzana wao na wao wakyamba, “Hivihivi maanaye ni?”
- <sup>13</sup>Ela wantu wangine wawabaladhaiya hawa wahikiza wawamba, “Hawa waruma nawe!”
- <sup>14</sup>Peḡero eyekuwa pfamodza na hawa ntumi kumi na mumodza, kasumama wima. Kaḡabva kunena ne tuḡa ya wantu na idzwi kuu kamba, “Wenzangu Wayahuḡi nanywi nyonse mwiwokukaani Yerusalemi, pfindiiyani muno hivi vyyuwo vyangu.
- <sup>15</sup>Hawa wantu ntawakuruma dzevi vyenu mwivyokuḡarani haḡa. Koro amaale ni saa ntahu tu za magura.
- <sup>16</sup>Ela haya ndiyo yanenejweyo ni nabii Yoeli akyamba, ‘Muungu kamba:
- <sup>17</sup>Haya ndiyo nidzeyohenda nsiku za mviso. Wantu wonse nidzawakakanyia Ruhu jwangu. Wanawayume na wanawake wenu wadzayavya unabii. Orani wenu wadzaona nzozi, na wazee wenu wadzayoheswa ndoho.

- <sup>18</sup>Ndivyo, haṭa wahumisi wangu, wake kwa wayume, nsiku hizo nidzawakanyia Ruhu jwangu, nao wadzayavya unabii.
- <sup>19</sup>Nidzahenda mafara ya kumakisa yuwinguni dzuu, na kuyanga vihambwiizo lumwenguni. Kudzahika mwazi, na kudzawa moho na mosi muziho.
- <sup>20</sup>Hiḍi dzuwa ḍidzagijwa ḍinjie kiza, na hu mwezi nao udzagijwa na unapfyehuka ranji ya moho dza mwazi. Haya yadzahendeka kaḅila hi Nsiku ya Ḃwana ya kujuhukumu lumwengu ntaidzafika.
- <sup>21</sup>Makisa, yuḍejwonse adzeemuiya Ḃwana, huyo kadzapfonywa.’ “
- <sup>22</sup>Kawii Peṭero kamba, “Wantu wa Isiraeli, pfindiiyani hivi vyuuwo! Yesu jwa Nazareti ewa muntu atsanijwe kuhenda kazi ya Muungu. Nanywi mwiiyangwa tswee na mambo ya mafara, mambo ya kumakisa, na vihambwiizo vya Muungu ahendeevyo kuchiiya kwakwe. Nywinywi wenye muyamanya haya, koro yahendeka hapfa, kahi yenu.
- <sup>23</sup>Muungu ewa kesakuhuna kwamba Yesu angizwe mikononi mwenu. Koro iwa miroye mwenye, na evimanya vyonse haṭa visidzahendeka. Nanywi mumuyaga, kwa kuhendeza wantu wanabvise wamupfatsike muhini mwa mpatsa.
- <sup>24</sup>Ela Muungu kamufufuya kuyawa kwa wafu. Kamunwiiya tsungu wa kufwa, kwa dzambo ḍya kwamba kifo ntachindeweza kumuweka mufungwa.
- <sup>25</sup>Koro Ḃauḍi kanena dzuuye, kamba, ‘Nimuona Ḃwana usoni yangu kuṭwa, jeje anami, ndookomu siṭosukusika.
- <sup>26</sup>Ndookomu moja wangu una tsekea, nami nanena na tsaiko. Na haṭa ninkiwa muntu jwa kudzafwa, nagija kuwa na madzikwatyo kuṭwa.
- <sup>27</sup>Kwa kwamba wewe Muungu nkunaniyatsa lumwengu jwa wafu, nolawe nkunamuyatsa muhumisi jwako mwema kufwa awowe.
- <sup>28</sup>Kuniyanga njia za maisha, na kwa dzambo ḍya kwamba kwaa pfamodza nami nina tsekea nkuu muno.’
- <sup>29</sup>Ndugu zangu, ni haḍi ninene wekeani tswee, dzuu ya bibi jwehu Ḃauḍi. Kafwa na kazikwa, na mbeeraye ya hapfa pfehu haṭa yeo.
- <sup>30</sup>Ḃauḍi ewa nabii, ndookomu emanya ahaḍi ya Muungu eyomuyapfia kwamba kadzamuhenda mumodza jwa kivyaziche kuwa haju, dzevide vyakwe evyokuwa haju.
- <sup>31</sup>Ḃauḍi ewa kaona mambo ya Muungu adzeyohenda. Ndookomu kanena dzuu ya kufufuka kwa Kiristo, epfokwamba, ‘Nkakuyatswa lumwengu jwa wafu, nolawe kivimbache ntachikuwowa.’
- <sup>32</sup>Ḃubva Muungu kamufufuya yuyo Yesu kuyawa kwa wafu, naswi hwonse humuona na matso yehu wenye.

- <sup>33</sup>Kapfazwa dzuu haṭa ḍanda ya mukono kuyume wa Muungu, na kapfokea Ruhu Mudheru dza vya Babajwe evyomuahiḍi. Ndookomu, mwichokuonani na kusikia hi hii saasambi ni huyu Ruhu Mudheru ayehejwe kwehu ni Yesu.
- <sup>34</sup>Koro Ḍauḍi mwenye nkakwenda mumpaka mbinguni, ela kamba, ‘Ḑwana kamwambia Ḑwana jwangu, “Ikaa mukono wangu wa kuyume,
- <sup>35</sup>haṭa nidzefowangiza nyabvao mikononi mwako.” ’ ’ “
- <sup>36</sup>Peṭero kongeza kunena kamba, “Ḍubva wantu wonse wa Isiraeli, nawamanye hakika kwamba huyu Yesu, mumupfatsikiye nywinywi muhini mwa mpatsa, ndiye jwa Muungu amuhendeye Ḑwana na Masiya!”
- <sup>37</sup>Hawa wantu wepfosikia hivi, wanjijwa ni muhangaiko mukuu wa myojo. Ndookomu wamuuza Peṭero na hawa ntumi wangine, wawamba, “Ndugu zehu, huhendedze?”
- <sup>38</sup>Peṭero kawambukuya kamba, “Pfyehuzani mama, kula mumodza jwenu, na muṭopyegwe kwa sari ḍya Yesu Kiristo ili mupate kuyatsijwa nabvise zenu. Nae Muungu anamumpa ṭolaye ya Ruhu Mudheru.
- <sup>39</sup>Koro ahaḍi ya Muungu iwa iwekwa kwenu na kwa vivyazi vyenu, na kwa wonse weo kuye, na kwa wonse wa Ḑwana Muungu jwehu ahaniyeo kwakwe.”
- <sup>40</sup>Peṭero kawafunda na kuwangiza nguvu hawa wantu na vyyuwo vingine vinji akiwamba, “Dzipfonyeni, mutsekudzahukumigwa dza hawa wantu wazuka wa hizi hizi nsiku!”
- <sup>41</sup>Wenji wao wahikiza vyyuwovye na waṭopyegwa. Kiṭaro cha wahikiza chongezeka na wantu chima cha elefu ntahu hiyo hiyo nsiku.
- <sup>42</sup>Hawa wonse wagija kuyongweezwa ni hawa ntumi, wakikaa pfamodza dza ndugu, wakihariana chakuḍyani na kumuyomba Muungu pfamodza.
- <sup>43</sup>Hawa ntumi wahenda mambo ya kumakisa na vihambwiizo vinji, haṭa kula muntu kanjijwa ni oga.
- <sup>44</sup>Hawa wamuhikiziyeo Kiristo wonse wakaa pfamodza dza ndugu, na kutumia kula wechokuwa nacho pfamodza.
- <sup>45</sup>Koro wekiguza makonde yao na vija vyao, na kugawana hizi fwedha kahi yao wonse, kula muntu kwa chima cha haḍya yakwe.
- <sup>46</sup>Kula nsiku wekitsanganika pfamodza Hekaluni. Ela wekikaa na kuḍya pfamodza madzumbani mwao. Wetsakana, na wekiḍya hicho chakuḍya na tsekea.
- <sup>47</sup>Wekikaa na kumushaḍa Muungu, na weetsakwa ni wantu wonse. Ḑwana kagija kuchongeza hichi kiṭaro cha hawa wahikiza nsiku kwa nsiku, koro kula nsiku kwiwa wantu wangine weowakimuhikiza Ḑwana.

### Mahendo 3

- <sup>1</sup>Nsiku modza Peṭero na Yohana wenda Hekaluni saa kenda za musikahi, saa za mayombo.
- <sup>2</sup>Hapfaḍe pfa hu muḍyango wa Hekalu wiwoukihanwa Muḍyango Mwema, kwiwa muntu eyekuwa kihewi hangu kuvyajwani kwakwe. Kula nsiku ekitsukujwa akawekwa hapfa muḍyangoni, ili ayombe fwedha kwa hawaḍe wantu weowakikaa na kunjia Hekaluni.
- <sup>3</sup>Epfomuona Peṭero na Yohana wakwakunjiani Hekaluni, kawayomba wamumpe fwedha.
- <sup>4</sup>Wamuḍeḍea gu huyu kihewi, makisa Peṭero kamwamba, “Ṭahuyowe!”
- <sup>5</sup>Ḍubva kawaperukia akiyoweeya kupata kintu kuyawa kwao.
- <sup>6</sup>Ela Peṭero kamwamba, “Si fwedha wala dhahaḅu za kukupfa. Ela nakupfa hikiḍe nichonacho: Kwa sari ḍya Yesu Kiristo jwa Nazareti nyakukwambiani, nuka wenende!”
- <sup>7</sup>Makisa kamugija mukonowe wa kuyume, kamusumamisa wima. Iyo saa maguuye na ngolokolaze zikumiiya.
- <sup>8</sup>Katsumpiiya dzuu, kasumama, kaḍabva kudzyenendea. Makisa kagijana nao wanjia Hekaluni, akyenda na kutsumpa-tsumpa huku akimushaḍa Muungu.
- <sup>9</sup>Ṭuṭa yonse ya wantu wamuona akiwa kwenendani na kumushaḍa Muungu.
- <sup>10</sup>Wepfohambuya kwamba ni huyuḍe muntu eyeakikaa hapfaḍe pfa hu Muḍyango Mwema wa Hekalu akiyomba-yomba, wamaka na kuṭaḅanka kwa haya yamuhendekeeyo.
- <sup>11</sup>Huyu kihewi kamumaṭana gu Peṭero na Yohana akwakwenendani. Na wantu wonse wamaka, na wawaḍaramia haṭa uani kwikonahanwa Ua ḍya Sulemani.
- <sup>12</sup>Peṭero epfowaona hawa wantu, kawamba, “Wantu wa Isiraeli, kuṭi mumakiswa ni hiḍi dzambo? Munahuḍeḍea muna? Mwakuṭarani kwamba nguvu zehu wenye ambu udheru wehu ndiwō uhuwezeseyeo kumuhendeza ayu muntu enende?”
- <sup>13</sup>Huyu Muungu jwa wabibi zehu aḍe Iburahimu, Isaka na Yakobo, kamurembosa Yesu, eye muhumisijwe. Mumungiza mikononi mwa wakuu wehu, nanywi mumudziza usoni ya Pilato, haṭa Pilato epfohuna kumuyatsa huru.
- <sup>14</sup>Yesu ewa kayawa kwa Muungu na ewa muhachi, ela nywinywi mumudziza. Ishinu mumuyomba Pilato amumufungwiye muntu eyekuwa muyaji.
- <sup>15</sup>Ndookomu mumuyaga huyu jwa kuyanga wantu maisha kindindi. Ela Muungu kamufufuya kuyawa kwa wafu. Naswi haya huyaona na matso yehu wenye.

<sup>16</sup>Nguvu za sariḍye ndizo zimumpiyezo huyu kihewi mumanyiyee na mwiye kuonani, kukumiiya maguuye. Faro yehu kwa Yesu ndiyo imumpiyeyo kuwa na matsea, dzevihivi mwivyokumuonani nyonse.

<sup>17</sup>Ḍubva wandugu zanguni, nimanya ya kwamba haya mumuhendeeyo Yesu nywinywi na wakuu wenu, muyahenda pfasipfo kuimuka mwiyoumukihenda.

<sup>18</sup>Koro Muungu ewa kavilalabva kae na manwa ya manabii wakwe wonse kwamba huyu Mutsanwa jwakwe adzeyemuyeha, ni haḍi aoneswe tsungu. Nae Muungu kayatimiza haya aneneyeyo kwa hivi vyenu muhendeyeyo.

<sup>19</sup>Ḍubva pfyehuzani mama, na mumuujie Muungu, ili apate kumuyatsia nabvise zenu.

<sup>20</sup>Hendani hivyo ili Ḑwana amumpe ngera za kuyavya hara myojoni mwenu na pia amumuhumiye kawii Yesu, eye Masiya amumutsaniyee hangu ḍura.

<sup>21</sup>Ni haḍi ahafe mbinguni haḍa ngera ya mambo yonse ya kuhendwa mapfya idzefofika, dza vya Muungu evyonena kuchiiya na kwa manabii wakwe, hangu kae na kae.

<sup>22</sup>Koro Musa kamba, 'Ḑwana Muungu jwenu kadzamuhumia nabii dzami, jwa kyeeti chenu wenye. Ni musikiiye kula adzechonena.

<sup>23</sup>Yudejwonse asisikia vyyuwo vya huyo nabii anaḥanywa na wantu wa Muungu na kunangwa.'

<sup>24</sup>Manabii wonse, hangu Samweli haḍa hawa wamuḥiyeyo nyuma, wewa na hi hii ḍaamisa na walalabva haya mambo yadzeyohendeka hizi hizi nsiku.

<sup>25</sup>Mu wana wa hawa manabii na waḍala wa ḍamano ḍya Muungu ahendeedyo na wabibi zenu. Dza evyonena na Ibrahimu akimwamba, 'Kuchiiya na kwa yuyeejo, navivodhya vyeeti vyonse vya humu lumwenguni.'

<sup>26</sup>Ndookomu Muungu kamutsana na kumuhuma nguzi muhumisijwe kwenu Amuvodhye kwa kumuhendeza nyonse mupfyehuze njia zenu nzuka."

#### **Mahendo 4**

<sup>1</sup>Peḥero na Yohana wepfowakinena na hawa wantu amaale, wadzijwa ni wakohani, Mukuu jwa wamia Hekalu na Masaḍukayo.

<sup>2</sup>Wewarejea hawa ntumi wowii kwa dzambo ḍya kwamba wekiyongweeza wantu kwamba Yesu ewa kafufuka kuyawa wafuni, dzambo ḍiyangiyedyo kwamba wafu wadzafufuka.

<sup>3</sup>Ndookomu wamugija Peḥero na Yohana, ela kwa dzambo ḍya kwamba iwa imaawa kioro muno, wawangiza gerenzani haḍa chamukoche.

- <sup>4</sup>Kenge wantu wenji wasikiiyeo haya ya Peṭero na Yohana wasumwiiyeyo, wayahikiza. Ndookomu wayume wamuhikiziyeyo Kiristo wenjipfa haṭa wafika chima cha elefu nsano.
- <sup>5</sup>Chamukoche, hawa Wakuu wa Wayahuḍi, wazee na waalimu wa Sharia wadziana pfamodza Yerusalemi.
- <sup>6</sup>Waṭuṭaa pfamodza na Mukohani Mukuu Anasi, pfamodza na Kayafa, Yohana, Alekizanda na wangine weokuwa wa sindo wa Mukohani Mukuu.
- <sup>7</sup>Wawaweka hawa ntumi usoni yao na wawakora wawamba, “Ayu kihewi mumuhendadze haṭa aweze kwenenda? Muvihenda na nguvu za ga, ambu na sari ḍya ga?”
- <sup>8</sup>Ḍubva Peṭero, akiwa kadzaa Ruhu Mudheru, kawambukuya kamba, “Wakuu na wazee wehu,
- <sup>9</sup>kwa kwamba mwakuhukorani yeo dzuu ya hendo dzema ahendeejweḍyo huyu kihewi na namuna apfozejwevyo,
- <sup>10</sup>ḍubva ni mumanye na wantu wonse wa Isiraeli wamanye kwamba huyu muntu kasumama usoni yenu hapfa. Nka untu uḍewonse kwa nguvu za Yesu Kiristo jwa Nazareti, huyu mumupfatsikiye na Muungu akimufufuya kuyawa wafuni.
- <sup>11</sup>Yesu ndiye jwa haya matsoro yambiyee, ‘Hiḍi iwe muḍidziziyeyo nywinywi wambaka, ndiḍyo ḍigaliyeyo iwe muhimu ḍya kumbakia.’
- <sup>12</sup>Mupfonyo ntaupatikane kwa yuḍejwonse yungine lamuḍa kwakwe jeje hekeṭu. Koro lumwengu yuzima, ntaku yuḍejwonse yungine jwa Muungu ayavize sariḍye kuwa Mupfonyo wehu.”
- <sup>13</sup>Hawa wazee we bokoli wepfomusikia Peṭero na Yohana wakwakunenani pfasipfo oga na wepfororoṭa kwamba wewa wantu wasiosoma muno, wamaka. Wahambuya kwamba katsi wekikaa na kugijana na Yesu.
- <sup>14</sup>Ela weewa watsowa cha kunena, koro wamuona huyu muntu apfozejwe akiwa kasumama hapfaḍe pfamodza nao wowii.
- <sup>15</sup>Ndookomu wamuamuru Peṭero na Yohana wanuke hapfaḍe gasani, makisa waḍabva kuuzanya wao na wao.
- <sup>16</sup>Wauzana wamba, “Awa wantu awa huwahendedze? Kula muntu eyekuishini Yerusalemi kamanya ya kwamba haya mafara makuu ya kumakisa wayahenda wao. Naloo naswi ntahunaweza kuvikana.
- <sup>17</sup>Kenge nahuwakanye watseenena kawii meshi na yuḍejwonse, kwa sari ḍya Yesu. Na kwehii njia hunadiḍangara hiḍi dzambo ḍitṣeḍachaa zaiḍi wantuni.”
- <sup>18</sup>Ndookomu wawahana gasani kawii, na wawamba watseenena ambu kuyongweeza kawii meshi kwa sari ḍya Yesu.

- <sup>19</sup>Ela Petero na Yohana wawambukuya wawamba, “Hunani nywinywi wenye, vivyo hachi kuhenda usoni kwa Muungu, kahi ya kumuṭii nywinywi na kumuṭii Muungu.
- <sup>20</sup>Koro ikwaakwamba ndiswi, ntahuṭoweza kuyatsa kunena haya huoneyeyo na kusikia swiswi wenye.”
- <sup>21</sup>Hi gasa iwakanya vyumuni, makisa iwayatsa wende. Ntawakuweza kuwahukumu, koro wantu wonse wewa kumushadani Muungu kwa haya yahendekeeyo.
- <sup>22</sup>Huyu muntu eyepfonywa ewa na zaiḍi ya myaka miyongo mine.
- <sup>23</sup>Petero na Yohana wepfoyatsigwa huru ṭu, wauja kiṭaroni mwao wenda wayavya maagu dzuu ya hayaḍe wambiijweyo ni hawa wakohani wakuu na wazee.
- <sup>24</sup>Wepfosikia haya maagu, watsanganika pfamodza kumuyomba Muungu na umodza wakyamba, “Ḑwana na Muumba jwa mbingu na nsi, rukanga na vyonse vivyo kuzimuye!
- <sup>25</sup>Kwa njia ya Ruhu Mudheru, kunena na kanwa ka bibi jwehu Ḑauḍi eye muhumisiwo, epfokwamba, ‘Kuṭi wantu wa vyeeti wana ngoro? Na kuṭi wanapanga mambo yasiyowa?’
- <sup>26</sup>Mahaju ya lumwengu yadziweka ṭayari, na waṭawala wadziyana pfamodza, kujwana na Ḑwana Muungu na Masiya jwakwe.’
- <sup>27</sup>Ndivyo ḍugha, koro Herode, Pontio Pilato, wantu wa vyeeti na wantu wa Isiraeli wekudziana pfamodza humu mudzini, kumupfinga huyu muhumisi jwako mudheru, Yesu Masiya.
- <sup>28</sup>Weṭuṭaa kuhenda kula kintu uhuniyecho hangu ḍura kwa nguvuzo na miroyo mwenye kwamba vinawa.
- <sup>29</sup>Ne saasambi Ḑwana, ṭayowa oga weokuhungizani. Ḑubva hupfe swiswi wahumisiwo, kusumwiiya chuuwocho pfasipfo oga.
- <sup>30</sup>Gonzowa mukonowo kupfonya wajwazi. Henda vihambwiizo na mambo ya kumakisa kuchiiya kwa muhumisiwo mudheru, Yesu.”
- <sup>31</sup>Wepfokwisa kuyomba, hapfa pfantu waṭuṭaiyepfo pfasukusika. Wonse wadzajwa ni Ruhu Mudheru na waḍabva kusumwiiya chuuwo cha Muungu pfasipfo oga.
- <sup>32</sup>Hichi kiṭaro cha hawa wahikiza kiiwa dza muntu mumodza maṭaroni na myojoni mwao. Ntaku afalamiye kijache kuwa chakwe jeje heketu. Kula mumodza katumia na mwenziwe hichi echokuwa nacho.
- <sup>33</sup>Hawa ntumi wasumwiiya na nguvu nyinji dzuu ya kufufuka kwa Ḑwana Yesu. Na Muungu kawavodhya wonse muno.



<sup>34</sup>Ntaku eyekuwa na t̄uri wa kiḁechonse. Koro hawaḁe weokuwa na makonde ambu madzumba, wekiyaguza, na hizi fwedha

<sup>35</sup>wakawapfa hawa ntumi, zikagawijwa kula mumodza, chima cha haḁya yakwe.

<sup>36</sup>Kwiwa na Mulawi jwa kuyawa Kupuro eyeakihanwa Yusufu. Hawa ntumi wekimuhana Baranaba. (Maana ya Baranaba ni muntu eyenangiza moja.)

<sup>37</sup>Nae ewa na nkonde, na zizo ngera kaiguza, makisa hizi fwedha kaziwapfa hawa ntumi.

## **Mahendo 5**

<sup>1</sup>Ela kwiwa muntu saridye ndiye Anania. Ewa na muke eyeakihanwa Sifira. Nao waguza nkonde yao.

<sup>2</sup>Kenge Anania kadziwekea sehemu ya hizi fwedha, huku mukaziwe akiwa kavimanya tswee, makisa hizi zingine ndizo apfiyezo hawa ntumi.

<sup>3</sup>Peḁero kamuuza kamwamba, “Anania, kuḁi kumuyatsa Shaaḁani auheke mojawo na akuhendeze umukulekule Ruhu Mudheru kwa kudziwekea sehemu ya hizi fwedha upatiyezo wipfoiguza hi nkondeyo?”

<sup>4</sup>E nkonde usidzaiguza, ntaiwa yako? Na haḁa wipfoiguza, hizi fwedha undezihendea viḁevyonse utsakiyevyo. Kuḁi ḁubva, kuhuna mojoni mwako kuhenda dzambo dza hiḁi? Nkukukulakula mwanaaḁamu, ela kumukulakula Muungu!”

<sup>5</sup>Anania epfosikia haya t̄u, kagwa kafwa. Makisa kudza worani waulinga-linga hu mwiiwe, wanuka nao wenda wauzika. Wantu wonse wasikiyeo hiḁi dzambo wanjiwani ni oga muno.

<sup>7</sup>Kwipfochia kiḁemo cha chima cha masaa mahahu, mukaziwe kanjia humuḁe kuzimu pfasipfo kumanya haya yamuhendekeeyo muumewe.

<sup>8</sup>Peḁero kamuuza kamwamba, “T̄anyambia, achi ndicho chima mupatiyecho, mwipfoiguza e nkonde yenu?” Ae kamwambukuya kamwamba, “Ee, ni hiyo mala.”

<sup>9</sup>ḁubva Peḁero kamwamba, “Kuḁi wewe na mumeo muhuna kumuḁema Ruhu jwa ḁwana? Hawa wantu wamuzikiyeo mumeo hivi wa hapfo muḁyangoni, na wadzakuhwaa nawe.”

<sup>10</sup>Iyo saa, Sifira kagwa hafufi na maguu ya Peḁero kafwa. Hawaḁe worani wepfonjia, wamuḁonga kamaafwa. Ndookomu wayawa nae nze, wenda wamuzika hafufi na muumewe.

<sup>11</sup>Tsanganiko ḁyonse pfamodza na wantu wonse wasikiyeo haya mambo wanjiwani ni oga muku.

- <sup>12</sup>Hawa ntumi wahenda mafara ya kumakisa na vihambwiizo kahi ya hawa wantu. Hawa wahikiza wonse wekitsanganika pfamodza uani mwa Sulemani.
- <sup>13</sup>Ntaku yudejwonse asikwaa muhikiza, eyeweza kugijana nao. Haṭa vivyo, wantu wangine wasiokuwa wahikiza wekiwahila muno.
- <sup>14</sup>Wake na wayume zaiḍi wamuhikiza Bwana, na hichi kiṭaro cha wahikiza chikuya.
- <sup>15</sup>Kwa dzambo ḍya haya mambo ya hawa ntumi weyowakihenda, wantu wekitsukuya wajwazi na kuwayavya majiani na kuwaṭambaarya maṭaṭani na misalani ili nangaa hichi kivwii cha Peṭero chiwafinikize wangine wao, akiwa kuchiani.
- <sup>16</sup>Na viṭaro vya wantu wadza kuyawa midzi iizingiyeyo Yerusalemi. Wayeha wajwazi wao na hawaḍe weokuwa na mpepfo nzuka, na wonse wapfozwa.
- <sup>17</sup>Kenge huyu Mukohani Mukuu na wenziwe wonse, wa kiṭaro cha hapfahapfaḍe cha Masadukayo, wawafwiya ḍea muno hawa ntumi.
- <sup>18</sup>Ḍubva wawagija hawa ntumi na wawangiza gerenzani.
- <sup>19</sup>Ela huḍe sikuwe, malaika jwa Bwana kawafungwiiya miḍyango ya gerenza, kawayongowa haṭa nze. Kisa kawamba,
- <sup>20</sup>“Endani mukasumame Hekaluni, muwasumwiiye hawa wantu kula kintu dzuu ya haya maisha yenu mapfya.”
- <sup>21</sup>Hawa ntumi wauḅa haya wambiijweyo ni huyu malaika. Ḍubva magura mapfema, wanjia humu Hekaluni waḍabva kuwayongweeza hawa wantu. Huyu Mukohani Mukuu na hawa wenziwe wahana gasa yonse ya wakuu wa Kiyahuḍi. Makisa wahuma wantu kwendawahwaa hawa ntumi gerenzani, wawapfiike gasani.
- <sup>22</sup>Ela wepfofika, ntawakuwaona hawa ntumi humuḍe gerenzani. Ndookomu wauja wenda waipfa maagu hi gasa,
- <sup>23</sup>wamba, “Hwipfofika hukuḍe gerenzani, huiṭonga hi miḍyango ifungwa gu na huwaṭonga na hawa wamia wakiwa kwamiani miḍyango. Ela hwipfofunguya hi miḍyango ntahukuona muntu humuḍe kuzimu!”
- <sup>24</sup>Huyu mukuu jwa wamia wa Hekalu na hawa wakohani wakuu wepfosikia hivi, waḍabva kumamaṭa haya yawahendekeeyo hawa ntumi.
- <sup>25</sup>Makisa kudza muntu, kawamba, “Mumanya! Hawa wantu mungiziyeo gerenzani, waa Hekaluni wakuwayongweezani hawa wantu.”
- <sup>26</sup>Ḍubva huyu mukuu jwa wamia wa Hekalu na wantuwe wenda wawahwaa hawa ntumi. Ela ntawakuwahwaa na nguvu koro wekiwashooga hawa wantu watsewabiga na mawe.

<sup>27</sup>Wawayeha hawa ntumi usoni ya hi gasa, na huyu Mukohani Mukuu kaḁabva kuwauza vyuuwo.

<sup>28</sup>Kawamba, “Ntahukumuseresa kwamba mutseyongweeza kwa sari ḁya Yesu? Ela ṭayowani haya muhendeyeyo! Ishinu muidzaza Yerusalemi nzima na mayongweezo yenu. Na mwakutsakani kuhufwariza kwamba ndiswi humuyagiyeo!”

<sup>29</sup>Peṭero na hawa ntumi wangine wambukuya wamba, “Ni haḁi humuṭii Muungu, ela si wanaaḁamu.

<sup>30</sup>Muungu jwa wabibi zehu kamufufuya kuyawa wafuni huyu Yesu muyagie kwa kumupfatsika muhini mwa mpatsa.

<sup>31</sup>Huyu ndiye apfazijwe haṭa mukono kuyume wa hila wa Muungu, dza haju na mupfonya, ili awawezese wantu wa Isiraeli wapfyehuze mama na wayatsijwe nabvise zao.

<sup>32</sup>Swiswi na huyu Ruhu Mudheru, jwa Muungu eyenapfa hawaḁe weonamuṭii, hu mashaahiḁi wa haya mambo.”

<sup>33</sup>Hawa wazee wa hi gasa wepfosikia hivi, wareja muno haṭa wahuna kuwayaga hawa ntumi.

<sup>34</sup>Ela Mufarisayo mumodza ahanijwe Gamalieli, eyekuwa mwaalimu jwa Sharia eyeakihilwa muno ni wantu kasumama hapfaḁe gasani. Kayomba hawa ntumi wanujwe kachuchu hapfaḁe gasani.

<sup>35</sup>Makisa kayambia hi gasa, “Wantu wa Isiraeli, manyani, haya mwiyoḁakutsakani kuwahendea hawa wantu.

<sup>36</sup>Kakae kachuchu kwiiṭupuka muntu eyeakihanwa Theuda. Kadzihana muntu mukuu, na wantu chima cha magana mane wamuuḁa. Ela kayagwa, na wonse wamuuḁiyeo waṭamisaa-ṭamisaa, na kiṭaroche chaara.

<sup>37</sup>Nyumae, huyu Yuḁa jwa Galilaya kaṭupuka ngera ya kuṭalwa kwa wantu. Nae kapata kiṭaro cha wantu wamuuḁiyeo. Ela nae kayagwa, na wantu wonse wamuuḁiyeo waṭamisaa-ṭamisaa.

<sup>38</sup>ḁubva, dzuu ya hiḁi dzambo ḁya hi saasambi, namutsewahenda kiḁechonse hawa wantu. Wayatseni na shuuli zao. Koro ikiwa kwamba haya ni maṭaro na kazi ya mwanaaḁamu inakwaara yenye.

<sup>39</sup>Ela ikiwa kwamba ni kazi ya Muungu, ntamuṭoweza kuinanga. Mudzaroroṭa kwamba mwakujwanani na Muungu!” Hi gasa ihwaa haya maghaghisa ya Gamalieli.

<sup>40</sup>Ndookomu wawahana hawa ntumi hapfaḁe gasani, wayavya amuri kwamba wabigwe na lucha, na wawaseresa kutsanena kawii meshi kwa sari ḁya Yesu. Makisa wawayatsa huru.

<sup>41</sup>Hawa ntumi wanuka hapfaḍe gasani wakiwa na tsekea nkuu, ya kwamba Muungu kawatsana wakuntiswe ḍina kwa dzambo ḍya sari ḍya Yesu.

<sup>42</sup>Na kula nsiku, wekyenda madzumbani mwa wantu na Hekaluni, kuyongweeza na kusumwiiya Maagu Mema dzuu ya Yesu kwamba ndiye Masiya.

## **Mahendo 6**

<sup>1</sup>Hichi kiḱaro cha wahikiza chipfogija kukuya, nyumae kujumuka matsowano kahi ya hawaḍe weowakinena Kiyunani na hawaḍe weowakinena Kieburania. Hawa Wayahuḍi weowakinena Kiyunani wamba kwamba wake wachiwa wao ntawekimuudamijwa kwa haḍya zao za kula nansiku.

<sup>2</sup>Ndookomu hawa ntumi kumi na wawii wakihana pfamodza kiḱaro chonse cha wahikiza na wawamba, “Si hachi kwehu kuyatsa kusumwiiya chuuwo cha Muungu hukaiye kuyowa haḍya za wantu.

<sup>3</sup>Ḍubva wandugu zehu, tsanani wantu wafungahe weonahikizika kahi yenu, wadzazijweo Ruhu Mudheru na karo. Naswi hunawapfa hi hii kazi.

<sup>4</sup>Ḍubva aswi, hunamuudamiya mayombo na kazi ya kusumwiiya.”

<sup>5</sup>Kiḱaro chonse cha wahikiza kitsakizwa ni hiḍi ḱaro. Ndookomu wamutsana Siḱefano, muntu eyekuwa na faro nkuu na adzaiye Ruhu Mudheru. Wamutsana na Filipo, Porokoro, Nikanora, Timona, Paramena na Nikolao jwa kuyawa Antiokia eyenja ḍini ya Kiyahuḍi.

<sup>6</sup>Wawaweka hawa wantu usoni kwa hawa ntumi, nao wawayombea na kuwapfaza mikono.

<sup>7</sup>Ndookomu chuuwo cha Muungu kigija kuḍachaa kula pfantu. Chima cha wahikiza huko Yerusalemi chongezeka muno, na wakohani wenji wayahikiza haya Maagu Mema.

<sup>8</sup>Siḱefano, muntu eyekuwa na winji wa ḱei ya Muungu na adzaiye nguvu, kahenda mafara makuu ya kumakisa na vihambwiiizo kahi ya hawa wantu.

<sup>9</sup>Ela wantu wangine washindana nae. Wewa wantu wa sunagogi ḍihanijweḍyo “Sunagogi ḍya wantu huru,” ḍiḍyokuwa na Wayahuḍi wa Ukirene na Alekizandaria. Wao na Wayahuḍi wangine kuyawa Kilikia na Asia waḍabva kuḍaaḱiana na Siḱefano.

<sup>10</sup>Ela ntawakumuweza kwa yuḍaaḱo, koro Ruhu Mudheru kamumpa karo wa kunenea.

<sup>11</sup>Ndookomu wawangiza wantu nsunziirya wambe, “Humusikia Siḱefano akiwa kunenani mambo mazuka dzuu ya Musa na dzuu ya Muungu!”

<sup>12</sup>Kwa hi hii njia wawatsunziirya hawa wantu, wazee na waalimu wa Sharia. Ḍubva wadza wamugija Siḱefano, wamupfiika usoni ye gasa.

<sup>13</sup>Makisa wahwaa wantu wendeyeo wakiyavya ushaahiḍi wa nsuwe wakyamba, “Huyu muntu huyu, meshi kakuneneani mazuka dzuu ya Hekalu yehu ḅerū na dzuu ya Sharia ya Musa.

<sup>14</sup>Humusikia akyamba huyu Yesu jwa Nazareti anainanga hi Hekalu na kuperuya maḁa yonse huyongweezejweyo ni Musa!”

<sup>15</sup>Hawa wonse wakaiyeo hapfaḁe gasani wamuḁeḁea Siḁefano gu, na wauona hu usowe ugala dza wa malaika.

## **Mahendo 7**

<sup>1</sup>Huyu Mukohani Mukuu kamuuzā Siḁefano kamwamba, “Ndivyo, avi vya hawa wantu wevyokukuḁiani navyo?”

<sup>2</sup>Siḁefano kambukuya kamwamba, “Wababa zangu na wandugu zangu, nipfindiiyani! Huyu Muungu mwenye nguvu kamuḁupukia bibi jwehu Ibrahimi epfokuwa Mesopotamia, asidzakwenda kuishini Harani.

<sup>3</sup>Kamwamba, ‘Nuka nsini mwenu, uwayatse wantu wa sindoni mwenu, na balabala ya babajo, wende haḁa nsi nidzeyokuyanga.’

<sup>4</sup>Ndookomu Ibrahimi kanuka nsi ya Wakalidayo, kenda kanjia kuishini Harani. Babajwe epfofwa, Muungu kamunuya Ibrahimi na Harani, kamuyeha hi hii nsi mwiyoḁukaani hi hii saasambi.

<sup>5</sup>Muungu nkakumumpa Ibrahimi haḁa kaḁinku ka hi nsi kawe kakwe mwenye. Ela kamuahiḁi kwamba anaimumpa, iwe yakwe na viḁukuḁukuyve, haḁa ingawa Ibrahimi ewa nkadzawa na mwana.

<sup>6</sup>Muungu emwamba, ‘Yuvyeejo judzaishi nsi ya genini, wadzekowa wahumwa. Wanahendegwa mambo ya kinyaya kwa myaka magana mane.

<sup>7</sup>Ela nachihukumu hichi kyeeti kiwahendezeyecho wahumwa. Kisa nidzawayavya na humo nsini nao wadzaniyomba hapfa hapfa.’

<sup>8</sup>Makisa Muungu kaweka ntinye iwe kihambwiizo cha hiḁi ḁamano. Ndookomu Ibrahimi kamuhinya mwanawe Isaka, nsiku ya nane ḁaḁa ya kuvyajwa. Nae Isaka kadza kamuhinya Yakobo. Yakobo nae kadza kawahinya hawaḁe wabibi zehu kumi na wawii.

<sup>9</sup>Hawaḁe wabibi wamufwiya ḁea ndugu yao Yusufu, na wamuguza akawe muhumwa Misiri. Ela Muungu ewa nae.

<sup>10</sup>Kamuyavyanya na ḁinaze zonse. Usoni kwa Farao, haju jwa Misiri, Muungu kamumpa Yusufu kutsakwa na kamumpa na karo. Haḁa Farao kamuweka kuwa mukuu jwa nsi na jwa nyumba ya kihaju.

<sup>11</sup>Makisa kunjia nzaa nsi yonse ya Misiri na Kanaani, iyeheyeo ḁina nkuu. Wabibi zehu ntawakuweza kudhumburya chakuḁya kiḁechonse.

- 12**Ndookomu Yakobo epfosikia kwamba Misiri kwiwa chakudya, kawahuma hawa wanawe, yani wabibi zehu, wende mweedha wa dura.
- 13**Wepfokwenda charo cha pfii, Yusufu kadzimanyisa kwa hawa wanduguzwe, na ndipfo pfa Farao adzepfoakiumanya sindo wa Yusufu.
- 14**Dubva Yusufu kamupfiikia daamisa babajwe, na sindowe wonse, wantu miyongo mifungahe na watsano, kawamba wende Misiri.
- 15**Makisa Yakobo kenda Misiri, endeekoakifwa jeje na wabibi zehu wangine.
- 16**Mii yao itsukujwa haṭa Shekemu, ipfozikwa mbeera ya Iburahimu agwiiyeyo kwa chima cha fwedha kuyawa kwa kyeeti cha Hamori.
- 17**Ngera ya Muungu ya kuṭimiza hiḍi ḍamano ḍyakwe na Iburahimu ipfofika hafufi, wantu wehu weokuwa Misiri wenjipfa.
- 18**Haṭa mwisowe, Misiri idabva kuṭawaligwa ni haju yungine asiyemumanya Yusufu wala kumufwanya kwamba ewa ga.
- 19**Kawakulakula wantu wehu na kuwahendea uyaji wabibi zehu kwa kuwasharuṭisa wawayatse wana wao nze ya madzumba yao ili wafwe.
- 20**Ndiyo ngera ya Musa, mwana ḥora muno usoni kwa Muungu, avyaijweyo. Kayejwa nyumbani mwa ise kwa myezi mihahu.
- 21**Wepfodhimwa kumufitsa amaale, wamuyatsa nze ye nyumba yao. Ela mwanamuke jwa Farao kamuhwaa na kamuyeya dza mwanawe.
- 22**Musa kayongweezwa mambo yonse ya ukaro wa Wamisiri, haṭa kahenda ḍubaṭa jwa vyuuwo na mahendo.”
- 23**Siṭefano kongeza kunena kamba, “Musa epfokuwa na myaka miyongo mine, kahuna kwendawaḍoya Waisiraeli wenziwe.
- 24**Kenda kamuona Muisiraeli akwakubigwani ni Mumisiri. Dubva katsumpa kumuvonea na kamuyaviza halo kwa kumuyaga huyu Mumisiri.
- 25**Echamba wantuwe wenye mbwakuimuka kwamba Muungu njwakumutumia jeje kuwayavya uhumwani. Kenge ntawakuimuka.
- 26**Chamukoche kaona Waisiraeli wawii wakiwa kujwanani, na kaḍema kuwakanya, kawamba, “Ṭasikiani, ntamukwaa wantu wamodza? Munajwana nywinywi na nywinywi muna?”
- 27**Ela huyuḍe eyeakimubiga huyu mwenziwe kamuḍaraba Musa geri, kamwamba, ‘Ni ga akuwekeye mukuu na ṭoibi jwehu?’
- 28**Unatsaka kuniyaga nami, dzevide umuyagiyevyo huyuḍe Mumisiri dzana?’
- 29**Musa epfosikia hivi, kaḍarama, kenda kanjia kuishini nsi ya Wamidiani, adzeekoakivyaa wanawayume wawii.

<sup>30</sup>Musa epfoishi hukude kwa myaka miyongo mine, katupukijwa ni malaika. Huyu malaika kamutupukia kitsoryani chichochikiguuka mabilibili hukude yuwandani, hafufi na Murima wa Sinai.

<sup>31</sup>Musa kamakiswa ni haya aoneyeyo, haṭa kadzikuntia hafufi na hiki kitsorya kukichimiza urembo. Ela kasikia idzwi ḍya Ḑwana

<sup>32</sup>ḍikimwamba, ‘Mimi ndimi Muungu jwa wabibizo, aḍe Iburahimu, Isaka na Yakobo.’ Musa kahehema na oga haṭa nkakudema kuchimiza kawii.

<sup>33</sup>Makisa Ḑwana kamwamba, ‘Vuya viyahuvyo, koro hapfa usumamiyepfo ni pfantu pfadheru.

<sup>34</sup>Niyaona mazuka ya wantu wangu weyokuhendejwani hukude Misiri. Nisikia chiiyo chao, nami nidzia kuwapfonya. Ḑubva nzoo nikuhume Misiri.’ “

<sup>35</sup>Siṭefano kongeza kunena amaale kamba, “Huyu Musa, ni yuyude jwa wantu wa Isiraeli wadziziyee, wepfokwamba, ‘Ni ga akuwekeye mukuu na ṭoibi jwehu?’ Huyu ndiye jwa Muungu ahumie dza mukuu na mupfonya, kwa ugijo wa huyude malaika amutupukiye humude mwa hiki kitsorya chichochikipfya.

<sup>36</sup>Kawayongowa wantu kuyawa Misiri, akihenda mafara ya kumakisa na vihambwiizo. Hivi kavihenda Misiri, ḥahari ya Shamu na hukude yuwandani kwa myaka miyongo mine.

<sup>37</sup>Musa ndiye awambiiye wantu wa Isiraeli, ‘Muungu kadzamuhumia nabii dzami, jwa kyeeti chenu wenye.’

<sup>38</sup>Musa ndiye eyekuwa pfamodza na wantu wa Isiraeli, wepfoṭuṭaa pfamodza hukude yuwandani. Ewapfo hukude pfamodza na wabibi zehu na pfamodza na huyude malaika aneneye nae murima wa Sinai. Ndiye apfegejwe vyuuwo vya Muungu vya moja, ahuyeheye.

<sup>39</sup>Kenge ndiye jwa wabibi zehu wadziziyee kumuṭii. Ishinu wamuḍaraba geri na waṭamani kuuja Misiri.

<sup>40</sup>Ḑubva wamwambia Haroni, ‘Hwelekanyize miungu, idzeyohuyongowa usoni kwehu. Koro huyu Musa ahuyavyie na Misiri, ntahudzi kwamba kapatwa ni ya.’

<sup>41</sup>Ndiyo ngera wadzihendeeyeo yumbo jwa mwana ngombe. Wajuvugiiya huju yumbo, na wahenda jila, kutsekea kwa kazi wahendeeyo wenye.

<sup>42</sup>Ela Muungu kanuka kahi yao, na kawayatsa wavunzie nkuhi nyoha za yuwinguni, dza vyorejwevyo chuoni mwa Manabii kwamba, ‘Wantu wa Isiraeli, simi haṭa mwiye mukinitsinzia waḍondo na kuniyavia mvuugiya, kwa myaka miyongo mine hukude yuwandani!

<sup>43</sup>Ela mwiitsukuya hema ḍya muungu jwenu Moloki, na yumbo jwa nyoha ya muungu jwenu Refani. Yewa maumbo mwelekanyiyeyo ili muyavunzie nkuhi. Na kwa dzambo hiḍyo namuhendeza munaḍaramiswa mumpaka usoni ya Babeli.’

- 44 Hukuḁe yuwandani, wabibi zehu wewa na hiḁi hema ḁiyangiyedyo kuwapfo kwa Muungu. ḁielekanywa dzeviḁe vya Muungu amuḁamiyevyo Musa, kwamba aḁielekanye na yuumbo ayangijwejo.
- 45 Nyumae, wabibi zehu wapfegejweo hiḁi hema ni wababa zao, weḁihwaa, wepfokwenda pfamodza na Yoswa na kuheka nsi ya vyeeti vya Muungu aḁaramisiyevyo wasidzaifika. ḁikaa hapfo haḁa ngera za ḁauḁi.
- 46 ḁauḁi ewa kamutsakiza Muungu. ḁubva kamuyomba amuruhusu kumumbakia kao Muungu jwa Yakobo.
- 47 Kenge Sulemani ndiye adzeyeakimumbakia nyumba.
- 48 Ela Muungu awee dzuu nkanaishi nyumba zimbakijwezo ni wantu. Dza vya nabii aneneyevyo akyamba,
- 49 ‘ḁwana kamba, yuwingu ndijo kiti changu cha kihaju, na lumwengu ndijo kibago cha maguu yangu. ḁubva ni nyumba ya namuna ga, mudzeyonimbakia mimi? Ni pfantu ga, pfangu nidzepfoyavya hara?’
- 50 Dzaambia haya haya yonse, si kazi ya mikono yangu?’
- 51 Nywinywi mwiwo na kimenudzi! Myojo yenu na masikio yenu ya dza ya hawa walumwengu. Mwa dza wabibi zenu; meshi munamudziza Ruhu Mudheru.
- 52 Ni nabii ga, asiyekuntiswa ḁina ni wabibi zehu? Wawayaga hawa manabii wa Muungu weolalabva kae kudza kwa muhumisijwe muhachi. Kadza, na hi saasambi mumuḁawanya na mumuyaga.
- 53 Ndinywi mupfegejweo Sharia ya Muungu, muiyeheejweyo ni malaika, ela ntamukuigija!”
- 54 Hawa wazee we gasa wepfosikia hivi, wareja na wamurhighia magego na ngoro.
- 55 Ela Siḁefano, akiwa kadzaa Ruhu Mudheru, kayowa yuwinguni dzuu na kaona marembo ya Muungu yakiwa kuyangaani. Kamuona na Yesu akiwa kwamba kasumama mukono kuyume wa Muungu.
- 56 Kawamba, “ḁayowani! Nyakuonani mbingu zipfenuka na Mwana jwa Aḁamu kasumama mukono kuyume wa Muungu.”
- 57 Gasa yonse ipfosikia haya, wayaḁucha haya masikio yao na maganza huku wakibiga vilele. Makisa dza muntu mumodza wamuguukia iyo saa,
- 58 wamugija, wayawa nae nze ya mudzi na wamubiga na mawe. Hawa mashaahiḁi waziyatsa nkanzu zao na muurani ahanijwe Sauli.
- 59 Wagija kumubiga na mawe huku akiwa kuyombani, akyamba, “ḁwana Yesu, ipfokeye ruhu yangu.”



<sup>60</sup>Makisa kavunza nkuhi na kaḅaa idzwi kuu kamba, “Bwana, nkudzoiwaṭalie nabvise yao hi!” Epfokwisa kunena haya kahuna nsoho.

## Mahendo 8

<sup>1</sup>Ae Sauli katsakizwa ni hiḁi hendo ḁya kumuyaga Siṭefano. Wantu weonamuhila Muungu, wenda wamuzika Siṭefano, na wamwiiya muno. Iyo nsiku, tsanganiko ḁya Yerusalemi, ḁiḁabva kukuntiswa ḁina nkuu. Sauli kagija kuḁema kuḁinanga hiḁi tsanganiko. Kenda nyumba kwa nyumba, akiwaḅaa mafururyo na kuwayavya nze hawa wahikiza, hangu wake haṭa wayume na kuwangiza gerenani. Hawa wahikiziyeo wonse waṭamisaa ḁanda zonse za Yuḁaya na Samaria, lamuḁa hawa ntumi.

<sup>4</sup>Hawa wahikiza waṭamisaiyeo, wenda kula pfantu wakisumwiiya hichi chuuwo.

<sup>5</sup>Filipo kenda mudzi wa Samaria na kawasumwiiya hawa wantu dzuu ya Masiya.

<sup>6</sup>Hivi viṭaro vya wantu wamupfindiia urembo. Wonse wamusikiia na waona haya mafara makuu ahendeyeyo.

<sup>7</sup>Mpepfo nzuka ziwayawa wantu wenji huku zikiḅaa madzwi. Wantu wenji wahinamfiyeo na virema, nao wapfozwa.

<sup>8</sup>Ndookomu kwiwa tsekea nkuu mudzini Samaria.

<sup>9</sup>Humuḁe mudzini kwiwa muntu eyeakihanwa Simioni, eyeakimakisa wantu wa Samaria na tsawiwe kwa muḁa. Kadzihwaa kuwa muntu jwa maana,

<sup>10</sup>na kula mumodza, hangu mukuu haṭa muchuchu wekimupfindiia muno. Wamba, “Huyu ndiye nguvu ya Muungu iyonahanwa, ‘Nguvu Nkuu.’ “

<sup>11</sup>Kamakisa wantu na tsawiwe kwa kiṭemo kiyeya mumpaka kula muntu ekikaa na kumupfindiia muno.

<sup>12</sup>Ela wepfohikiza nsumwiizi za Filipo dzuu ya Maagu Mema ya Uhaju wa Muungu na sari ḁya Yesu Kiristo, waṭopyegwa hangu wake haṭa wayume.

<sup>13</sup>Simioni mwenye nae kahikiza. Epfoṭopyegwa ekigijana na Filipo kula pfantu na kamakiswa ni vihambwiizo na mafara makuu yahendejweyo ni Filipo.

<sup>14</sup>Hawa ntumi weokuwa Yerusalemi wepfosikia kwamba wantu wa Samaria wahikiza chuuwo cha Muungu, wamuhuma Peṭero na Yohana kwao.

<sup>15</sup>Wepfofika, wawayombea hawa wahikiziyeo ili wamupfokeye Ruhu Mudheru.

<sup>16</sup>Koro Ruhu Mudheru ewa nkadzasukia haṭa mumodza jwa hawa wahikiziyeo. Wewa waṭopyegwa ṭu kwa sari ḁya Bwana Yesu.

<sup>17</sup>Makisa Peṭero na Yohana wawapfaza mikono hawa wahikiza, nao wamupfokea Ruhu Mudheru.

- <sup>18</sup>Simioni ewa kaona ya kwamba hawa wahikiza wepfopfazwa mikono ni hawa ntumi, wamupfokea Ruhu Mudheru. Dubva ekitsaka kuwapfa fwedha Peṭero na Yohana,
- <sup>19</sup>na kawamba, “Nimpani nami hizi nguvu, ili yuḑejwonse nidzeyemupfaza mikono amupfokeye Ruhu Mudheru.”
- <sup>20</sup>Kenge Peṭero kamwambukuya kamwamba, “Awe na fwedhazo namunjie mananzini, kwa kuṭara ya kwamba unaweza kuiguya ṭola ya Muungu na fwedha.
- <sup>21</sup>Nku fungu wala hachi kwa hi hii kazi, kwa dzambo ḑya kwamba mojawo si murongaaro usoni kwa Muungu.
- <sup>22</sup>Dubva, pfyehuza mamazo nzuka, na umuyombe Bwana, akuyatsie kwa kuwa na maṭaro dzayohayo.
- <sup>23</sup>Koro nikuona una wivu mwinji muno, na kuhenda mufungwa jwa nabvise!”
- <sup>24</sup>Simioni kambukuya kamba, “Namuyomba muniyombeye kwa Bwana, ili nitsefikwa ni haṭa dzambo modza, ḑya haya mwambiiyeyo kwamba yananifika.”
- <sup>25</sup>Wepfokwisa kuyavya ushuhuda dzuu ya Yesu Kiristo na kusumwiiya maagu ya Bwana, Peṭero na Yohana wauja Yerusalemi. Wepfowakiuja wenda na kusumwiiya Maagu Mema midzi minji ya Wasamaria.
- <sup>26</sup>Makisa malaika jwa Bwana kanena na Filipo kamwamba, “Dzielekanye, wende nsini haṭa njia ya yuwandani iyawiyeyo Yerusalemi kwenda Gaza.”
- <sup>27</sup>Ndookomu Filipo kadzielekanya, kachia. Iiḑe saa kwiwa muntu mukuu Muithiopia, eyekuwa kuujani nyumbani. Huyu ewa muntu aṭumijwe, muntu mukuu jwa kuṭunza nkandi ya malikia jwa Ithiopia. Ewa kayawa Yerusalemi kumuyombani Muungu, na ekiuja akiwa dzuu ya gari ḑyakwe ḑya kunuhwa.
- <sup>28</sup>Humu njiani, kaka humuḑe garini huku akiwa kudzisomeani chuo cha nabii Isaya.
- <sup>29</sup>Dubva Ruhu Mudheru kamwambia Filipo, “Enda hafufi na hiḑiḑe gari ukagijane naḑyo.”
- <sup>30</sup>Filipo kaḑiḑaramia hafufi hiḑiḑe gari na kenda kamusikia huyuḑe muntu kakusomani chuo cha nabii Isaya. Dubva kamuuza kamwamba, “Amevihivi kwakuimukani maana ya haya wiyokusomani?”
- <sup>31</sup>Huyuḑe muntu kamwambukuya kamba, “Nawezadze kuimuka, ninkitsaawa na muntu jwa kunipfenwiiya?” Na kamuyomba Filipo apfae hapfaḑe garini dzuu, akae nae.
- <sup>32</sup>Hichi kiḑinku cha haya matsoro echoakisoma chamba hidzaa: “Ewa dza mbuzi ya hako iyokupfiikwani kutsinzwani. Ewa dza mwanambuzi jwa hako asiyeiya akwakupfeejwani ḑabasa ḑyakwe, na wala nkakwambukuya chuuwo.

<sup>33</sup>Kagizwa yutswa na kunyimwa hachiye. Na ntaku yudejwonse adzeyeweza kunena dzuu ya kivyaziche, kwa kwamba maishaye ya hapfa lumwenguni yasiya.”

<sup>34</sup>Huyu mukuu jwa Kiithiopia kamuuza Filipino kamwamba, “Tanyambia, ayu nabii ekinena dzuu ya ga? Ekinena dzuu ya muntu yungine?”

<sup>35</sup>Dubva Filipino epfoḃaa kanwa kunena, kaḃabva na chichiḃe kiḃinku cha matsoro na kamusumwiiya Maagu Mema dzuu ya Yesu.

<sup>36</sup>Wepfokuwa charoni amaale, wenda wakumpwiiya pfantu pfepfo na kibwola cha madzi. Na huyude mukuu kamba, “Hayano madzi. Ni kintu ga cha kuniḃidhya nitsetopyegwa?”

<sup>38</sup>Makisa huyu mukuu kaamuru hiḃi gari ḃisumamiswe, na wowii wasuka humu madzini, na Filipino kamuḃopya.

<sup>39</sup>Wepfoyawa nomu madzini, Ruhu jwa Ḃwana kamuhwaa Filipino. Huyude mukuu nkakumuona kawii, ela kagija charoche akiwa na tsekea.

<sup>40</sup>Filipo kadza kadziona ka Azoto. Na kenda akichia na midzi yonse na kusumwiiya Maagu Mema, haḃa kafika Kaisaria.

## **Mahendo 9**

<sup>1</sup>Zizo ngera, Sauli kadzaa voku wa kuwalacha wanafunḃi wa Ḃwana akitsaka kuwayaga. Kenda kwa Mukohani Mukuu

<sup>2</sup>na kayomba ḃaruwa za umanyizo kwa masunagogi yeyo Damasiko. Kahenda hivi ili kwamba akiona muhikiza yudejwonse jwa Njia ya Ḃwana hukude, akiwa muke ambu muyume, amugije na auje nae Yerusalemi.

<sup>3</sup>Kenge humu njiani, epfokuwa hafufi na Damasiko, ḃwikira kumwala muyanga na yuwinguni, umuyangaiyeo ḃanda zonse.

<sup>4</sup>Kagwa mutsangani na kasikia idzwi ḃimwambiyedyo, “Sauli, Sauli! Kuḃi kwakunionesani tsungu?”

<sup>5</sup>Sauli kauza kamba, “Ndiwe ga, Ḃwana?” Hiḃi idzwi ḃimwamba, “Ndimi Yesu wiyekunionesani tsungu.

<sup>6</sup>Ela nuka wima, wende huko mudzini udzekokwambijwa haya yakumaliyeyo kuhenda.”

<sup>7</sup>Hawa wantu weokuwa charoni pfamodza na Sauli, wahuka na wasumama, watsowa haḃa cha kunena. Koro weḃisikia hiḃi idzwi, kenge ntawakuona yudejwonse.

<sup>8</sup>Sauli kanuka wima na hapfa mutsangani, na kapfenuya matso ela nkakuweza kuona kiḃechonse. Dubva hawaḃe wantu wangine wamugija yuroi haḃa Damasiko.

<sup>9</sup>Kwa nsiku ntahu nkakuweza kuona. Nae ngera yonse hiyo, nkakuḍya nolawe kunwa kiḍechonse.

<sup>10</sup>Hukuḍe Damasiko kwiwa mwanafunḍi mumodza eyeakihanwa Anania. Bwana kamuhana nzozini kamwamba, “Anania!” Anania kamwambukuya kamba, “Ndimi huyu Bwana.”

<sup>11</sup>Nae Bwana kamwamba, “Dzielekanye wende haḥa njia iyonahanwa ‘Njia Ndongaaro,’ na hapfaḍe nyumbani pfa Yuḍa mulache muntu jwa Tariso eyenahanwa Sauli. Hi hii saasambi kakuyombani

<sup>12</sup>na kaona nzozini. Humu nzozini kamuona muntu eyenahanwa Anania kanjia humuḍe kuzimu, na kamuwekea mikono ili aweze kuona kawii.”

<sup>13</sup>Ela Anania kamwambukuya kamba, “Bwana, wantu wenji wesakunisumwiiya dzuu ya huyu huyu muntu na dzuu ya mambo mazuka yonse awahendeeyeo wantuwo hukuḍe Yerusalemi.

<sup>14</sup>Na kadza hapfa Damasiko, na ruhusa ya wakohani wakuu, awagije wonse weonakuvunzia nkuhi wewe.”

<sup>15</sup>Kenge Bwana kamwambia Anania, “Enda ṭu koro nimutsana kwa kazi ya muḍa, aḍihendeze sari ḍyangu ḍimanyikane kwa wantu wa vyeeti na kwa mahaju, na kwa wantu wa Isiraeli.

<sup>16</sup>Na mimi mwenye namuyanga menji yadzeyomumala kukuntiswa ḍina kwa dzambo ḍyangu.”

<sup>17</sup>Ḍubva, Anania kenda kanjia humuḍe nyumbani, na kamuwekea mikono Sauli. Kamwamba, “Ndugu Sauli, Bwana kanihuma, Yesu mwenye akuṭupukiyee humu njiani wipfokuwa kudzani hapfa. Kanihuma ili upate kuona kawii na kudzazwa Ruhu Mudheru.”

<sup>18</sup>Iyo saa, kugwa vija dza magamba nomu matsoni mwa Sauli na kaweza kuona kawii. Ḍubva kanuka wima na kaṭopyegwa.

<sup>19</sup>Epfodya chakuḍya, nguvu zimuujia. Sauli kakaa kwa nsiku kachuchu na hawa wanafunḍi hukuḍe Damasiko.

<sup>20</sup>Nkakukawa, kaḍabva kusumwiiya masunagogini akyamba, “Yesu ni Mwana jwa Muungu.”

<sup>21</sup>Wantu wonse wamusikiiyeo wamaka haḥa waḍabva kuuzana wao na wao wakyamba, “Huyu huyu si ayu muntu eyeakiwahenga awa wantu weowakiyomba kwa sari ḍya Yesu hukuḍe Yerusalemi? Siye eyekudza awagije wantu dzao awapfiike kwa wakohani wakuu?”

<sup>22</sup>Kenge Sauli, kwa nsumwiizi zakwe, kagija kuheka mama za wantu zaiḍi na zaiḍi. Kawayanga tswee hawa Wayahuḍi wa Damasiko, kwamba Yesu ndiye huyu Masiya, haḥa waḍanganika.

- <sup>23</sup>Kwipfochia kitemo kiyeya, hawa Wayahuḍi wahenda shauri ya kumuyaga Sauli.
- <sup>24</sup>Siku na musikahi wayamia hi miḍyango ya hu mudzi, wakimuindiiya wamuyage. Ela kapata mfunyenye ya haya wahuniyeyo kuhenda.
- <sup>25</sup>Na wanafunḍi wa Sauli wamuhwaa nasiku, wamuyavya na angani ḍiḍyokuwa jwedzini, na wamususya nsii na chikapfu.
- <sup>26</sup>Sauli epfokwenda Yerusalemi kaḍema kudzigijanisa na hawaḍe wanafunḍi. Ela wonse wekimushooga, koro wewa ntawadzahikiza kwamba kagala mwanafunḍi.
- <sup>27</sup>Kenge Baranaba, kamuhwaa kenda nae kwa hawa ntumi. Kawambia namuna ya Sauli amuoneyevyo Bwana humu njiani, na kwamba Bwana kanena nae. Kawambia na namuna ya Sauli asumwiiyevyo pfasipfo oga kwa sari ḍya Yesu, hukude Damasiko.
- <sup>28</sup>Ḍubva Sauli kakaa pfamodza nao na kwenda Yerusalemi nzima akisumwiiya pfasipfo oga kwa sari ḍya Bwana Yesu.
- <sup>29</sup>Kanena na kuḍaaḥiana na Wayahuḍi weonanena Kiyunani, ela kuḥwa wekitsaka kumuyaga.
- <sup>30</sup>Hawa wandugu wepfodimanya hiḍi dzambo, wamuhwaa Sauli, wamupfiika haḥa Kaisaria na wamugonzoza ende Tariso.
- <sup>31</sup>Ḍubva tsanganiko ḍiwa na ngera ya naghea Yuḍaya, Galilaya na Samaria yonse. Chima cha tsanganiko ḍimuhiliyevyo Bwana, ndiyo mala ḍikwiiyevyo na kwongezeka kwa kungizwa moja ni Ruhu Mudheru.
- <sup>32</sup>Iwa kwamba Peḥero epfoakichia huku na huku, ngera modza kenda haḥa kwa wantu wa Muungu weowakikaa mudzi wa Lida.
- <sup>33</sup>Hukude kaḥongana na muntu ahinamfiye eyeakihanwa Aneya. Nkakuweza kunanuka na hapfa ḥaḥani kwa myaka minane.
- <sup>34</sup>Peḥero kamwamba, “Aneya, Yesu Kiristo kakukupfozani. Nuka wima uḍihandike hiḍi ḥaḥaḍyo.” Mweedha Aneya kanuka wima.
- <sup>35</sup>Wantu weowakikaa Lida na Sharoni wepfomuona Aneya kapfozwa, wamuhikiza Bwana.
- <sup>36</sup>Hukude Yopa kwiwa na mwanafunḍi muke ahanijwe Tabita (Sariḍye kwa Kiyunani ndiye Dokasi, maanaye ni nkuyungu). Huyu muke meshi ekihenda mema na kuwagija masikini.
- <sup>37</sup>Hizo ngera, kahenda mujwazi na kafwa. Wantu waukosa hu mwiiwe na wauweka chumbani ḍarini dzuu.
- <sup>38</sup>Mudzi wa Yopa ntawiiwa kuye na Lida. Ḍubva hawa wanafunḍi weokuwa Yopa wepfosikia kwamba Peḥero ka Lida, wamupfiikia ḍaamisa na wantu wawii wamwamba, “Rebva udze huku.”

<sup>39</sup>Ndookomu Peṭero kadzielekanya na kagijana nao. Epfofika, kahwajwa kapfiikwa humuḁe chumbani ḁarini dzuu. Hukuḁe, Peṭero karingwa ni wake wachiwa wenji wakiwa kuiyani na kumuyanga nkanzu welekanyijwezo ni Dokasi epfokuwa moja.

<sup>40</sup>Peṭero kawayavya nomu chumbani wonse, makisa kavunza nkuhi kayomba. Kisa kachiperukia hichi kivimba na kamba, “Tabita, nuka wima!” Kapfenuya haya matsoye, na epfomuona Peṭero, kanuka chihako.

<sup>41</sup>Peṭero kamunyopezea mukono na kamugija asumame wima. Makisa kawahana hawa wantu wa Muungu na hawaḁe wake wachiwa, na kamuwapfa huyu muke akiwa moja.

<sup>42</sup>Haya maagu ya hiḁi dzambo yaḁachaa mudzi muzima wa Yopa, na wantu wenji wamuhikiza Ḃwana.

<sup>43</sup>Peṭero kakaa nsiku nyinji Yopa na muelekanya nchingo ahanijwee Simioni.

## **Mahendo 10**

<sup>1</sup>Hukuḁe Kaisaria, kwiwa muntu mumodza eyeakihanwa Koronelio. Jeje ewa ni mura jwa kiṭaro cha asikari wa Kirumi kihanijwecho, “Kiṭaro cha Uṭaliano.”

<sup>2</sup>Ewa muntu muchuuwo. Jeje na sindowe wonse wewa wantu weowakimuhila Muungu. Kahenda menji ya kuwasaiḁia Wayahuḁi masikini na kuṭwa ekimuyomba Muungu.

<sup>3</sup>Ndookomu nsiku modza, chima cha saa kenda za musikahi, Koronelio kaona nzozini. Humu nzozini, kamuona tswee malaika jwa Muungu kamudzia na kumuḁankuwa sari kamwamba, “Koronelio!”

<sup>4</sup>Ae kamuḁeḁea huyu malaika akiwa na oga na kamuuzwa kamwamba, “Kunaa Ḃwana?” Huyu malaika kamwambukuya kamwamba, “Muungu kapfokea mayombo yako na mvuugiyazo kwa masikini. Na huku ndiko kwambukuyakwe.

<sup>5</sup>Ḃubva huma wantu Yopa, wende wakamuhane muntu mumodza eyenahanwa Simioni Peṭero.

<sup>6</sup>Kakukaani dza mugeni nyumbani mwa muelekanya nchingo mumodza eyenahanwa Simioni. Nyumbaye ya geri ya ḁahari.”

- <sup>12</sup>Hwojeka mudzi wa Sirakuze, hwendeekohukikaa nsiku ntahu.
- <sup>13</sup>Hwipfonuka na hapfo, hwenda haṭa mudzi wa Regume. Chamukoche kuḍabva kubiga mpepfo na ḍanda ya nsini, na hufika ḅandari ya Putoli kwa nsiku mbii.
- <sup>14</sup>Hukuḍe hwenda huṭonga wahikiza, wahuyombeyeo hukae pfamodza nao kwa ḍyuma modza. Makisa hwenda Rumi.
- <sup>15</sup>Hawa wandugu wa Rumi wepfohupata maagu, wangine wadza wahuṭangera na hapfa pfa hu mudzi wiwonahanwa Marikiti ya Apiyo na wangine wadza wahuṭangera na hapfa pfa hu mudzi wiwonahanwa Nyumba ntahu za wageni. Paulo epfowaona, kamuyaviza asanṭa Muungu, na kanjia moja.
- <sup>16</sup>Hwipfofika Rumi, Paulo kayatsigwa adzikaiye pfaḍepfonse atsakiyepfo ela awe na asikari mumodza jwa kumwamia.
- <sup>17</sup>Kwipfochia nsiku ntahu, Paulo kawahana mukutanoni hawa wakuu wa Kiyahuḍi wa hukḍe. Wepfokudziana kawamba, “Ndugu zangu, mimi sikuwahendea uzuka uḍewonse wantu wehu ambu kudziza mila za wabibi zehu. Ela nihendezwa mufungwa Yerusalemi na ningizwa mikononi mwa Warumi.
- <sup>18</sup>Wanikora-kora na wekitsaka kuniyatsa huru, koro ntawakuona zuka ḍiḍeḍyonse nihendeyeḍyo ḍya kuniyagia.
- <sup>19</sup>Kenge wantu wangu wadziza niyatswe huru. Nami vinihendeza niyombe kwamba hi ḍubi yangu ikanenegwe ni Kaisari, haṭa nipfokuwa si kintu cha kuwaḍia nacho wantu wangu.
- <sup>20</sup>Ndiyo maana nitsakiyeyo kuonana nanywi na ninene nanywi. Koro mimi ni mufungwa kwa dzambo ḍya huyu Masiya eye madzikwaṭyo ya wantu wa Isiraeli.”
- <sup>21</sup>Ao wamwambukuya wamwamba, “Ntahudzapata ḅaruwa ziḍezonse dzuuyo kuyawa Yuḍaya, nolawe ntaku Muyahuḍi mwenzehu yuḍejwone adziye na maagu yaḍeyonse ambu kunena kiḍechonse kizuka dzuuyo.
- <sup>22</sup>Ela hundetsaka kusikiiya maṭaroyo. Koro humana ya kwamba kula pfantu wantu ntawakiṭaki hichi kiṭaro uicho.”
- <sup>23</sup>ḍubva wahuniyana nsiku ya kuṭongana na Paulo, na hiyo hiyo nsiku kwenda wantu wenji hapfa pfa Paulo epfoakikaa. Hangu magura haṭa mioro kanena nao na kuwaimusya dzuu ya Uhaju wa Muungu. Kaḍema kuwahendeza wahikize maagu dzuu ya Yesu akitumia Sharia ya Musa na matsoro ya manabii, kuyanga ya kwamba haya eyokunenani nza hachi.
- <sup>24</sup>Wangine wao wahikiza hivi vyyuwovye, ela wangine ntawakuhikiza.
- <sup>25</sup>Kwa kwamba wasidzanuka wagawikana haya maṭaro, Paulo kawamba, “Huyu Ruhu Mudheru kanena hachi, ephonena na kanwa ka nabii Isaya kwa wabibi zenu.

<sup>26</sup>Ewa kamba, 'Enda kwa hawa wantu, uwambe: Munapfindiia na kupfindiia, ela ntamuṭoimuka kintu. Munachimiza na kuchimiza, ela ntamuṭoona kintu.

<sup>27</sup>Koro vitswa vyenu vihenda vyumu, masikio yenu yahenda maziho, na mufinya matso yenu. Ela ṭambere si hivyo, matso yenu yandeona, masikio yenu yandesikia, akili zenu zindeimuka. Nanywi mundemuujiya Muungu, nae andemupfonya.' "

<sup>28</sup>Paulo kesa na kuwamba, "Ḑubva mumanye ya kwamba, maagu ya mupfonyo yapfiikijwa wantu wa vyeeti vingine. Wao wanayasikiya!"

<sup>30</sup>Paulo kaka hukuḑe kwa myaka miwii, akiwa kuishini nyumba adzikodishiiyeyo mwenye. Na ekimukarabisha kula muntu endeye na kumuyowa.

<sup>31</sup>Kasumwiiya dzuu ya Uhaju wa Muungu na kuyongweeza dzuu ya Ḑwana Yesu Kiristo, akinena pfasipfo oga wala kuingirwa ni muntu.

## Warumi

### Warumi 1

<sup>1</sup>Mimi Paulo, niiye muhumisi jwa Kiristo Yesu, nyakumworeani nywinywi wantu wa Rumi mwiwo wahikiza. Muungu kanitsana dza ntumi jwa Kiristo na kanimpa kazi ya kusumwiiya Maagu Mema yakwe.

<sup>2</sup>Muungu ewa kaahidi dzuu ya haya haya Maagu Mema hangu kae na kae kuchiiya na kwa manabii wakwe. Hawa hawa manabii ndiwo woreyeo haya haya mambo humu mwa haya matsoro madheru.

<sup>3</sup>Haya Maagu Mema ya Muungu aahidiyeyo ni dzuu ya huyu Mwanawe, avyaijwee dza mwanaadamu kuyawa sindo wa haju Daudi.

<sup>4</sup>Dzuu ya udheru wakwe wa kimuungu, Yesu Kiristo Bwana jwehu katanwa kuwa Mwana jwa Muungu eye na uwezo mkuu hapfaye epfufujwa kuyawa kwa wafu.

<sup>5</sup>Kuchiiya na kwa Yesu, Muungu kanivodhya niwe ntumi jwakwe, ili kwa dzambo dyakwe niwahendeze wantu wonse wasiokuwa Wayahuji wamuhikize na kumuji jeje.

<sup>6</sup>Haṭa nanywi pia mwaa humu longoni mwa hao hao wantu. Muhanigwa ili muweze kuwa wantu wa Yesu Kiristo.

<sup>7</sup>Ndookomu nyakumworeani nywinywi wantu wonse mwiwo Rumi. Nywinywi mu wantu mutsakijweo ni Muungu na akimuhana muwe wantuwe wadheru. Muungu Baba na Bwana jwehu Yesu Kiristo nawamuvodhye na kumumpa naghea nto.

<sup>8</sup>Nguzi cha dura namuyaviza duḍa Muungu jwangu kwa dzambo dyenu nyonse, kuchiiya na kwa Yesu Kiristo. Koro faro yenu mwiyonayo kwa Yesu Kiristo yakusumwiiwani lumwengu yuzima.

<sup>9</sup>Haṭa Muungu mwenye, huyu niyenamuhumikia na moja wangu wonse kwa kuyasumwiiya haya Maagu Mema dzuu ya huyu Mwanawe, kamanya kwamba nakaa nakumukumbuka nyonse

<sup>10</sup>kula nikwakuyombani. Nakaa nikamuyomba Muungu kwamba, ikiwa kwamba ni miroye, nangaa sasa animpe namfasi niweze kumuṭembeeya huko kwenu.

<sup>11</sup>Nina hamu ya kuonana nanywi muno ili niweze kudzamumpa mvoni ya kiruhu idzeyokumiiza hizi faro zenu.

<sup>12</sup>Yani nichokunenani ni kwamba, hunangizana nguvu kwa hizi faro zehu. Hi faro yangu inamungiza nguvu nywinywi, na faro zenu zinaningiza nguvu mimi.

<sup>13</sup>Wandugu zanguni, natsaka mumanye kwamba nikipanga muno kumuṭembeeya. Nikitsaka kudza nihende kazi ili kahi yenu nipate wantu wa

kumuhikiza na kumuuba Kiristo, dza vivide nihendeyevyo kahi ya wantu wa vyeeti vingine. Ela kula nikitsaka kudza, kunawa na kintu chichonanivingira kudza, na haṭa hi saasambi sidzapata namfasi.

<sup>14</sup>Nina muzigo wa kuyasumwiiya haya Maagu Mema kwa hawa hawa wantu wonse wa vyeeti. Hangu wasiṭaarabikiyeo na haṭa wasiosiṭaarabika, wasomeyeo na haṭa wasiosoma.

<sup>15</sup>Ndiyo maana nina hamu muno ya kudza nimusumwiiye nanywi nywinywi mwiwo Rumi.

<sup>16</sup>Mimi sione yutswa kuyasumwiiya haya Maagu Mema. Koro haya haya maagu ndiyo nguvu ya Muungu iyonawapfonya wonse weonayahikiza. Dura yasumwiiwa kwa Wayahuḍi na wapata mupfonyo, na sasa yakusumwiiwani kwa wantu wa vyeeti vingine, nao wakupfonywani.

<sup>17</sup>Koro hi injili inahuyanga wazi tswee namuna ya Muungu evyonawahwaa wantu kuwa wahachi usoni kwakwe. Muungu anamuhwaa muntu kuwa muhachi kuubana na hivide amuhikiziyevyo Muungu tu. Dza vya matsoro yaneneyevyo yakyamba, “Huyude jwa Muungu eyenamuhwaa kuwa muhachi kwa dzambo dya faroye, huyu anaishi maisha ya dughu.”

<sup>18</sup>Muungu kakuhuyangani wazi tswee kwamba karejeswa ni haya mazuka na nabvise zonse za wanaadamu wezonahenda. Kakuhuyangani kwamba anawahukumu na hukude mbinguni aiko, koro kwa haya mazuka yao weyonahenda, wanaikaiya machingama hi hachi itsemanyikana.

<sup>19</sup>Si ya kwamba ati ntawadzi kidetchonse kuhusu Muungu haṭa. Koro haya mambo ya kwamba wayamanye dzuuye, Muungu kesakuyawapfenwiiya wazi tswee.

<sup>20</sup>Hangu kuumbwa kwa lumwengu, wantu wesakuviona hivide vyonse vya Muungu aumbiyevyo. Yani kuchiiya na kwa hivi aumbiyevyo, wanaadamu wesakuuona hu Umuunguwe na uwezowe usiwo chima, ingawa jeje mwenye nkaonekane na matso. Ndookomu ntawa kipfangizo kidetchonse cha kutsamuṭii Muungu!

<sup>21</sup>Koro ingawa wamanya kwamba kuna Muungu, ntawakae na kumuhila dza evyonamala kuhilwa, na wala ntawakae na kumuyaviza dudu. Ishinu wagala kutara mambo ya upuudhi muhupfu, na ntawaimuke kintu koro akili zao ziwanzia kiza.

<sup>22</sup>Wanakaa na kudziona kwamba ni makaro, na hali huku ni maḍyura.

<sup>23</sup>Badala ya kumuyomba huyu Muungu mwenye nguvu eyenaishi maishi, wananjia kuyombani miungu ya masanamu. Hi miungu yao ingine ni masanamu ya wanaadamu, na hali mwanaadamu ni kiumbe chichonafwa kikawowa! Miungu yao ingine ni masanamu ya nyuni ambu ya wadondo wangine garagara.

<sup>24</sup>Ndookomu Muungu kawayatsa nangere wadzihendeye haya mambo yao machafu weyonadzisikia kuhenda. Nao wanakaa na kuhendeanamambo machafu wao na wao.

<sup>25</sup>Hi hachi dzuu ya Muungu wanaiperuya ikawa nsuwe. Wanakaa na kuviyomba na kuvihumikia hivi vija vya Muungu aviumbiyevyo, badala ya kumuyomba huyu aviumbiye jeje mwenye! Jeje ni Muungu eyenamala kushadwa haṭa pfasipfosia. Amina.

<sup>26</sup>Kwa dzambo d̄yevihivi, Muungu kawayatsa wauḃe hizi ṭamaa zao nzuka nzuka za kimwii. Wake wangine wakuyaani na wake wenzao na hali Muungu nkakuumba kwamba vihendeke dzevyohivyo.

<sup>27</sup>Hawa wayume nao wanayatsa hi njia ya sawa ya muke na muyume, wakanjia ṭamaa ya kuyaana wao na wao. Wayume kwa wayume wanakaa na kuhendeanamambo machafu machafu. Ndookomu wanadzingizia kuhukumigwani dza wevyonamala, kwa dzambo d̄ya haya mahendo yao mazuka mazuka.

<sup>28</sup>Kwa kwamba wadziza kumuhambuya Muungu, nae Muungu kawayatsa wakidz̄itaria haya maṭaro yao mazuka mazuka, ili kwamba wakidzihendea ḃasi haya mambo wasiyomala kuyahenda.

<sup>29</sup>Myojo yao idzaa kula aina ya mazuka, kind̄eḃi, hamile na ugid̄ifa. Wadzaa muriṭi wa uyaji na kufwia wantu d̄ea. Kazi yao ni nkondo na winji wa makulekule na myojo mizuka mizuka kwa wantu. Wao wabarata nyano ṭu

<sup>30</sup>na kunenea wantu mazuka. Ni wantu wamukeveyeo Muungu na weo waṭiriri, weonadziona na kudzishada. Ao meshi wakulachani njia mpya mpya za kuhendea mazuka, na ni wantu wasiowasikia wavyazi wao.

<sup>31</sup>Ntawa akili, na ni wantu wasiohikizika, wasiotsaka wantu wa madzumbani mwao na wasiowafwiya ṭei wangine.

<sup>32</sup>Hawa hawa wantu wamanya tswee kwamba, wantu weonahenda mambo mazuka mazuka dzayo, Muungu anawahukumu kufwa. Ela wao ntaviwamuḃe! Wanagija kuhenda mazuka nangere na kuwangiza moja na wangine wagije kuhenda mazuka.

## Warumi 2

<sup>1</sup>Dubva wewe mwenzangu, ikiwa kwamba unawanena wangine kwamba wanahenda mazuka, ḃasi umanye kwamba haṭa nawe nkuwezi kudzihehea haṭa kachuchu. Koro ukwakuwahukumuni wangine, kwakudziyeheani hukumu wewe mwenye, kwa dzambo haṭa nawe kwakuyahendani yayade mambo wiyokuwanenani nayo wenziwo kwamba wakuyahendani.

<sup>2</sup>Humanya ya kwamba Muungu anawahukumu na hachi hawade weonahenda mambo dzayo.



- <sup>3</sup>Wewe ukwakuwanenani kwamba hawaḍe weonahenda mambo dzayo wanamala kuhukumigwa, na hali nawe pia kwakuyahendani, unataḗara kwamba e hukumu ya Muungu inakusaza?
- <sup>4</sup>Ambu kwakumubalifani Muungu kwa dzambo ḍya kwamba jeje ni munanso muno kwako? Yani kwakuonani kwamba jeje si muharaka jwa kukuadhiḗu na kakukuiḗisiani! Munamba nkwaona haḗa kwamba hu huu wemawe wonse eokukuhendeani, kakukupfani namfasi nangere ili upate kupfyehuzama?
- <sup>5</sup>Ela kwa dzambo ḍya kitswacho chumu na kutsaatsaka kupfyehuzama mama kwako, kwakudzifundikiani adhaḗu nkuu idzeyokudza hiyo hiyo nsiku ya Muungu adzeyowarejea wanabvise, na kuwahukumu na hachi.
- <sup>6</sup>Hiyo hiyo nsiku, Muungu kadzamuipfa kula mumodza kuḗana na mahendoye.
- <sup>7</sup>Hawaḍe weonagija kuhenda mema na kulacha kwamba Muungu awakuzye na kuwahendeza wapfegwe hila na kuwa na maisha yasiyosia; wantu dzao, Muungu anawapfa maisha ya kuunga na yuungo.
- <sup>8</sup>Ela hawaḍe weo na umimi, weonayatsa haya mambo ya hachi wakauḗa mazuka, ngoro ya Muungu idzawasukia.
- <sup>9</sup>Kudzawa na ḍina na tsungu mukuu muno kwa kula mwanaaḍamu eyenahenda mazuka. Na haya haya mambo yadzawapata hangu Wayahuḍi mumpaka wantu wa vyeeti vingine.
- <sup>10</sup>Kenge kwa hawaḍe wonse weonahenda mema, Muungu kadzawakuzya na kuwapfa hila nkuu na naghea. Na haya haya mambo kadzayawahendea hangu Wayahuḍi mumpaka wantu wa vyeeti vingine.
- <sup>11</sup>Koro Muungu nka upendeleo kwa yuḍejwone.
- <sup>12</sup>Wayahuḍi weonahenda nabvise na hali huku waimanya hi Sharia ya Musa, wadzahukumigwa kuḗana na hi Sharia. Wantu wa vyeeti vingine ntawa Sharia ya Musa. Ela hawaḍe weonahenda nabvise na hali wamanya kwamba wakuhendani nabvise, nao pia wadzanangwa, haḗa ingawa ntawaidzi hi Sharia ya Musa.
- <sup>13</sup>Koro Muungu nkamuhwae muntu kuwa muhachi kwa dzambo ḍya kuisikiiya hi Sharia haḗa, ela anamuhwaa muntu kuwa muhachi ikiwa kwamba kahenda hivi vya hi Sharia ivyonamumala kuhenda.
- <sup>14</sup>Gula wantu wa vyeeti vingine hi Sharia ya Musa ntawanayo. Ela kula pfa akili zao zipfonawahuma kuhenda hivi vye Sharia ivyonatsaka, ḗasi wao wenye wanawa dza kwamba hi Sharia yoregwa myojoni mwao.
- <sup>15</sup>Hii inayanga kwamba hivi vye Sharia ivyonatsaka, wavimanya myojoni mwao. Haḗa hizi mama zao zinayanga tswee kwamba hiḍi hiḍi dzambo ni ḍugha. Koro akili zao zinawapfa kumanya kwamba dzambo siku ni dzema ambu ni zuka.

**16**Ndookomu hivi hivi ndivyo vidzevyowahendekela hiyo hiyo nsiku ya Muungu adzeyowahukumu wanaadamu kwa dzambo dya haya mambo weyonafitsa myojoni mwao. Kuubana na hi Injili niyonasumwiiya, Muungu kadzawahukumu wanaadamu wonse kuchiiya na kwa Kiristo Yesu.

**17**Wewe unadziona kwamba u Muyahuḍi na ukadzihwaiya kwamba aṭi nku untu kwa dzambo kuimanya hi Sharia ya Musa. Unadziona kwamba u jwa Muungu

**18**na ukadzihwaiya kwamba kuimanya miro ya Muungu. Unadziona kwamba hi Sharia ikuyongweeza namuna ya kuhambuya mambo yeyo mema ya mwisu.

**19**Unadziona ya kwamba unaweza kuwagija yuroi ntumbu matso, na unadzihwaa dza muyanga wa kuwayangaiya hawaḍe weo kizani.

**20**Unadziona dza kwamba u mwaalimu mkuu jwa kuyongweeza maḍuḍalesa na wantu wasiodzangora. Una hakika ya kwamba hi Sharia ikuyongweeza hi hachi pfamodza na umanyi wonse.

**21**Dubva, wewe wiyenawayongweeza wangine, nkwadziyongweeza wewe mwenye nguzi? Unawambadze wantu watseekwiwa, na hali katsi wewe mwenye kwakukwiwani?

**22**Unawamba wantu, “Namutsevunza ukwe,” na hali wewe mwenye kwakuvunzani ukwe. Unakwamba kukeva mambo ya miungu na hali wewe mwenye unakaa na kukwiwa vija vivyonawekwa mahekaluni mwa miungu ya nsuwe.

**23**Aṭi unakaa na kudziona kwamba kuimanya hi Sharia ya Muungu. Munamba nkukwakuonani haṭa kwamba avi wivyokuvunzani Sharia kwakuḍihendezani hiḍi sari dya Muungu ḍinjie kubalifigwani?

**24**Koro vyoregwa matsoroni kwamba, “Wantu wa vyeeti vingine wakuḍikufuruni sari dya Muungu kwa dzambo dyenu nywinywi Wayahuḍi!”

**25**Huko kuhinywa kwako kunawa na maana ikiwa kwamba kuiṭii hi Sharia. Ela ikiwa kwamba kwakuivunzani, ḅasi nku ugaragara uḍewonse na muntu asiyengizwa ntinyeni!

**26**Muntu jwa kyeeti kingine asiyedzahinywa, akiṭii hi Sharia, Muungu nkamuhwaa dza muntu ahinyijwe?

**27**Ndookomu nywinywi Wayahuḍi mudzahukumigwa ni wantu wa vyeeti vingine weokuiubani hi Sharia ingawa ntawadzahinywa. Wadamuhukumu kwa dzambo dya kwamba, ingawa mwakuhinywani na hi Sharia muyorejwa, ela munakaa na kuivunza.

**28**Hivi ni kunena kwamba, si kula avyaijwe Muyahuḍi kwamba ni Muyahuḍi jwa ḍugha haṭa. Na wala kuhinywa ḅasi kimwii ntakumuhendeze muntu kuwa Muyahuḍi jwa ḍugha.

<sup>29</sup>Ela Muyahuḍi jwa ḍugha ni huyuḍe eyenamuti Muungu na moja. Yani ni huyuḍe ahinyijwe mojoni mwakwe. Hidi hidi ni dzambo ḍya kiruhu na wala si dzambo ḍya kuuḅa matsoro ya Sharia yorejweyo pfantu. Muntu dzae nkapate shaḍu kuyawa kwa wanaaḍamu, ela anapata shaḍu kuyawa kwa Muungu.

### Warumi 3

<sup>1</sup>Mani ḍubva kuwa Muyahuḍi kuna faida ga? Ambu muntu akihinywa kuna wema ga?

<sup>2</sup>Kuwa Muyahuḍi kuna maana kwa kula njia. Cha ḍura ni kwamba Wayahuḍi ndiwo wantu wa Muungu awakaḅidhiyeo haya maaguye.

<sup>3</sup>Gula ni ḍugha kwamba wangine wao ntaweewa wahikizika kwa Muungu le. Ela hivyo hivyo ni kunena kwamba nae Muungu anavunza ahaḍi zakwe?

<sup>4</sup>Moro, sivyo kaḅisa! Muungu anagija kuwa muhachi kwa kula dzambo aneneyeyo, haḅa ikiwa kwamba wanaaḍamu wakaiya kunena nsuwe. Koro haya matsoro yamba, “Wipfonanyambia uzuka wangu, vyyuwo vyako mvyo hachi; na ukinipfiika ḍubini, wewe unashinda.”

<sup>5</sup>Ikiwa kwamba mazuka yehu yanayanga namuna ya Muungu aivyo muhachi ephonahukumu, ḍubva aswi hwambedze? Hwambe kakuhuoneani? Nyakunenani hivi koro ndivyo vya wantu wangine wevyonaḅara.

<sup>6</sup>Ela sivyo kaḅisa! Ṭambere Muungu nkahukumu na hachi mani andeweza kujuhukumu aju lumwengu?

<sup>7</sup>Ela ṭambere Muungu anagija kuonekana muhachi na kugija kupata shaḍu kuchiiya na hivi niivyo munsuwe, mani kuḅi amaale nahwajwa kuwa munabvise?

<sup>8</sup>Wantu wangine wakuhupfangizani kwamba hwakuwayongweezani wantu wagije kuhenda mazuka ili waweze kupata mema. Hao hao wantu Muungu anawahukumu dza wevyonamala kuhukumigwa.

<sup>9</sup>ḍubva hwambedze? Hwambe swiswi Wayahuḍi huna maana kuchia wantu wa vyeeti vingine? Moro sivyo kaḅisa! Koro nimaanena hangu hapfo kaḍura kwamba, Wayahuḍi na wantu wa vyeeti vingine, wonse wakuḅawaligwani ni nabvise.

<sup>10</sup>Ni dza hivi vya haya matsoro yaneneyevyo yakyamba, “Ntaku haḅa mumodza eye muhachi usoni kwa Muungu.

<sup>11</sup>Ntaku haḅa mumodza eyenaimuka, wala eyenamulacha Muungu.

<sup>12</sup>Wanaaḍamu wonse wamuyatsa Muungu. Wonse watsowa tswee, na ntaku haḅa mumodza eyenahenda mema.

<sup>13</sup>Vyuuwo vyao wevyonanena, ni vizuka vizuka dza tsatsu wa mbeera ziizo wazi. Nyiimi zao zibarata kunena nsuwe, na manwa yao yananena vyuuwo vizuka vizuka, viivyo dza singo wa nyoka.

<sup>14</sup>Manwa yao yanakakanyika maduwo mazuka mazuka.

<sup>15</sup>Na ni waharaka wa kukukamisa wantu na kuwayaga.

<sup>16</sup>Kula wepfonakwenda, kazi yao ni kunanga-nanga maisha ya wantu na kuwayatsia dina.

<sup>17</sup>Ao meshi ntawadzi kukaa na naghea na wantu,

<sup>18</sup>na wala ntawamushooge Muungu!”

<sup>19</sup>Sasa humanya kwamba hi Sharia inawahusu Wayahuḍi, koro ndiwo waipfegejweo. Na waipfegwa ili lumwengu jwonse jutseewa na kiḍechonse cha kudzihehea nacho usoni kwa Muungu.

<sup>20</sup>Koro ntaku yuḍejwonse eyenahwajwa kuwa muhachi usoni kwa Muungu kwa dzambo ḍya kuiuḅa hi Sharia, kwa kwamba kazi ya hi Sharia ni kuwayanga wantu kwamba ni wanabvise.

<sup>21</sup>Ela sasa Muungu kaihuyanga hi njia ya kuhuhendeza kuwa wahachi usoni kwakwe. Si kwa kuuḅa Sharia, ela ni kwa kuuḅa hi njia ihadzijweyo humu matsoroni.

<sup>22</sup>Muungu anawahwaa wantu kuwa wahachi kuuḅana na faro weyonayo kwa Yesu Kiristo. Na anahenda hivi kwa wonse wahikiziyeo, kwa kwamba ntaku ugaragara kahi ya Wayahuḍi na wantu wa vyeeti vingine.

<sup>23</sup>Koro wanaadamu wonse wahenda nabvise na wapfungukijwa ni udheru wa Muungu.

<sup>24</sup>Ela kwa dzambo ḍya teiye, Muungu kawapfa wanaadamu wonse tubvo ḍya kuwahendeza wawe wahachi usoni kwakwe. Kahenda hivi kwa kumuhuma Yesu Kiristo adziye akiwayavya nabviseni na akiwaweka huru.

<sup>25</sup>Muungu kamuyavya Yesu awe dza mvuugiya ili kwamba kuchiiya na kwa hu mwaziwe ehiyeo, hawaḍe wamuhikiziyeo wapate kuyatsijwa nabvise zao. Kavihenda nangere ili apate kuwayanga wanaadamu kwamba jeje ni muhachi. Koro kae Muungu kawaitisia wanaadamu haḷa nkakuwahukumu kwa nabvise zao wahendeyezo.

<sup>26</sup>Na kwehii ngera ya yeo, Muungu kayanga wazi tswēe kwamba jeje ni muhachi. Na hawaḍe wanabvise wamuhikiziyeo Yesu, jeje anawahwaa kuwa wahachi usoni kwakwe.

<sup>27</sup>Dubva ati hunaweza kudzivunia kwamba huhenda kiḍechonse kimuhendezeyecho Muungu ahuhwae kuwa wahachi usoni kwakwe? Ntaku kiḍechonse! Na ni kwa dzambo ga ntaku kintu? Ni kwa kwamba ntahuwezi kuwa

wahachi usoni kwakwe kwa kuuḅa Sharia. Ela hunahwajwa kuwa wahachi kwa dzambo ḍye faro yehu hwiyonayo kwa Yesu Kiristo.

<sup>28</sup>Ndookomu hunakwamba Muungu anamuhwaa muntu kuwa muhachi kuuḅana ne faro eyonayo, na wala si kwa kuuḅa Sharia.

<sup>29</sup>Ambu munaḥara kwamba Muungu ni Muungu jwa Wayahuḍi ḅasi? Dzaambia siye Muungu jwa wantu wa vyeeti vingine pia? Ndivyo, Muungu ni Muungu jwa wantu wa vyeeti vingine pia.

<sup>30</sup>Koro kuna Muungu mumodza tu. Na kuna njia modza tu iyonawahendeza wantu kuwa wahachi usoni kwakwe. Hangu Wayahuḍi wahinyijweo na haḥa wantu wa vyeeti vingine wasiohinywa, wonse anawahwaa kuwa wahachi usoni kwakwe kuuḅana ne faro weyonayo.

<sup>31</sup>Dubva avi hwivyokungiziani mukazo dzuu ya kuwa na faro, ni kunena kwamba hwakuihendezani e Sharia kutsaawa na maana? Moro, sivyo haḥa. Hivi hwivyokunenani hwakuizingiziani mukazo hi Sharia.

#### Warumi 4

<sup>1</sup>Dubva hwambedze dzuu ya bibi jwehu Ibrahimi? Muungu kamuhwaadze kuwa muhachi usoni kwakwe?

<sup>2</sup>Tambere Muungu andeewa kamuhwaa Ibrahimi kuwa muhachi kwa dzambo ḍya mahendoye mema, ḅasi Ibrahimi andeewa na kintu cha kudzivunia. Ela nka saḅaḅu ya kudzivunia usoni kwa Muungu.

<sup>3</sup>Koro haya matsoro yamba, “Ibrahimi kamuserefaḥa Muungu, nae Muungu kamuhwaa kuwa muntu muhachi.”

<sup>4</sup>Muntu eyenahenda kazi anapfegwa maipfo. Na haya maipfoye nkayapfegwe dza kwamba ni nḥunu, ela anayapfegwa kwa kwamba ni hachiye.

<sup>5</sup>Ela kwa Muungu muntu anahwajwa kuwa muhachi kwa dzambo ḍya kumuserefaḥa jeje eyenawayatsia haḥa wanabvise, na wala nkahwajwe kuwa muhachi kwa dzambo ḍya mahendoye.

<sup>6</sup>Haḥa haju Daḍi kanena dzuu yedihiḍi dzambo, ephonena dzuu ya tsekea ya muntu yudejwonse jwa Muungu eyenamuhwaa kuwa muhachi pfasipfo kuyowa mahendoye.

<sup>7</sup>Kamba, “Wana tsekea iyodze hawaḍe wa Muungu awayatsiiyeo mazuka yao na kuziwafutia nabvise zao!

<sup>8</sup>Wana tsekea iyodze hawaḍe wa Bwana asiowaḥalia nabvise zao kawii meshi!”

<sup>9</sup>Dubva ai tsekea ya haju Daḍi aneneeyo, nza Wayahuḍi ḅasi ambu haḥa wantu wa vyeeti vingine? Dzaambia si ya wantu wonse? Hunakaa na kwamba Muungu kamuhwaa Ibrahimi kuwa muntu muhachi kwa dzambo ḍya faro eyokuwa nayo.

<sup>10</sup>Epfootaligwa kuwa muhachi, ewa kamaahinywa ambu baḍo? Humanya ya kwamba Muungu kamuhwaa kuwa muntu muhachi ḍura, makisa kadzakahinywa nyuma.

<sup>11</sup>Ibrahimu kahinywa baḍa ya kwamba Muungu kamuhwaa kuwa muntu muhachi. Kuhinywa kwakwe kwiwa ni alama ya kuyanga kwamba Muungu kamuhwaa kuwa muntu muhachi kwa dzambo ḍya namuna amuserefaṭiyevyo Muungu, ingawa ewa nkadzahinywa. Ndookomu Ibrahimu ndiye baba jwa kiruhu jwa hawaḍe wonse wamuhikiziyeo Muungu na wakiṭaligwa kuwa wahachi, ingawa ntawadzahinywa.

<sup>12</sup>Na pia ni baba jwa kiruhu jwa hawaḍe wonse wahinyijweo na wakimuhikiza Muungu. Si baba jwao kwa dzambo ḍya kuhinywa, ela ni baba jwao kwa dzambo ḍya kwamba wamuhikiza Muungu dza viviḍe vya baba jwehu Ibrahimu amuhikiziyevo haṭa kaḅila nkadzahinywa.

<sup>13</sup>Muungu ewa kamuahiḍia Ibrahimu na yuvyeejwe kwamba kadzajumumpa huju lumwengu jwonse juwe jwakwe. Ibrahimu nkakuiwekejwa hi hii ahaḍi kwa dzambo ḍya kuziuba Sharia haṭa, ela kaiwekejwa kwa dzambo ewa kamuhikiza Muungu, na Muungu kamuhwaa kuwa muntu muhachi.

<sup>14</sup>Koro ṭambere hawaḍe wa kupata hivi vya Muungu evyonaahiḍi ni hawaḍe weonauba Sharia, baṣi ni kunena kwamba kumuhikiza Muungu ntaku maana, na haṭa hi ahaḍi ya Muungu ntaṭi faiḍa iḍeyonse.

<sup>15</sup>Hi Sharia inawahendeza hawaḍe weonaivunza wakaadhibigwa. Ela ikiwa kwamba ntaku sharia, baṣi ntakuwe na muntu jwa kuadhibigwa kwa tsowa ḍya kuvunza sharia.

<sup>16</sup>Ndiyo maana kumuhikiza Muungu ndiḍyo dzambo muhimu. Muungu kaihuwekea hi ahaḍiye bure, ndookomu ni ahaḍi iyo na uhakika. Hi hii ahaḍi si ya hawaḍe weo na Sharia ṭu, ela nza haṭa hawaḍe wasio na Sharia wamuhikiziyeo Muungu dza Ibrahimu. Koro Ibrahimu ndiye huyu baba jwa wonse weonamuhikiza Muungu.

<sup>17</sup>Dza vya matsoro yaneneyevyo yakyamba, Muungu kamwamba Ibrahimu, “Nikuhendeza kuwa baba jwa vyeeti vinji.” Epfoakiyambijwa haya haya, Ibrahimu ewa usoni kwa Muungu na kayahikiza. Huyu ndiye huyu Muungu eyenawafufuya wafu, na haṭa mambo yasiyodzahendeka akayahwaa dza kwamba yesakuhendeka.

<sup>18</sup>Hi hiḍe ngera, Ibrahimu ewa na chima cha myaka gana. Ela nkakufwa moja, kagija kumuserefaṭa Muungu ṭu haṭa ingawa edzimanya kwamba kamaawa jarisa ghogho, na mukaziwe ewa ni ndaṭa. Muungu epfomuahiḍi Ibrahimu kwamba anawa baba jwa vyeeti vinji, na kwamba yuvyeejwe junawa yukuu dza hizi nyoha, Ibrahimu kamuserefaṭa Muungu, ingawa dzambo dzadyo ḍinaonekana kwamba ntaḍiwezi kuhendeka. Na Ibrahimu kadzakawa baba jwa vyeeti vinji ḍugha.

<sup>20</sup>Ibrahimu nkakungiza kajela ideyonse kwa hi ahađi ya Muungu amuwekeeyo. Ishinu serefano yakwe igija kuwa na nguvu na kamuyaviza shađu Muungu,

<sup>21</sup>akiwa na uhakika kwamba Muungu ana uwezo wa kuhenda hivi aahidiyevyo.

<sup>22</sup>Na ndiyo maana Muungu kamuhwaa Ibrahimu kuwa muntu muhachi kwa dzambo ɗye faroye eyokuwa nayo.

<sup>23</sup>Hivi vyorejwevyo kwamba, “Muungu kamuhwaa Ibrahimu kuwa muntu muhachi,” ntavikworegwa kwa dzambo ɗya Ibrahimu jeje heketu hađa,

<sup>24</sup>ela vyoregwa kwa dzambo ɗyehu pia. Vinahupfa uhakika wa kwamba hukimuhikiza Muungu, huyu amufufwiiye Bwana jwehu Yesu Kiristo kuyawa kwa wafu, ɓasi hađa naswi pia Muungu anahuhwaa kuwa wahachi.

<sup>25</sup>Bwana Yesu kayavigwa apate kufwa kwa dzambo ɗya nabvise zehu, na kafufujwa kuyawa kwa wafu ili naswi huweze kuwa wantu wahachi usoni kwa Muungu.

## Warumi 5

<sup>1</sup>Na kwa kwamba Muungu anahuhwaa kuwa wahachi usoni kwakwe kwa dzambo ɗya faro zehu, ɓasi huna naghea na Muungu kuchiiya na kwa Bwana jwehu Yesu Kiristo.

<sup>2</sup>Kiristo kahupfa njia ya kuifikia hi hii ɗei ya Muungu huipatiyeyo hi hii saasambi kwa dzambo ɗya faro zehu. Ndookomu naswi hunatsekea kwa haya madzikwatyo hwiyonayo, ya kwamba Muungu kadzahungiza maremboni mwakwe.

<sup>3</sup>Na zaidi ya hayo, hađa hukiwa mađinani pia hunatsekea, koro humanya kwamba mađina yanahuyongweeza kuitisa.

<sup>4</sup>Kuitisa kunahupfa nguvu za kugija kuwa na myenendo myema, na myenendo myema inahwongezea madzikwatyo yehu ya kupata mupfonyo.

<sup>5</sup>Na haya haya madzikwatyo hwiyonayo ntayanahungiza yutswani, koro Muungu kahuyanga matsakoye makuu kuchiiya na kwa Ruhu Mudheru jwakwe. Muungu kamuhukakanyia huyu huyu Ruhu myojoni mwehu dza ɗola yakwe ahupfiyeyo.

<sup>6</sup>Koro hwipfokuwa amaale ntahudziwezi hađa kachuchu, Kiristo kadza na wakati mwema ɗa, na kafwa kwa dzambo ɗyehu hwonse hwiwo wanabvise.

<sup>7</sup>Si rahisi kuona muntu adzibigie koɓela kuyagwa kwa dzambo ɗya muntu muhachi yudejwone. Pfangine muntu anaweza kudziɗolea kuyagwa kwa dzambo ɗya muntu mwema.

<sup>8</sup>Ela ɗayowani namuna ya Muungu ahuyangiyevyo kwamba kahutsaka. Koro ingawa hwikiishi nabviseni, Kiristo kadza kafwa kwa dzambo ɗyehu!

<sup>9</sup>Kwa kwamba Kiristo kamahuhendeza kuwa wahachi usoni kwa Muungu kuchiiya na kwa kifoche, basi pia huna uhakika kwamba anahupfonya kuyawana ne hukumu ya Muungu idzeyokudza.

<sup>10</sup>Hivi hivi huna uhakika navyo kwa dzambo dya kwamba hwipfokuwa nyabva na Muungu, hupatanishwa nae kawii kuchiiya na kwa hichi kifo cha huyu Mwanawe. Na sasa hukimapanishwa na Muungu, basi huna uhakika kwamba hunapfonywa, koro huyu Mwanawe ka moja.

<sup>11</sup>Na si hivyo tu, ela sasa huna tsekea nkuu muno kwa Muungu kwa dzambo dya kwamba kuchiiya na kwa Bwana jwehu Yesu Kiristo swiswi hupatanishwa na Muungu.

<sup>12</sup>Kae nabvise injia lumwenguni kwa dzambo dya muntu mumodza. Na hiyo hiyo nabvise ahendeeyo iyeha kufwa. Ndookomu kufwa kunamufikia kula mwanaadamu kwa kwamba wonse wahenda nabvise.

<sup>13</sup>Gula wanaadamu wekihenda nabvise hangu kae na kae kabila Muungu nkadzawayeha hi Sharia. Ela nabvise zao ntazitaligwe koro ntakwiwa sharia ideyonse.

<sup>14</sup>Ingawa hangu ngera ya Adamu haṭa ngera ya Musa apfegejweyo hi Sharia wantu wekifwa, ntawekifwa kwa dzambo dya kuvunza amuri ya Muungu dza hivide vya Adamu ahendeeyo. Adamu ewa ni dza kivwii cha huyude adzeekudza, yani Kiristo.

<sup>15</sup>Ela kuna ugaragara kahi ya hi nabvise ya Adamu ayeheeyo, na hi tola ya kuyatsijwa nabvise iyehejweyo ni Yesu Kiristo. Koro kuchiiya na kwa nabvise ihendejweyo ni muntu mumodza, yani Adamu, wantu wenji wanjia kufwani. Ela huyu yungine, yani Yesu Kiristo, kahendeza wenji wapate kuyatsijwa nabvise zao kuchiiya na kwa ṭei ya Muungu aikakanyiyeyo kwa wenji.

<sup>16</sup>Hi namuna ya Muungu evyonayavya tola yakwe kwa wanaadamu, ni garagara na hivi vya nabvise injiiyevyo kuchiiya na kwa muntu mumodza. Nabvise modza ihendejweyo, iyeha hukumu kwa wantu, koro iwahendeza watsovi. Ela baada ya wantu kuhenda nabvise nyinji na nyinji, Muungu kaiwayeha hi tolaye ili aweze kuwahendeza wahachi usoni kwakwe.

<sup>17</sup>Nabvise ya muntu mumodza iyeha kufwa kwa lumwengu yuzima. Ela kuchiiya na kwa muntu mumodza yungine, yani Yesu Kiristo, hawaḍe waipfokeeyeo hi ṭei nkuu ya Muungu ne tolaye ya kuwahendeza wahachi, hao wadzaishi maisha ya kuunga na yuungo.

<sup>18</sup>Basi na dza vya nabvise ya muntu mumodza iyeheeyo hukumu kwa wantu wonse, ndivyo vya hendo modza dya hachi dihendejweyo ni Yesu Kiristo divyokuwahendezani wantu wonse kuwa wahachi usoni kwa Muungu na kuwapfa maisha.



<sup>19</sup>Koro dza vya wantu wonse wagaliyevyo wanabvise usoni kwa Muungu kwa dzambo dya muntu mumodza kutsamuṭii Muungu, basi ndivyo vya Muungu adzevyowahendeza wantu wonse kuwa wahachi usoni kwakwe, kwa dzambo dya uṭiifu wa muntu mumodza.

<sup>20</sup>Hi Sharia ipfoyehegwa, injipfisa mazuka, ela kula pfa wantu wagijiyepfo kuhenda nabvise, Muungu kagija kuwafwiya ṭei zaiḍi na zaiḍi.

<sup>21</sup>Cha mwisu ni kwamba kae nabvise iwa ijuṭawala lumwengu kwa kuwangiza wantu kufwani. Ela sasa hi ṭei ya Muungu ndiyo iyokuhuṭawalani kwa kuhuhendeza kuwa wahachi usoni kwa Muungu na kuhupfa maisha ya kuunga na yuungo. Na hivi hunavipata kuchiiya na kwa kumuhikiza Bwana jwehu Yesu Kiristo.

## Warumi 6

<sup>1</sup>Dubva hwambedze? Hwambe kwamba hugije kuhenda nabvise amaale ili kwamba Muungu agije kuhufwiya ṭei na kuhuyatsia zaiḍi na zaiḍi?

<sup>2</sup>Sivyo haṭa! Nabvise hwisakuifwiya hangu iide ṭi! Sasa hunawezadze kugija kuishi nabviseni amaale?

<sup>3</sup>Munamba ntamudzi haṭa kwamba hwonse hwipfoṭopyegwa huunganywa na Kiristo Yesu, na ni dza kwamba hufwa pfamodza nae?

<sup>4</sup>Hwipfoṭopyegwa, ni dza kwamba hufwa na huzikwa pfamodza na Kiristo. Hivi vihendeka ili kwamba naswi huweze kuishi maisha mapfya, dza vya Muungu Baba jwehu amufufwiiyevyo Kiristo kuyawa kwa wafu kwa uwezowe mukuu.

<sup>5</sup>Koro kwa kwamba huunganywa na Kiristo kwa kufwa pfamodza nae, basi pia hudzafufujwa dza viviḍe afufwiiywevyo.

<sup>6</sup>Na humanya kwamba hu ubenaadamu wehu wa dura upfatsikwa hapfaḍe muhini mwa mpatsa pfamodza na Kiristo, ili kwamba nabvise itseewa na nguvu kawii maishani mwehu. Ntahukwaa wahumwa wa nabvise kawii.

<sup>7</sup>Koro yuḍejwone akisa kufwa anawa ka huru kuyawana na uhumwa wa nabvise.

<sup>8</sup>Na kwa kwamba hufwa pfamodza na Kiristo, huhikiza kwamba hudzaishi pfamodza nae kawii.

<sup>9</sup>Koro humanya kwamba Kiristo kafufujwa kuyawa kwa wafu na nkafwe kawii meshi. Kufwa ntaku nguvu kawii dzuu yakwe.

<sup>10</sup>Huku kufwa afwiyeko, kazifwiya nabvise mweedha mumodza ṭu, ela hivi evyokuishini kakuishini kwa dzambo dya uhusiano wakwe na Muungu.

<sup>11</sup>Dubva nanywi pia dzihwaeni dza wantu muifwiiyeo nabvise na mwiwokuishini kwa dzambo dya Muungu kuchiiya na kwa Kiristo Yesu.

- 12**Ndookomu namutseyatsa nabvise iitawale kawii hi mii yenu ya kufwa. Namutseyatsa imuhendeze mukidziitoseza hadya zenu nzuka nzuka za kimwii.
- 13**Namutseyiyatsa sehemu zidezonse za mii yenu ziihumikie nabvise kwa kuhenda mazuka. Ishinu dzyavyeni kwa Muungu koro muyawa kufwani na sasa mumapfegwa maisha mapfya. Kula kiiriiri cha mii yenu nakihumike kwa kazi nyema ya Muungu.
- 14**Koro nabvise ntai nguvu kawii dzuu yenu kwa kwamba ntamukwaa nsii ya Sharia, ela mwaa nsii ya t̄ei ya Muungu.
- 15**Ikimaawa kwamba hi t̄ei ya Muungu ihuweka huru hutseewa wahumwa wa Sharia, d̄ubva ni kunena kwamba hunaweza kugija kudzihendea nabvise basi? Moro sivyo haṭa!
- 16**Dzaambia ntamukumanya kwamba mukidziyavya kumuṭii muntu, basi mu wahumwa wa huyo huyo muntu? Munaweza kutsana kuitii nabvise na mwisowe munjie kufwani, ambu munaweza kutsana kumuṭii Muungu na muwe wantu wa kuhenda yeyo ya hachi usoni kwakwe.
- 17**Haṭa vivyo namuyaviza d̄uḍa Muungu, koro kae mwiiwa wahumwa wa nabvise, makisa mudzamuyatii na moja mumodza haya mayongweezo ya hachi muyongweezejweyo.
- 18**Mwisakuwekwa huru kuyawana na uhumwa wa nabvise, na sasa mumaawa wahumwa wa Muungu wa kuhenda yeyo ya hachi.
- 19**Nyakumumpani mufaano wa wahumwa na maḥwana zao nangere, kwa dzambo d̄ya udhaifu wenu wa kibenaadamu. Kae mwiiwa mudziyavya kuwa wahumwa wa mambo machafu na mwikihenda kula aina ya mazuka. Ela sasa dzyavyeni kuwa wahumwa wa kuhenda mambo yeyo ya hachi, ili mugije kuwa wantu wa Muungu d̄ugha.
- 20**Mwipfokuwa wahumwa wa nabvise, ntamwikimuudama kuhenda mambo yeyo ya hachi.
- 21**Mwikihenda mambo mazuka mazuka ya kwamba haṭa yakihadzwa saambi munaona yutswa. Ela kisa mupata kintu ga? Ntamukupata kiḍechonse! Koro haya haya mambo mwisowe yanangiza wantu kufwani.
- 22**Ela sasa kwa kwamba mwisakuwekwa huru kuyawana na nabvise na mwisakuwa wahumwa wa Muungu, hi faida mwiyo kupatani ni kwamba mwakuhendzewani kuwa wadheru, na mwisowe mudzapata maisha ya kuunga na yuungo.
- 23**Koro t̄ubvo d̄ya kuhenda nabvise ni kufwa. Ela hi t̄ola ya Muungu ayaviyeyo ni maisha ya kuunga na yuungo kuchiiya na kwa Kiristo Yesu Bwana jwehu.

## Warumi 7

- <sup>1</sup>Nywinywi wandugu zangu Wayahuḍi muimanyiyeo hi Sharia, munamba ntamudzi kwamba Sharia inamuṭawala muntu ṭu akiwa kwamba ka moja?
- <sup>2</sup>Kwa mufaano muke ahwaijwe, hi sharia ya kwamba ni mukaza muntu inamugija-gija ṭu ikiwa kwamba muumewe ka moja. Ela muumewe akifwa, ḅasi hi sharia ya kwamba ni mukaza muntu ntaimugije-gije kawii.
- <sup>3</sup>Ndookomu ikiwa kwamba muke kahwajwa ni muyume yungine na hali muumewe ka moja, huyo anawa kakunjiani rangani. Ela muumewe akifwa anawa nkakufungwa ni sharia kawii, na akihwajwa ni muyume yungine nkawe kunjiani rangani.
- <sup>4</sup>Dubva nanywi pia wandugu zangu, mwisakuwa huru kuyawana na hi Sharia kuchiiya na kwa hivi vya Kiristo afwiyevyo hapfaḍe muhini mwa mpatsa. Muwekwa huru ili muweze kuwa wa muntu yungine. Yani muweze kuwa wa huyu afufwiijwe kuyawa kwa wafu, ili kwamba hwonse huweze kudziyavya wazima wazima kwa Muungu.
- <sup>5</sup>Koro hwipfohukiṭawaligwa ni hu ubenaadamu wehu, hi Sharia ikiziyamusa hizi ṭamaa nzuka nzuka zizokuwa miini mwehu, na hwikidziyavya wazima wazima kwa mambo ya nabvise yeyonayeha kufwa.
- <sup>6</sup>Kenge sasa hwisakuwa huru kuyawana na hi Sharia. Iwa ihuweka dza wafungwa, ela sasa hwaa huru na ntahukwakumuhumikiani Muungu kwa njia ya kuuḅa Sharia ya kworegwa pfantu dza ḍura. Ela hwakumuhumikiani kwa njia mpya, yani kuchiiya kwa Ruhu jwa Muungu.
- <sup>7</sup>Dubva kwa avi nineneyevyo, wangine wenu wakuimukani dza kwamba nyakwambani ai Sharia ni nzuka? Moro sikwakunenani hivyo haṭa! Ae sokwaa ai Sharia, ami nindemanya haṭa ya kwamba nabvise ni kintu gani le? Ṭambere hi Sharia ntaindekwamba, “Nkudzomiye mahe cha mwenziwo,” haṭa sindeemanya ya kwamba katsi kumiiya mahe cha muntu ni nabvise.
- <sup>8</sup>Ela hi nabvise iyo kuzimuni mwangu iitumia hi hii amuri na injumuiya kula aina ya ṭamaa nzuka! Na hali ṭambere ntaku Sharia, nabvise ntaindeewa na nguvu.
- <sup>9</sup>Mimi mwenye nipfokuwa sidzaihambuya hi Sharia, nikidziona dza kwamba nyakuishini urembo. Ela nipfokudza ninkiimanya hi hii amuri, nabvise nayo ifufuka na iniyaga kiruhu.
- <sup>10</sup>Ndookomu niona kwamba hi amuri iyehejweyo kunimpa maisha ya tsekea, ishinu ndiyo iningizieyo kufwani kafu.
- <sup>11</sup>Koro nabvise iitumia hi amuri, iniḍyuurisa na iningiza kufwani.
- <sup>12</sup>Ndookomu nichokunenani ni kwamba hi Sharia iyawa kwa Muungu. Na hi amuri nayo pia iyawa kwa Muungu, na inahukumu na hachi na ni nyema.
- <sup>13</sup>Mani ḍubva kwa avi nineneyevyo mwakuniimukani dza kwamba nyakwambani achi chicho chema kiniyehea kufwa? Moro sikwakunenani hivyo haṭa! Ela

nyakunenani kwamba, nabvise ndiyo itumiiyeyo hichi hichi chicho chema, yani hi amuri, na yakuningizani kufwani. Tayowani namuna ya nabvise ivyo nzuka! Inatumia kintu chema kiyawiyecho kwa Muungu, na ikangiza wantu kufwani.

<sup>14</sup>Hwonse humanya kwamba hi Sharia nza mambo ya kiruhu, ela mimi ni mwanaadamu niyekutawaligwani ni mambo ya kimwii. Mimi nya dza muhumwa niguzijwee kuihumikia nabvise.

<sup>15</sup>Haya mambo niyonahenda, mimi mwenye sikae na kuyaimuka. Koro haya niyonatsaka kuyahenda siyahende, ishinu yayade nisyotsaka kuyahenda, ndiyo niyonayahenda.

<sup>16</sup>Na kwa kwamba nakaa na kuhenda haya nisyotsaka kuyahenda, basi vinayanga wazi kwamba nikubali kwamba hi Sharia ni nyema.

<sup>17</sup>Ndookomu kunena hida ya hachi, sikwakuvihendani kwa kutsaka kwangu, ela hi nabvise iyo kuzimuni mwangu ndiyo iyokunihendezani nihende hivi hivi.

<sup>18</sup>Nimanya kwamba ntaku dzema didedyonse didyo kuzimuni mwangu kwa dzambo dya hu ubenaadamu wangu. Koro ingawa kuzimuni mwangu nakaa na kudzisikia kuhenda mema, inanga siyahende.

<sup>19</sup>Haya mema niyonakaa na kutsaka kuyahenda siyahende, ishinu nahenda haya mazuka nisyotsaka kuyahenda.

<sup>20</sup>Dubva kwa kwamba nakaa na kuhenda haya nisyotsaka kuyahenda, basi ni kunena kwamba simi kawii niyenavihenda, ela ni hii nabvise iyo kuzimuni mwangu.

<sup>21</sup>Ndookomu naona kwamba vinikaiya dza sharia ya kwamba kula ninkitsaka kuhenda mema, haya mazuka ndiyo niyonatsana kuhenda.

<sup>22</sup>Humu mojonni mwangu nakaa nikitsekezwa ni hi Sharia ya Muungu.

<sup>23</sup>Ela nyakuonani kwamba kuna sharia ingine iyokuhendani kazi mwiini mwangu. Ni sharia iyokuipfingani hi sharia ya hi akili yangu ibaratiyeyo, na inakaa na kunihendeza mufungwa jwa hi sharia ya nabvise iyokuhendani kazi mwiini mwangu.

<sup>24</sup>E mimi nya dinani ti! Ni ga jwa kunipfonya na haya haya maisha ya kuningiza kufwani?

<sup>25</sup>Ela namuyaviza duda Muungu, koro ananipfonya kuchiiya na kwa Bwana jwehu Yesu Kiristo! Ndookomu munaona namuna viivyo. Humu mojonni mwangu natsaka kuitii hi Sharia ya Muungu, ela kwa dzambo dya hu ubenaadamu wangu, nigala muhumwa jwa hi sharia ya nabvise.

## Warumi 8

<sup>1</sup>Ndookomu sasa hawade weokuishini hariani mwa Kiristo Yesu ntawawezi kuhukumigwa.

- <sup>2</sup>Koro kuchiiya na kwa Yesu Kiristo, hizi nguvu za huyu Ruhu jwa Muungu eyenamumpa maisha ya kuunga na yuungo zisakumuweka huru kuyawana na hi sharia ya nabvise iyonayeha kufwa.
- <sup>3</sup>Hi Sharia ntaikuweza kuhuweka huru kwa dzambo dya udhaifu wehu wa kibenaadamu. Ela Muungu kahuweka huru kwa kumuhuma huyu Mwanawe jeje mwenye, adziye akivyajwa na mwii wiwo dza hi mii yehu ya nabvise. Kadza lumwenguni kahukumigwa ili azihunwiiye nabvise zehu.
- <sup>4</sup>Muungu kahenda hivi ili kwamba swiswi husiokuwa kuuḅani mambo ya kimwii, hwiwokuyongojwani ni huyu Ruhu jwakwe, huweze kuhenda yeyo ya hachi, dza hivi vye Sharia ivyonatsaka.
- <sup>5</sup>Hawaḁe weonaishi kwa kuuḅa mambo ya kimwii, wanaḁaria mambo ya kimwii. Ela hawaḁe weonaishi kwa kuuḅa mambo ya huyu Ruhu, wanaḁaria mambo yeyonamutsakiza huyu Ruhu.
- <sup>6</sup>Huyuḁe eyenaiyatsa hi akili yakwe ikaḁaria mambo ya kimwii, anadziyeheya kufwa. Ela huyuḁe eyenadziyatsia kuyongojwa ni huyu Ruhu jwa Muungu, Muungu anamumpa maisha mapfya na naghea.
- <sup>7</sup>Ndookomu muntu eyenaḁaria ḅasi mambo ya kimwii ni nyabva jwa Muungu. Muntu dzae nkawezi kuiḁi Sharia ya Muungu haḁa kachuchu.
- <sup>8</sup>Ndiyo maana wantu weonaḁawaligwa ni mambo ya kimwii ntawawezi kumutsakiza Muungu.
- <sup>9</sup>Ela nywinywi ntamukwakuḁawaligwani ni mambo ya kimwii. Ikiwa kwamba huyu Ruhu jwa Muungu ka kuzimuni mwenu, ḅasi ndiye eyekumuyongowani. Kumbukani kwamba muntu asiye Ruhu jwa Kiristo, huyo si jwa Kiristo.
- <sup>10</sup>Haḁa ingawa mii yenu idzafwa kwa dzambo dya nabvise, huyu Ruhu jwa Kiristo anagija kumumpa maisha mapfya, kwa kwamba Kiristo ka myojoni mwenu. Koro Kiristo ndiye amuhendezeye kuwa wahachi usoni kwa Muungu.
- <sup>11</sup>Na kwa kwamba huyu Ruhu jwa huyu Muungu amufufwiiye Kiristo Yesu kuyawa kwa wafu ka kuzimuni mwenu, ḅasi yuyude amufufwiiye Kiristo anamumpa maisha mapfya nywinywi mwiwo na mii ya kufwa. Nevihivi anavihenda kuchiiya na kwa huyu Ruhu jwakwe eye kuzimuni mwenu.
- <sup>12</sup>Dubva wandugu zanguni, ntahu ruhusa ya kuishi maisha ya kimwii kawii, ela ni haḁi huishi kwa kuuḅa hivi vya huyu Ruhu jwa Muungu evyonatsaka.
- <sup>13</sup>Koro mukiishi maisha ya kuḁawaligwa ni mambo ya kimwii, hachi munafwa. Ela ikiwa kwamba kwa nguvu za Ruhu Mudheru muyatsa kuhenda mambo mazuka kaḅisa, ḅasi munaishi.
- <sup>14</sup>Wonse weonayongojwa ni Ruhu jwa Muungu, ni wana wa Muungu.

**15**Kwa kwamba Muungu nkakumumpa Ruhu jwa kumuhendeza wahumwa woga kawii, ela kamumpa Ruhu jwa kumuhendeza wana wa Muungu. Na huyo huyo Ruhu ndiye eyenahuwezesha hukwakumuyombani Muungu hukamuhana Baba jwehu.

**16**Ndookomu huyu Ruhu jwa Muungu pfamodza na hizi ruhu zehu vyakuyavyani ushaahidi kwamba hu wana wa Muungu dughu.

**17**Kwa kwamba hu wanawe, basi hizi mvoni aziwawekeeyezo wantuwe hunazipata, na hunazipfokea pfamodza na Kiristo, kwa kwamba kula kintu cha Muungu amumpiyecho Kiristo, naswi pia nchehu. Ela hukitsaka kunjia maremboni pfamodza na Kiristo, ni hadi hukubali kukunta dina dza vivide vyakwe akuntiyevyo dina.

**18**Nina hakika kwamba hizi dina hwizokuzikuntani hi saasambi si kintu, hukiziinganya na haya marembu hudzeyopfegwa.

**19**Koro kula kiumbe cha Muungu aumbiyecho chakuindiiyani na hamu muno hiyo hiyo nsiku ya Muungu adzeyowayanganya hawa wanawe.

**20**Viumbe vyonse vya lumwenguni vina duo dya Muungu ingawa ntavikudzitsakia duo vivyo vyenye, koro iwa ni miro ya Muungu mwenye. Ela haata vivyo Muungu ewa na mupango wa kuvipfonya.

**21**Na ndiyo maana nsiku modza viumbe vyonse navyo vidzapfonywa kuyawana na hu uhumwa wa kwamba ni hadi vinangike, ili viweze kuupata hu uhuru wa mafara, wa hawa wana wa Muungu wadzeowa nao.

**22**Humanya kwamba haata hi hii saasambi viumbe vyonse vyakuuguyani na tsungu mukali dza tsungu wa muke jwa kuvyaa.

**23**Na si hivi viumbe tu, ela haata swiswi hupfegejweo Ruhu Mudheru dza hakikisho dya haya marembu hudzeyopfegwa baadaye, naswi pia hunakaa na kuuguya. Hwakuuguyani na kuindiiya na hamu muno hiyo hiyo nsiku ya Muungu adzeyohuhendeza wanawe kabisa, yani nsiku adzeyohuweka huru kuyawana na hi mii yehu.

**24**Kwa kwamba humapfonyegwa, hwakukuyoweeyani na hamu muno huku huku kuwekwa huru. Koro ni ga eyenayoweeya kukipata kintu echonacho tayari mukononi?

**25**Ela hwipfonaindiiya kintu husichodzakupata, hunaitisa muno.

**26**Dza vivyo, huyu Ruhu nae pia anakaa na kuhugija udhaifuni mwehu. Koro ntahudzi haata namuna hwivyonamala kuyomba. Ela huyu Ruhu jeje mwenye anakaa na kuhuyombea kwa Muungu muno huku akiwa kuuguyani na njia isiyoneneka.

- <sup>27</sup>Na Muungu, huyu aimanyiye myojo ya wantu kamanya hivi vya huyu Ruhu evyonanena, kwa dzambo ɔya kwamba huyu Ruhu anawayombea wantu wa Muungu kuubana na hivi vya Muungu evyonatsaka.
- <sup>28</sup>Humanya kwamba Muungu anahenda kula dzambo ɔipate kuwa dzema kwa hawaɔe wamutsakiyeo na awahaniyeo kuubana na mupangowe kwao.
- <sup>29</sup>Koro hawaɔe wa Muungu awatsaniyeo iide na iide, pia kawapangia kwamba wawe dza huyu Mwanawe, ili kwamba jeje awe ndiye huyu ndugu yao hangafa.
- <sup>30</sup>Hawaɔe wa Muungu awapangiyeo kuwa wanawe, kawahana. Na hawaɔe awahaniyeo kawahwaa kuwa wahachi, na hawaɔe awahwaiyeo kuwa wahachi, anawapfa maremboye.
- <sup>31</sup>Dubva kwa haya haya yonse hwambedze? Koro ikiwa kwamba Muungu ka yupfande jwehu, ni ga jwa kuweza kuhupfinga na ahushinde?
- <sup>32</sup>Huyu Mwanawe jeje mwenye tu, Muungu nkakumuhofea, ela kamuyavya dza mvuugiya kwa dzambo ɔya nabvise zehu hwonse. Dubva ikiwa kwamba huyu Mwanawe tu, kamuhupfa dzevihivi, dze, nkawezi kuhupfa mema yonse haɔa?
- <sup>33</sup>Haya, ni ga jwa kuhusiɔaki swiswi watsanwa wa Muungu? Ntaku yudejwonge! Koro Muungu mwenye ndiye ahuhendezeye kuwa wahachi usoni kwakwe.
- <sup>34</sup>Na ntaku yudejwonge jwa kuhuhukumu koro Kiristo Yesu ndiye afwiye, akifufuka na akikaa mukono kuyume wa Muungu, na jeje ndiye eyenahuyombea kwa Muungu.
- <sup>35</sup>Dubva ni ga eyenaweza kuhuɔanya na tsako ɔya Kiristo kwehu? Yuhangaiko ambu maɔina, vinaweza kuhuɔanya na tsako ɔya Kiristo? Kukuntiswa ɔina, nzaa ambu umasikini vinaweza kuhuɔanya na tsakoɔye? Ehe haɔari ideyonge ambu kifo vinaweza kuhuɔanya? Moro ntaviwezi!
- <sup>36</sup>Koro haɔa haya matsoro yamba, “Kula nsiku hwaa haɔarini ya kutsaka kuyagwa kwa dzambo ɔyako. Wantu wanahwaa sawa sawa na mbuzi za hako zizokupfiikwani kutsinzwani.”
- <sup>37</sup>Ela kwa haya haya yonse huna ushindi mkuu muno kuchiiya na kwa huyu ahutsakiye!
- <sup>38</sup>Koro nina hakika kwamba ntaku cha kuhuɔanya na hiɔi tsako ɔya Kiristo ahutsakiyeɔyo. Si kufwa kwehu wala kuishi kwehu, si malaika wala nguvu zidezonse za mpepfo nzuka zizonaweza kuhuɔanya na tsakoɔye. Na haɔa mambo yeyopfo ambu yadzeyokudza ntayawezi kuhuɔanya na tsakoɔye.
- <sup>39</sup>Ntaku kiɔechonse chicho mbinguni dzuu ambu lumwengu jwa wafu, wala kingine kiɔechonse kiumbijwecho, chichonaweza kuhuɔanya na namuna ya Muungu ahutsakiyevyo kuchiiya na kwa Kiristo Yesu.

## Warumi 9

<sup>1</sup>Haya niyokutsakani kunena nza ɗugha, koro mimi ni jwa Kiristo na siwezi kunena nsuwe. Haɗa haya maɗaro yangu yeyokuyongojwani ni huyu Ruhu Mudheru, nayo pia yakunimpani uhakika kwamba sikwakunenani nsuwe.

<sup>2</sup>Hachi mojoni mwangu nina ngiru na tsungu mwinji usiosia,

<sup>3</sup>kwa dzambo ɗya hawa wandugu zangu, Waisiraeli. Haɗa naɗamani kwamba heri Muungu andenid̄uwa mimi mwenye na anitanye na Kiristo kafu, ɗambere hid̄yo hid̄yo ɗindeweza kuwapfonya!

<sup>4</sup>Wao ni Waisiraeli, na ni wantu watsanijweo kuwa wana wa Muungu. Muungu kawayanga namuna aivyo na kahenda maɗamano nao na pia kawapfa hi Sharia yakwe. Wao wanamuyomba jeje Muungu jwa hachi na ndiwo wapfokeeyeo hizi ahaɗi za Muungu.

<sup>5</sup>Wabibi zao, (aɗe Ibrahimi na wanawe) wewa ni wantu wa Muungu. Na haɗa huyu Kiristo mwenye, kavyajwa dza mwanaaɗamu kuyawa chicho kyeeti chao cha Waisiraeli. Jeje ni Muungu eye dzuu ya vyonse na anamala kushaɗwa haɗa pfasipfosia! Amina.

<sup>6</sup>Sikwakunenani kwamba Muungu kayatsa kuiɗimiza hi ahaɗi awekeyeo kwa Waisiraeli haɗa. Koro si kula eye Muisiraeli kwamba ni mutsanwa jwa Muungu!

<sup>7</sup>Na wala si kula eye mudzukuu Ibrahimi kwamba ni mudzukuuwe jwa ɗugha. Haɗa Muungu kanena na Ibrahimi kamwamba, “Huju yuyee nikuahidiyejo unajupata kuchiiya na kwa Isaka,” ingawa Ibrahimi ewa na wana wangine.

<sup>8</sup>Hivi ni kunena kwamba, muntu akiwa mudzukuu Ibrahimi si kwamba ɓasi ni mwana jwa Muungu haɗa. Ela wana kindindi wa Ibrahimi ni hawaɗe wavyaijweo kuɓana na hi ahaɗi ya Muungu.

<sup>9</sup>Koro Muungu ewa kamuahidia Ibrahimi kamwamba, “Mwaka keso ngera dzehii nauja kwako kawii, na mukaziwo Sara anawa na mwanamuyume.”

<sup>10</sup>Na si hivyo ɗu, ela huyu huyu mwana, yani bibi jwehu Isaka, epfokuya kamuhwaa Rebeka na kavyaa nae mpatsa ya wanawayume wawii.

<sup>11</sup>Ela hangu hawa wana wepfokuwa ntawadzavyajwa, na wepfokuwa ntawadzahenda dzambo ɗideɗyonse dzema ambu zuka, Muungu kanena na mama jwao kamwamba, “Kyeeti cha huyu mukuu, kidzahumikia kyeeti cha huyu muɗoɗo.” Ndookomu vinayanga tswEE kwamba Muungu anamutsana muntu kuɓana na hiviɗe evyonapanga mwenye. Nkamutsane muntu kwa dzambo ɗya mahendoye.

<sup>13</sup>Dza vya matsoro yambiyevyo, “Yakobo nimutsaka, ela Esau nimudziza.”

<sup>14</sup>ɗubva hwambedze? Hwambe kwamba Muungu nkakuhenda hachi? Moro sivyo haɗa!



- 15**Koro Muungu ewa kamwamba Musa, “Namufwiya ƣei yuḁejwonse nitsakiye kumufwiya ƣei, na nawa munanso kwa yuḁejwonse nitsakiye kuwa munanso kwakwe.”
- 16**Ndookomu kutsanigwa kwa muntu, ntakudze kwa muntu kudzihendea hiḁu jeje mwenye ambu kwa kutsaka kwakwe jeje mwenye, ela ni kwa ƣei ya Muungu.
- 17**Koro humu matsoroni Muungu kamwamba Farao, “Nikuweka haju nangere ili niweze kuyanga uwezo wangu, na sari ḁyangu ḁipate kushaḁwa lumwengu yuzima.”
- 18**Ndookomu Muungu anamufwiya ƣei yuḁejwonse eyenatsaka kumufwiya ƣei, na huyuḁe eyenatsaka awe muḁiriri, anamuhendeza kuwa muḁiriri.
- 19**ḁubva wangine wenu wanaweza kuuza wambe, “Ikiwa kwamba niyohivyo, mani kuḁi Muungu anawaona wanaaḁamu kuwa watsovi, na hali katsi ntaku jwa kuweza kudziza kuhenda miro ya Muungu?”
- 20**Ela wewe mwanaaḁamu, hivi hivi nawe u ga, haḁa uweze kumwambukuya Muungu? Kuna nyungu ga iumbijweyo iyonaweza kumuuzwa huyu muntu aiumbiye ikamwamba, “Kuḁi wewe kuniumba dza avi niivyo?”
- 21**Hangu ḁura muntu eyenaumba vija vya haka, nkakwaa na hachi ya kuutumia au haka kuumbia kiḁechonse echonatsaka? Kuyawana na lingole modza ḁya haka, anaweza kuumba vija aina garagara. Vingine vinawa vya kutumika kwa mambo ya hila na vingine vinawa vya matumizi ya kawaiḁa.
- 22**ḁasi haḁa kwa Muungu vyaa dzevihivi. Ingawa Muungu ekitsaka kuiyanga hi ngoroye na ayange uwezowe eokuwa nao, kawaindiyya na kuwaiḁisia hawaḁe eowarejea, yani hawaḁe weonamala kunangwa-nangwa.
- 23**Na pia ekitsaka kuhuyanga swiswi ahufwiiyeo ƣei, namuna aivyo muḁei. Ekitsaka kuhuyanga uwezowe kwa dzambo ḁya kwamba swiswi ndiswi ahutsaniyeo huwe dza hiviḁe aivyo.
- 24**Swiswi ndiswi wantu huhanijweo ni Muungu. Na nkakuhuhana swiswi Wayahudi ƣu, ela haḁa wantu wa vyeeti vingine.
- 25**Hivi ndivyo aneneyevyo chuoni mwa Hosea. Kamba, “Hawaḁe wantu wasiokuwa wangu, nawahana, ‘Wantu wangu.’ Hikiḁe kyeeti nisichokitsaka ḁura, nakihana, ‘Kyeeti nitsakiyecho.’
- 26**Na pfapfaḁe pfantu niwambiiyepfo, ‘Ntamukwaa wantu wangu,’ ḁasi ndipfo pfantu wazepfohanigwa, ‘Wana wa Muungu eye moja.’ “
- 27**Nabii Isaya kalalabva dzuu ya Isiraeli kamba, “Ingawa wantu wa Isiraeli ni wenji dza mutsanga wa ḁahari, ni wantu wachuchu ƣu kahi yao wadzeopfonyegwa.

<sup>28</sup>Koro Muungu njwakujuhukumu lumwengu na ajwise kaḥisa pfasipfo kuḍaḍamaa.”

<sup>29</sup>Na kungine nabii Isaya kamba, “Ṭambere huyu Ḑwana mwenye nguvu zonse nkandehusazia yuvyee, swiswi Waisiraeli hwonse hundeewa hwisakunangwanangwa, dza midzi ya Sodoma na Gomora.”

<sup>30</sup>Ḑubva hivi hwivyokunenani ni kwamba, hawa wantu wa vyeeti vingine wahenda wahachi usoni kwa Muungu. Na wahenda wahachi kwa dzambo ḍya kumuhikiza Kiristo, ingawa ntawekidzilachia kuwa wahachi usoni kwa Muungu.

<sup>31</sup>Ela hawa Waisiraeli weowakidzilachia kuwa wahachi usoni kwa Muungu kwa kuuḅa hi Sharia, ntawakuweza kuiṭimiza na wawe wahachi.

<sup>32</sup>Kuṭi ntawakuweza kuwa wahachi? Ni kwa kwamba wekidzilachia kuwa wahachi usoni kwa Muungu kwa kuuḅa hi Sharia na kuhenda mahendo mema, ḅaḍala ya kuwa na faro kwa Kiristo. Ndookomu wakolasika na hiḍi iwe ḍiḍyonakolasa wantu.

<sup>33</sup>Haya matsoro yanena dzuu yeḍihiḍi iwe yamba, “Ṭayowa, nyakuwekani iwe mudzini Sayuni. Ni iwe ḍya kuwahendeza wantu wakolasike wagwe. Na yuḍejwonse amuhikiziye huyu eye dza iwe, nkanagizwa yutswa meshi.”

## Warumi 10

- <sup>18</sup>Wanangu watsakwa, matsako yehu ni kutsaawa matsako ya vyyuwo na kanwa basi ha! Ni hadi yawe matsako ya dgha na huyayange na mahendo.
- <sup>19</sup>Hukihenda hivi, ndipfo hudzefomanya hakika ya kwamba hu wantu wa hi hachi, na ntahuwe na oga usoni kwa Muungu.
- <sup>20</sup>Kula pfa myojo yehu ipfonahudia, hunamanya ya kwamba Muungu kamanya zaidi ya hivi humanyiyevyo, koro kamanya kula kintu.
- <sup>21</sup>Dubva watsakwa, ikiwa kwamba myojo yehu ntaikwakuhandiani, ntahuwezi kuwa na oga hukwakumuyombani Muungu.
- <sup>22</sup>Na kula hwichonamuyomba anachihupfa, kwa dzambo dya kwamba hwakuzigijani hizi amuri zakwe na kuhenda yeyonamutsakiza.
- <sup>23</sup>Eyokuhuamuruni huhende ni kwamba, humuhikize Yesu Kiristo, huyu Mwanawe, na hutsakane dza vya Kiristo ahuamuriyevyo.
- <sup>24</sup>Kula eyenagija amuri za Bwana, anawa na haria na Bwana na Bwana anawa na haria nae. Hunavimanyadze ya kwamba ana haria naswi? Hunavimanya na huyu Ruhu Mudheru amuhupfiye.

## 1 Yohana 4

- <sup>1</sup>Watsakwa, namutsemuhikiza kula muntu eyenakwamba ana Ruhu. Ishinu wademeni nguzi muwaone kwamba huyu ruhu jwao weyena njwa Muungu dgha ambu ha. Koro humu lumwenguni, kwisakuhandaiya manabii wa nsuwe wenji na wenji.
- <sup>2</sup>Muntu eye na Ruhu jwa Muungu munamumanya hidzaa: akitamuka kwamba Yesu Kiristo kadza lumwenguni dza mwanaadamu, basi huyo muntu ana Ruhu jwa Muungu.

- <sup>3</sup>Ela yudejwonse ambiye Yesu Kiristo nkakudza dza mwanaadamu, huyo nka Ruhu jwa Muungu. Hiyo ni ruhu ya mupfinga Kiristo. Muisikia kwamba ijwakudza, na hi hii saasambi imaawa humu lumwenguni.
- <sup>4</sup>Ela nywinywi, wanangu watsakwa, mu wana wa Muungu, na muwashinda hawa manabii wa nsuwe. Muwashinda kwa kwamba, huyu awee kuzimuni mwenu ana nguvu kuchia huyu awee kuzimuni mwa hawa walumwengu.
- <sup>5</sup>Hawa hawa manabii wa nsuwe mbwa huju huju lumwengu. Weyonanenea yonse nza huju huju lumwengu, ndookomu hawa walumwengu wanawapfindiia.
- <sup>6</sup>Ela swiswi hu wantu wa Muungu. Na yudejwonse amumanyiye Muungu anahupfindiia. Na yudejwonse asikwaa muntu jwa Muungu nkahusikiiye. Dubva, kwe hi namuna, hunamanya ugaragara kahi ya Ruhu jwa hachi na ruhu jwa nsuwe.
- <sup>7</sup>Watsakwa, nahutsakane swiswi na swiswi kwa dzambo dya kwamba matsako yanayawa kwa Muungu. Na yudejwonse eye na matsako anayanga kwamba jeje ni mwana jwa Muungu na kamumanya Muungu.
- <sup>8</sup>Yudejwonse asiye matsako, nkamudzi Muungu, kwa dzambo dya kwamba Muungu ni Muungu jwa matsako.
- <sup>9</sup>Muungu kayanga tswee matsakoye kwehu, kwa kumuhuma lumwenguni Mwanawe madiani. Kamuhuma ili kwamba kuchiiya na kwakwe, hupate maisha ya kuunga na yuungo.
- <sup>10</sup>Matsako, ni haya ya kwamba Muungu kahutsaka haṭa kamuyavya Mwanawe kuwa mvuugiya ya kuyatsijwa nabvise zehu. Si kwamba swiswi hwiimutsaka!
- <sup>11</sup>Watsakwa, ikiwa kwamba hi hii ndiyo namuna ya Muungu ahutsakiyevyo, dubva, hunamala kutsakana swiswi na swiswi.
- <sup>12</sup>Gula ntaku amuoneye Muungu meshi. Ela hukitsakana swiswi na swiswi, Muungu anawa na haria naswi na wangine wanaona matsakoye kuchiiya na kwehu.
- <sup>13</sup>Hichi cha kuyanga ya kwamba hwakuishini Muunguni na ya kwamba Muungu kakuishini kuzimuni mwehu, ni huyu Ruhu jwakwe amuhupfiye.
- <sup>14</sup>Na vya kwamba huyu Baba kamuhuma Mwanawe adze awe mupfonya jwa lumwengu, huviona, na hwakuvisumwiiyani na wangine.
- <sup>15</sup>Yudejwonse ashuhudie ya kwamba Yesu ni Mwana jwa Muungu, Muungu kakuishini kuzimuni mwakwe, nae kakuishini Muunguni.
- <sup>16</sup>Haṭa naswi wenye huyamanya na hunadzikwāya haya matsako ya Muungu eyonayo kwehu. Muungu ni Muungu jwa matsako. Na yudejwonse eyekuishini na matsako, kakuishini Muunguni na Muungu kakuishini kuzimuni mwakwe.

<sup>17</sup>Maana ya matsako ya Muungu kungoreswa kuzimuni mwehu, ni kwamba, hutsekudzawa na oga nsiku ya kuhukumigwa wantu. Na ntahukudzawa na oga kwa kwamba haya maisha yehu humu lumwenguni, yaa dza haya maisha ya Kiristo.

<sup>18</sup>Pfepfonawa matsako, oga ntauwepfo. Matsako yangoreyeo yanamuyavya muntu oga. Koro muntu akishooga hukumu, vinayanga wazi kwamba matsakoye ntayadzangora.

<sup>19</sup>Muungu ndiye ahutsakiye jeje dura, na ndiyo maana naswi huna matsako.

<sup>20</sup>Ikiwa kwamba muntu kamba kamutsaka Muungu, na huku kamukeva ndugujwe, huyo ni munsuwe. Kwa dzambo dya kwamba, muntu nkawezi kumukeva ndugujwe eyenamuona na matso, kisa amutsake Muungu asiyemuona na matso.

<sup>21</sup>Dubva hi amuri ya Kiristo ahupfiyeyo ni hii: ya kwamba, kula amutsakiye Muungu ni hadi amutsake na ndugujwe.

## 1 Yohana 5

<sup>1</sup>Kula ahikiziye kwamba Yesu ndiye huyu Masiya, huyo ni Mwana jwa Muungu. Na yudejwone amutsakie babajwe muntu, kamutsaka na mwana jwa huyo muntu pia.

<sup>2</sup>Ikiwa kwamba humutsaka Muungu na huzigija hizi amuri zakwe, hunamanya hakika kwamba huwatsaka hawa wanawe.

<sup>3</sup>Koro kumutsaka kwehu Muungu, ni kuzigija hizi amurize. Na kuzigija amuri zakwe si vyumu haṭa,

<sup>4</sup>kwa dzambo dya kwamba, kula mwana jwa Muungu anajushinda huju lumwengu. Na kujushinda huju lumwengu, hunakaa na kujushinda kwa faro yehu.

<sup>5</sup>Ela eyenaweza kujushinda huju lumwengu ni ga? Ni huyude tu ahikiziye ya kwamba Yesu ni Mwana jwa Muungu.

<sup>6</sup>Yesu Kiristo mwenye ndiye adziye. Kadza kaṭopyegwa na madzi, na keha mwaziwe na kafwa. Na nkakuṭopyegwa tu, ela kaṭopyegwa na keha mwaziwe, kafwa. Na huyu Ruhu mwenye kashuhudia ya kwamba haya haya ni dughu, koro huyu Ruhu nkanene nsuwe.

<sup>7</sup>Kuna mashaahidi wahahu,

<sup>8</sup>nao ni huyu Ruhu, haya madzi, na hu mwazi. Na wonse wohahu wayanga ushaahidi unjiyananiyeo, kwamba Yesu kadza dza mwanaadamu.

<sup>9</sup>Ikiwa kwamba ushaahidi wa wantu hunauhikiza, basi ushaahidi wa Muungu una nguvu zaidi. Nao hu ushaahidi wakwe ni hu ayaviyeo dzuu ya Mwanawe.

- <sup>10</sup>Dubva yudejwone amuhikiziye huyu Mwana jwa Muungu, kamanya hakika ya kwamba haya haya ni dughha. Ela yudejwone asiyemuhikiza, kesakumuhendeza Muungu kuwa munsuwe, kwa kwamba nkakuhikiza haya ya Muungu aneneyeyo, dza ushaahiḍi dzuu ya huyu Mwanawe.
- <sup>11</sup>Na hu ushaahiḍi hwiwo nao ni huu wa kwamba, Muungu kahupfa maisha ya kuunga na yuungo. Na haya haya maisha kayahupfa na kwa Mwanawe.
- <sup>12</sup>Kula awee na haria na huyu Mwana jwa Muungu, anaishi maishi. Ela kula asikwaa na haria na huyu Mwana, huyo nka maisha.
- <sup>13</sup>Mimi nyakumworeani nywinywi haya mambo, nywinywi mumuhikiziyeo Yesu Kiristo Mwana jwa Muungu. Nyakumworeani mupate kumanya hakika ya kwamba muna maisha ya kuunga na yuungo.
- <sup>14</sup>Swiswi hunadzimukwatya Muungu, kwa kwamba, huna hakika ya kwamba, hukimuyomba kidechonse kuubana na miroye, jeje anahusikia.
- <sup>15</sup>Na kwa kwamba humanya ya kwamba, kula hwipfonamuyomba nkahudziziye kintu, hunawa na uhakika wa kwamba kula hwichonamuyomba anahupfa.
- <sup>16</sup>Muntu akimuona ndugujwe kahenda nabvise, ela si nabvise ya kumutsovyo maisha ya kuunga na yuungo, namuyombeye kwa Muungu, na Muungu anamumpa maisha. Nyakunenani hawaḍe wahendeyeo nabvise zisizowangiza kufwani. Ela kuna nabvise iyonangiza muntu kufwani, na sikwakunenani ya kwamba dzuu ye hi nabvise mumuyombe Muungu.
- <sup>17</sup>Kula hendo zuka ni nabvise, ela kuna nabvise isiyongiza muntu kufwani.
- <sup>18</sup>Humanya ya kwamba, ntaku muntu eyenawa mwana jwa Muungu kisa akakaiya kuhenda nabvise, koro huyu Mwana jwa Muungu anamwamia, na huyu Muzuka nkanamuhora.
- <sup>19</sup>Humanya ya kwamba hu wana wa Muungu, ela lumwengu jwone jwaa mikononi mwa Muzuka Shaatani.
- <sup>20</sup>Na pia humanya ya kwamba huyu Mwana jwa Muungu kadza, na kahupfa kuimuka hupate kumumanya huyu Muungu jwa dughha. Naswi hwakuishini kuzimuni mwa huyu Muungu jwa dughha, koro hwaa kuzimuni mwa huyu Mwanawe, Yesu Kiristo. Na huyu ndiye huyu Muungu jwa dughha na ndiye eye na haya maisha ya kuunga na yuungo.
- <sup>21</sup>Wanangu watsakwa, dziṭunzeni na miungu ya nsuwe.

## 2 Yohana

### 2 Yohana 1

<sup>1</sup>Mimi muzee, nyakukworeani wewe muke utsanijwee ni Muungu. Nyakukworeani wewe na wanao nimutsakiyeo muno. Simi tu nimutsakiyee, ela haṭa na hawaḍe wonse waimanyiyeo hi hachi. Wamutsaka

<sup>2</sup>kwa dzambo ḍya kwamba hi hachi yaa kuzimuni mwehu na inawa naswi maishi.

<sup>3</sup>Muungu Baba, na Yesu Kiristo, Mwana jwa huyu Baba, nawahuvodhye nto, wahufwiye ṭei na kuhupfa maisha ya naghea. Na wanavihupfa ikiwa kwamba hukaa hachini na matsakoni.

<sup>4</sup>Ami niwa na tsekea hii, nipfokudza nikiwaona wangine wa hawa wanao wakuishini hachini, dza viviḍe vya Baba ahuamuriyevyo!

<sup>5</sup>Dubva wewe muke utsakijwe, nichokukworeani kukuyomba, ni kwamba hutsakane swiswi na swiswi. Hi hii amuri si amuri ngeni haṭa, ni iḍe amuri hwiyo kuwa nayo hangu ḍabvu.

<sup>6</sup>Haya matsako niyokunenani ni kwamba, ni haḍi huzigije hizi amuri za Muungu. Na dza musikiiyevyo hangu ḍabvu, hi amuri yakwe ni hii ya kwamba, muishi maisha ya matsako.

<sup>7</sup>Humu lumwenguni kuhika waalimu wenji na wenji weo na makulekule. Hawa ni wantu weokudzizani kuhikiza ya kwamba Yesu Kiristo kadza dza mwanaadamu. Wantu dzao ni wapfinga Kiristo na ni wantu weonakulakula.

<sup>8</sup>Dubva dziṭunzeni, ili kazi zenu muhendeyezo zitsekudzadziaria ḅasi, ela mudzemupate maipfo yenu mazima!

<sup>9</sup>Yuḍejwone eyenayawa nze ya mayongweezo ya Kiristo, akavuka mimpaka, huyo nka haria na Muungu. Ela yuḍejwone eyenakaa kuzimuni mwa haya mayongweezo, ana haria na huyu Baba na huyu Mwana.

<sup>10</sup>Dubva muntu yuḍejwone akimudzia, na akitsamudzia na haya haya mayongweezo, namutsemukarabisha nyumbani kwenu. Na haṭa kumukedhya, namutsemukedhya!

<sup>11</sup>Koro yuḍejwone amukarabishiye muntu dzae nyumbani mwakwe, kakugijanani nae kuhenda haya mazukaye.

<sup>12</sup>Nina menji na menji ya kukwambia, ela sikitsaka kuyakworea yonse humu baruwani. Nyakuyoweeyani ya kwamba nakuṭembeeya, ninene nawe kanwa na kanwa, ili hupate kunjijwa ni tsekea ṭipu.

<sup>13</sup>Hawa wana wa imbuḍyo atsanijwe ni Muungu, nao wakukedhya nto.

## 3 Yohana

### 3 Yohana 1

- <sup>1</sup>Mimi muzee, nyakukworeani wewe ɓamu jwangu Gayo nikutsakiyee muno.
- <sup>2</sup>ɓamu jwangu mutsakwa, nyakukuyombeani ya kwamba mambo yakwendeye urembo na uwe na matsea mwiini. Nimanya ya kwamba kiruhu le nku untu.
- <sup>3</sup>Ami ninjijwa ni tsekea hii kwipfokudza wangine wa hawa wandugu, wakidza wakisumwiiya namuna ugijiyevyo kusumama hachini, dza nikumanyievyo ya kwamba u muntu wiyenaishi hachini!
- <sup>4</sup>Ntaku kintu chichonanitsekeza dza kusikia ya kwamba, hawa wanangu watsakwa wakuishini hachini.
- <sup>5</sup>Mutsakwa jwangu, kazi wiyokuwahendeani hawa wandugu weonazunguuka na kusumwiiya, ni kazi ya kuhikizika muno, haɓa ingawa wao ni wantu usiowamanya.
- <sup>6</sup>Hawa hawa wantu waɗisumwiiya hiɗi tsanganiko dzuu ya haya matsakoyo kwao. ɗinawa dzambo dzema ukiwangiza kwendeleani na charo chao na njia ya kwamba inamutsakiza Muungu.
- <sup>7</sup>Koro wepfonjia charo cha kwenda na kuhenda kazi ya ɓwana, wadziza kupfokea ugijo uɗewonse kuyawa kwa wantu wasiokuwa wahikiza.
- <sup>8</sup>ɗubva swiswi hunamala kuwapfa ugijo wa kula namuna hawa wantu, hupate kugijijana nao kwa hi kazi ya kusumwiiya hi hachi.
- <sup>9</sup>Niwa nyora ɓaruwa mfufi kwa hiɗi tsanganiko ɗya huko kwenu. Ela Diotirofe, adzihendezeye kitsampizi, kadziza kunisikia.
- <sup>10</sup>ɗubva nidzefokudza, haya yonse ahendeyeyo nayabaaba tswee. Kakuhungiziani mambo mazuka mazuka menji na menji. Na dza kwamba hiɗyo hiɗyo ntaɗikuɗosa, kanjia kudzizani kuwapfokea hawa wandugu. Ana haɓa kuwavingira hawaɗe weonatsaka kuwapfokea, na haɓa akawayavya tsanganikoni!
- <sup>11</sup>Mutsakwa, nkudzotaɓe myenendo mizuka, taɓa myenendo myema. Kula eyenahenda mema huyo njwa Muungu. Ela kula eyenahenda mazuka nkadzamumanya Muungu.
- <sup>12</sup>Wantu wonse wakunenani wema wa Demetirio. Na haɓa namuna eyonakigija hichi chuuwo cha hachi, vinayanga kwamba ni muntu mwema. Naswi hwakwongezani na ushaahiɗi wehu, nawe mwenye kumanya ya kwamba hwichokunenani swiswi ni ɗugha.
- <sup>13</sup>Nina menji na menji ya kukwambia, ela si haɗya ya kuyakwambia yonse na ɓaruwa.



<sup>14</sup>Nyakudzikwatyani ya kwamba hunaonana si haṭa kae, na hunanena kanwa na kanwa.

<sup>15</sup>Ikaa naghea. Hawa waḅamuzo wonse weo huku wakukedhya nto. Naswi hukedhyeye waḅamu zehu wonse weo huko huko, mumodza kwa mumodza.

## Yuda

### Yuda 1

- <sup>1</sup>Mimi Yuda ndugujwe Yakobo, niye muhumisi jwa Yesu Kiristo, nyakumworeani nywinywi nyonse muhanijweo ni Muungu Baba muwe wantuwe. Jeje kamutsaka muno na mwakwamijwani ni Yesu Kiristo.
- <sup>2</sup>Muungu namufwiye ũei na kumumpa nagheaye na matsakoye kwa winji.
- <sup>3</sup>Watsakwa, gula ninkitsaka muno kwamba nimworeye dzuu ya hu mupfonyo huupatiyeo hwonse. Ela niona kwamba ni urembo nimworeye kwamba muyaheheye haya Maagu Mema muyahikiziyeyo. Hi hachi ya haya haya Maagu Mema, Muungu kaiyavya kwa hawaũe wonse weo wakwe na ntaiperuke meshi.
- <sup>4</sup>Nyakunenani hivi kwa kwamba kuna wantu wangine wasiomumanya Muungu wadzinyeezeyeo-nyeezeyeo wakinjia kahi yenu. Hawa hawa wantu wakuyongweezani kwamba, aũi hunaweza kugija kuishi maisha ya kuuũa ũamaa nzuka nzuka za kimwii koro Muungu anahufwiya ũei. Hukumu ya hawa hawa wantu iyavigwa hangu kae na kae, koro wamukana huyu Bwana jeje hekeũu hwiyenae, yani Yesu Kiristo.
- <sup>5</sup>Natsaka kumukumbusya kwamba ingawa Bwana ewa kakipfonya kyeeti cha Muisiraeli kuyawa Misiri, ɓaaũaye kadza kawananga-nanga hawaũe wonse wayatsiyeo kumuserefaũa. Gula nimanya ya kwamba haya haya ni mambo muyamanyiyeyo urembo muno, ela nikitsaka kumukumbusya ũu.
- <sup>6</sup>Na pia natsaka kumukumbusya kwamba hawaũe malaika wayayatsiyeo haya mamulaka ya Muungu awapfiyeyo, na wakikuyatsa hukuũe kuntu kwao wapangiijweko kukaa, Muungu kawafunga-funga na minyoro isiyohunika meshi. Kisa kawangiza simo dya kiza wemokuindiiyani Nsiku ya kuhukumigwa.
- <sup>7</sup>Kumbukani wantu wa midzi ya Soɗoma na Gomora na hiũe midzi ingine iyokuwa hafufi. Hawa hawa wantu wekihenda kula aina ya uɓari na kuyaana na njia isiyokuwa ya sawa, ndookomu Muungu kawananga-nanga na moho. Hihiiũe midzi Muungu kaihenda dza hivihiviũe nangere kuyanga namuna ya hawaũe wonse weo wazuka wadzevyotsomwa na moho usiwosia.
- <sup>8</sup>Hivi hivi ndivyo vya hawa waalimu wa nsuwe waivyo. Haya mandoho yao weyonayoha yanakaa na kuwahendeza wakaingiza mii yao kuhendani mambo machafu. Wanakaa na kunyira mamulaka ya Muungu na kuvitsola-tsola ɓasi viumbe vya mbinguni.
- <sup>9</sup>Bela Mikaeli eye mumodza jwa hawa malaika wakuu ũu, nkakusubuũu kumutsola Shaatani epfoakiɗaaũiana nae dzuu ya hu mwii wa Musa. Ishinu kamwamba, "Bwana nakuhukumu!"

- 10**Ela hawa waalimu wa nsuwe wanatsezea kula wasichokiimuka. Wanadzihendea mambo dza binensa pfasipfo kuṭara na wakadzingiza mananzini wao wenye.
- 11**Hachi wadzawa na ḍina nkuu muno! Koro wakuhendani dza hiviḍe vya Kaini amuyagiyevyo ndugujwe. Wao ni wantu watsakiyeo fwedha dza hiviḍe vya Balamu evyokuwa. Na kwa kwamba wamutsowea Muungu, wananangwanangwa dza hiviḍe vya Kora evyotsowa na akinangwanangwa.
- 12**Wepfonakaa kuḍyani pfamodza nanywi dza wantu wa Ḑwana, wanamungiza ṭamba zuka kwa dzambo ḍya kwamba, wanakaiya kudzimuḍamia wao hekeṭu pfasipfo haṭa yutswa. Hawa hawa waalimu wa nsuwe waa dza mawingu ya mvuya yeyonabigwa ni vuṭo ḥasi na yakatsayeha mvuya iḍeyonse. Waa dza mihi isiyovyaa matunda haṭa ikiwa kwamba ni ngera ya kwamba iwe na matunda. Waa dza mihi ifwiyeo na ikikujwa-kujwa na miziye.
- 13**Haya mahendo yao mazuka mazuka yanadziyavya nze tswee dza hiviḍe vya mawimbi makali ya ḥahari yevyonabiga na kuyavya povu ḍya uchafu. Wao waa dza hiziḍe nyoha zizonadzichiiya ḥasi humu yuwinguni, yani hiziḍe nyoha zizonachia zikaariya kuntu kwa kiza cha go.
- 14**Henoke eyeishi kivyazi cha fungahe ḥaada ya Aḍamu ewa kayavya unabii dzuu ya wantu dza hawa hawa epfokwamba, “Ṭayowa, Ḑwana kakudzani na maelefu na maelefu ya malaikawe.
- 15**Kakudzani kuwahukumu wantu wonse weo lumwenguni. Kadzawahukumu wanabvise wonse wasiomumanya Muungu. Kadzawahukumu kwa dzambo ḍya haya mahendo yao mazuka yonse wahendeyeo pfasipfo haṭa kumushooga Muungu. Na pia kadzawahukumu kwa dzambo ḍya hivi vyuuwo vizuka vizuka vyonse vya hawa hawa wantu waneneyevyo dzuu ya Muungu.”
- 16**Hawa hawa waalimu wa nsuwe ao meshi kazi yao ni kuḥuguma-ḥuguma na kualaṭa wantu wangine. Wanakaa na kuḥa hizi ṭamaa zao nzuka nzuka na kudziona kwinji, na wakashaḍa wantu ili waweze kuonegwa wema.
- 17**Ela wandugu zangu watsakwa, ni haḍi mukumbuke haya ya hawa ntumi wa Ḑwana jwehu Yesu Kiristo wamwambiiyeo.
- 18**Wamwamba, “Ngera za mviso kudzawa na wantu weo na baladha weonaṭawaligwa ni ṭamaa zao nzuka nzuka pfasipfo haṭa kumushooga Muungu.”
- 19**Hawa hawa ndiwo weonaḥaa wantu viṭaro viṭaro. Wanaṭawaligwa ni hizi ṭamaa zao za kimwii ṭu, koro Ruhu jwa Muungu nkapfo kuzimuni mwao.
- 20**Ela nywinywi waḥamu zangu, ni haḍi mugije kuyambaka maisha yenu dzuu ya hu musinji we faro yenu iyawiyeyo kwa Muungu, na mugije kuyomba kuḥana na hiviḍe vya Ruhu Mudheru evyonamuyongowa.

<sup>21</sup>Gijani kuishi kuubana na matsako ya Muungu, huku mukwakuindiiyani kupata haya maisha ya kuunga na yuungo mudzeyopfegwa ni Bwana jwehu Yesu Kiriṣṭo kwa dzambo dya hi ṭeiye eyonayo kwenu.

<sup>22</sup>Ikaani mukiwafwia ṭei hawaḍe weo na faro zizokutsakani kupfunguya.

<sup>23</sup>Wangine wapfoweni muwapfonye kuyawana na haya makaa ya moho weyokutsakani kunjia. Kuna na wangine weo wanabvise mwiwonamala kuwafwiya ṭei, ela chimizani watsekudzamuhendeza mugwe nabviseni munjie ṭamba zuka.

<sup>24</sup>Na sasa Muungu ashadwe. Jeje ndiye eyenaweza kumuṭunza mutsekudzagwa nabviseni na anamungiza maremboni mwakwe mukiwa na tsekea nkuu muno, koro munawa kwamba ntamu haṭa kaṭamba ka nabvise.

<sup>25</sup>Muungu eye Mupfonya jwehu jeje hekeṭu ashadwe kuchiiya na kwa Bwana jwehu Yesu Kiriṣṭo. Marembo, nguvu, uhaju na mamulaka, mvyakwe hangu ngera zichiiyezo, sasa, na haṭa pfasipfosia. Amina.

## Upfenuo wa Yohana

### Upfenuo wa Yohana 1

<sup>1</sup>Haya ni mambo ya Yesu Kiristo ayanipfenwiiyeyo mimi Yohana. Kayapfegwa ni Muungu awayange wahumisiwe haya ya kwamba ni hađi yahendeke si hađa kae. Nae Yesu kahuma malaika jwakwe kwangu mimi muhumisijwe, kuyanipfenwiiya haya yadzeyohendeka.

<sup>2</sup>Nami nyora hayade yonse niyangijweyo. Nyora hi ya hachi dzuu ya hichi chuuwo cha Muungu na haya niyangijweyo dzuu ya Yesu Kiristo.

<sup>3</sup>Kadzawa na tsekea iyodze huyude adzeevisoma hivi hivi vyuo vya unabii, na wadzawa na tsekea iyodze hawade wadzeovisikiya na kuvihwaa na moja. Koro ngera ya haya mambo kuhendeka imaawa hafufi.

<sup>4</sup>Mimi Yohana, nyakumworeani nywinywi wantu wa matsanganiko mofungahe yeyo dyimbo dya Asia. Huyu eyekwapfo, eyepfo na adzeyekudza, pfamodza na hizi ruhu mfungahe zizonasumama usoni ya kitiche cha kihaju na Yesu Kiristo eye shaahidi jwa kuhikizika, nawamuvodhye na kumumpa naghea nto. Yesu Kiristo ndiye jwa dura afufukie kuyawa kwa wafu na akiwa Haju jwa mahaju yonse ya humu lumwenguni. Jeje kahutsaka na kahuweka huru kuyawana na nabvise kwa kwiha mwaziwe.

<sup>6</sup>Kahuhendeza huwe wantu wa Uhajuwe na wakohani wa kumuhumikia Muungu Babajwe. Dubva jeje Yesu nashadwe na kukuzwa maishi na maishi. Amina.

<sup>7</sup>Tasikiani! Yesu kakudzani! Kakudzani na mawingu na kula dzitso didzamuona. Hađa hawade wamusimikiyeo wakimuyaga nao pia wadzamuona. Na vyeeti vyonse vimudziziyevyo, vidzasikitika kwa dzambo dya kudzakwe. Na ndivyo vidzeyowa! Amina.

<sup>8</sup>Bwana Muungu mwenye nguvu zonse, jeje eyekwapfo, eyepfo na adzeyekudza, kamba, "Mimi ndimi Dabvu na Mwisu. Ndimi niyenadabvisa mambo yonse na ndimi niyenayesa."

<sup>9</sup>Mimi ndugu yenu Yohana, nyakukuntiswani dina dzanywi kwa dzambo dya Yesu Kiristo. Nyakuuyoweyani Uhaju wa Muungu na kuitisa madinani dzanywi kwa dzambo dya Yesu. Mimi nisamiswa nipfiikwa kilulu cha Patimo, kwa dzambo dya kuyongweeza chuuwo cha Muungu na kusumwiiya wantu dzuu ya Yesu.

<sup>10</sup>Nsiku modza ya Bwana, niwa Ruhuni. Nisikia sauti nkuu nyuma yangu iyokuwa dza sauti ya tarumbeta.

<sup>11</sup>Hi sauti inyamba, "Haya wiyokuyaonani, yore uyapfiike kwa haya matsanganiko mafungahe yeyo dyimbo dya Asia. Yapfiike kwa tsanganiko dya Efeso, Simirina, Pagamo, Thiatira, Saridi, Filadelifia na Laodekia."

<sup>12</sup>Nipfoperuka ili nimuyowe huyu eyeakinena nami, niona mihi mifungahe ya dhahaḅu ya kupfatsikia tsaa.

<sup>13</sup>Na kahikahi ya hi mihi ya kupfatsikia tsaa, niona muntu kasumama. Huyu ewa dza Mwana jwa Aḁamu. Ewa kavwaa loṭa ḁiḁyomufika mumpaka nyajoni, na kadzifunga mukanda wa dhahaḅu na hapfa ḅagwini.

<sup>14</sup>Hizi nywiize ziwa nyeupe pee! Ziwa nyeupe dza sufi. Na haya matsoye yewa dza maḅilibili ya moho.

<sup>15</sup>Maguuye yekingara dza shaḅa ingizijweyo mohoni ikiḁauswa na ikiyavigwa uchafu wonse. Na hi sautiye iwa dza sauti ya mvuha ya madzi menji.

<sup>16</sup>Mukono wakwe wa kuyume ewa kagija nyoha mfungahe. Kanwani mwakwe kwikiyawa yupfanga jwijokuwa na makai kuwii. Na hu uso wakwe wikiyangaa dza dzuwa ḁya musikahi.

<sup>17</sup>Mimi nipfomuona, nimugwiya maguuni pfakwe, na nikaa dza muntu afwiye. Ela jeje kaniweka mukono wakwe wa kuyume na kanyamba, “Nkudzoshooḡe! Mimi ndimi ḁabvu na mwiso.

<sup>18</sup>Mimi ndimi huyu niye moja. Niwa nifwa, ela sasa nya moja maishi na maishi. Mimi nina mamulaka dzuu ya kufwa na dzuu ya lumwengu jwa wafu.

<sup>19</sup>ḁubva wewe, yore haya mambo uoneyeo, yeyokuhendekani na yadzeyohendeka ḅaaḁaye.

<sup>20</sup>Na siri ya hiziḁe nyoha mfungahe uoneyezo nikizigija na mukono wangu wa kuyume na hiḁe mihi mifungahe ya dhahaḅu ya kupfatsikia hizi tsaa ni hii: Hizi nyoha zomfungahe ni malaika wa haya matsanganiko mafungahe. Na hi mihi myofungahe ya hizi tsaa, ni haya matsanganiko mafungahe.”

## Upfenuo wa Yohana 2

<sup>1</sup>Huyu eyekuwa dza Mwana jwa Aḁamu kagija kunena nami kanyamba, “Kwa huyu malaika jwa tsanganiko ḁya Efeso, mworeye umwambe, ‘Huyu azigijiye hizi nyoha mfungahe na mukono wakwe wa kuyume na eyenakwenenda kahi ya hi mihi mifungahe ya dhahaḅu ya kupfatsikia tsaa, kamba hivi:

<sup>2</sup>Mimi niyamanya mahendo yenu yonse. Nimanya kuiṭisa kwenu na hiḁu yenu ya kunikumikia. Nimanya ya kwamba ntamuwezi kuiṭisiana na wantu wazuka. Na haṭa hawa weonadzihendeza kuwa ntumi wangu, nywinywi muwapima na muwahambuya kwamba ni wansuwe.

<sup>3</sup>Nimanya namuna mwivyokuiṭisani maḁinani pfasipfo kudhimwa kwa dzambo ḁyangu.

<sup>4</sup>Ela kuna dzambo modza ḁisiḁyonitsakiza. Naḁyo ni hiḁi ḁya kwamba, hiḁiḁe tsako mwiḁyokuwa naḁyo ḁura, sasa ntamu naḁyo kawii.

<sup>5</sup>Kumbukani hapfāde mugwiyepfo napfo, mupfyehuze mama na muwe dza hapfāde dūra mwipfonihikiza. Ambu sivyo, nakudza naunuya pfantupfe hu muhi wenu wa kupfatsikia tsaa.

<sup>6</sup>Haṭa vivyo, muna dzambo modza dzema mwiḍyokuhendani. Naḍyo ni hiḍi ḍya kwamba, nywinywi muyakeva mahendo ya Wanikolai dza hivi vyangu niyakeveyevyo.

<sup>7</sup>Dubva eye na masikio, nasikiye hivi vya huyu Ruhu evyokuyambiani matsanganiko. Na kula adzeyeshinda, namumpa hachi ya kuḍya matunda ya muhi wiwonapfa wantu maisha, wiwo Paradisoni mwa Muungu.’ “

<sup>8</sup>Kisa huyu eyekuwa dza Mwana jwa Aḍamu kanyamba, “Kwa huyu malaika jwa tsanganiko ḍya Simirina, mworeye umwambe, ‘Huyu eye ḍabvu na mwisu, na afwiye kisa akifufuka, kamba hivi:

<sup>9</sup>Mimi nimanya ḍina mwizonazo na umasikini wenu mwiwo nao. Ela kunena hiḍe ya hachi nywinywi mu majabva! Nimanya haṭa hu uzuka wa hawa wapinzani wenu weokumuneneani. Wao wakudzihanani wantu wa Muungu na hali huku ni wantu wa Shaṭani.

<sup>10</sup>Mudzakuntiswa ḍina zaiḍi na zaiḍi mahafufini. Ela namutseshooga. Ṭasikiani, Shaṭani njwakumuyehea maḍemo ya kuhendeza wangine wenu wangizwe magerenzani. Munawa ḍinani kwa muḍa wa nsiku kumi. Nywinywi haṭa ni kufwa fwani, ela namutseyekeza faro yenu. Nami namumpa ṭubvo ḍya maisha ya kuunga na yuungo.

<sup>11</sup>Eye na masikio, nasikiye hivi vya huyu Ruhu evyokuyambiani matsanganiko. Na kula adzeyeshinda, huku kufwa kwa pfii kwa maishi na maishi, ntakuwezi kumupata.’ “

<sup>12</sup>Huyu eyekuwa dza Mwana jwa Aḍamu kagija kunena nami kanyamba, “Kwa huyu malaika jwa tsanganiko ḍya Pagamo, mworeye umwambe, ‘Huyu eye na yupfanga jwijo na makai kuwii, kamba hivi:

<sup>13</sup>Mimi nimanya kwamba huku mwikokuishini ndiko kwa Shaṭani mwenye ekoḱuṭawalani. Ela faro yenu kwangu muigija gu! Na haṭa masiku ya Antipa shaahiḍi jwangu muhikizika, epfoyagwa humo mudzini mwenu, wiwo makao ya Shaṭani, nywinywi ntamukuuja na nyuma.

<sup>14</sup>Haṭa vivyo, kuna mambo machuchu yeyokuhendekani yasiyonitsakiza. Wangine wenu wakuuḅani njia ya Balamu, amuyongweezeye Balaki kuwakulakula Waisiraeli wagwe nabviseni na wanjie kuhendani uḅari na kuḍya vyakuḍya viyavijwevyo mvuugiya kwa miungu ya nsuwe.

<sup>15</sup>Na haṭa kahi yenu pia, kuna wantu weokuuḅani mayongweezo ya Wanikolai.

<sup>16</sup>Dubva pfyehuzani mama! Ambu sivyo namudzia dza kupfesa nidzenijwane nao na yupfanga jwijonayawa kanwani mwangu.

<sup>17</sup>Eye na masikio, nasikiye hivi vya huyu Ruhu evyokuyambiani matsanganiko. Na kula adzeyeshinda, namumpa sehemu ya hiḁe mana ifitsijweyo na namumpa iwe dzeupe ḁyorejweḁyo sari ipfya ḁisidyomanyigwa ni yuḁejwonse, lamuḁa huyu adzeyedipfegwa.’ “

<sup>18</sup>Kisa huyu eyekuwa dza Mwana jwa Aḁamu kanyamba, “Kwa huyu malaika jwa tsanganiko ḁya Thiatira, mworeye umwambe, ‘Huyu Mwana jwa Muungu, eye na matso yeyo dza maḁilibili ya moho na eye na maguu yeyonangara dza shaḁa ikolejweyo, kamba hivi:

<sup>19</sup>Mimi niyamanya mahendo yenu yonse. Nimanya matsako yenu, faro yenu, kuiḁisa kwenu na uhumisi wenu. Na nimanya kwamba haya mwiyo kuhendani hi hii saasambi, yachia hayaḁe mwiyo mukihenda ḁura.

<sup>20</sup>Ela kuna dzambo modza ḁidyokuhendekani ḁisidyonitsakiza. Naḁyo ni hiḁi ḁya kwamba, huyu muke eyenahanwa Yezebeli, eyenadzihana nabii, mwakumuyatsani awaarye wantu wangu. Jeje kakuwayongweezani wantu wangu kuhenda uḁari na kuḁya vyakuḁya viyavijwevyo mvuugiya kwa miungu ya nsuwe.

<sup>21</sup>Mimi nimumpa muḁa wa kupfyehuzi mama, ela jeje kadziza kuyatsa uḁariwe.

<sup>22</sup>ḁubva nijwakumugisa chisa na nḁwari! Hangu jeje na hawa weokuhendani uḁari nae, nawabiga na nḁwari nzuka muno ikiwa kwamba ntawakupfyehuzi mama wayatse haya weyokuhendani.

<sup>23</sup>Wonse weokuuḁani mayongweezoye nawayaga tswee! Na matsanganiko yonse yanamanya kwamba mimi ndimi nimanyiye moja wa kula muntu na maḁaroye. Nami kula mumodza jwenu namuipfa kuuḁana na mahendoye.

<sup>24</sup>Ela kuna wangine wenu huko Thiatira mudziziyeyo kuyauḁa haya mayongweezo ya Yezebeli na ntamukudzingiza kwa haya ya wantu wangine weyonakwamba ni “ngadzi za Shaḁani.” Mimi nami siwezi kumupfaza muzigo ungene zaiḁi.

<sup>25</sup>Changu tu cha kumwambia ni kwamba, gijani muno hikiḁe mwichonacho mumpaka hapḁe nidzefokudza.

<sup>26</sup>Kula adzeyeshinda na akigija kuniḁii mumpaka mwisu, nidzamumpa mamulaka dzuu ya wantu wa vyeeti

<sup>27</sup>dza viviḁe vya Baba animpiyevyo mamulaka. Nae kadzawaḁawala na nsimbo ya chuma na kuwavunza-vunza dza nyungu za haka. Nami nidzamumpa nyoha ya magura kuyanga kwamba ni mushindi.

<sup>29</sup>Eye na masikio, nasikiye hivi vya huyu Ruhu evyokuyambiani matsanganiko.’ “

### Upfenuo wa Yohana 3

<sup>1</sup>Huyu eyekuwa dza Mwana jwa Aḁamu kagija kunena nami kanyamba, “Kwa huyu malaika jwa tsanganiko ḁya Saridi, mworeye umwambe, ‘Huyu eye na hizi



ruhu mfungahe za Muungu na hizi nyoha mfungahe, kamba hivi: Mimi nimanya mahendo yenu yonse. Munaonekana dza wantu mwiwo moja, katsi huku mufwa.

<sup>2</sup>Dubva yamukani! Yafufuyeni hayađe yasaiyeo yeyokutsakani kufwa. Koro niona kwamba mahendo yenu ntayadzafikia hiviđe vya Muungu jwangu evyonatsaka.

<sup>3</sup>Kumbukani hayađe mwiyojongweezwa na mwiyoopfokea. Yagijeni na mupfyehuze mama. Ela mukitsayamuka, namudzia dza mwivi, wala ntamumanye saa yangu ya kumudzia.

<sup>4</sup>Hađa vivyo, huko Saridi kuna wachuchu wasiodzayangiza uchafu mavwazi yao. Nao wanakwenenda nami wakiwa wavwikwa nguo nyeupe pee, koro wana hachi ya kuvwikwa dzevihivi.

<sup>5</sup>Kula adzeyeshinda, anavwikwa nguo nyeupe dzao. Nami saridye siwezi kuđifuta kuyawa kwa hichi Chuo cha Maisha. Nanena usoni kwa Baba na malaikawe kwamba huyu ni muntu wangu.

<sup>6</sup>Eye na masikio, nasikiye hivi vya huyu Ruhu evyokuyambiani matsanganiko.’ “

<sup>7</sup>Kisa huyu eyekuwa dza Mwana jwa Ađamu kanyamba, “Kwa huyu malaika jwa tsanganiko đya Filadelifia, mworeye umwambe, ‘Huyu eye Mudheru na Muhikizika, eye na yufunguo jwa Đauđi na ambaye kwamba akifunguya muđyango ntaku eyenaweza kuufunga na akifunga muđyango ntaku eyenaweza kuufunguya, kamba hivi:

<sup>8</sup>Mimi niyamanya mahendo yenu yonse. Nimanya kwamba ntamukwaa tsanganiko kuu đidyo na nguvu muno, ela mukigija chuuwo changu na nguvu na wala ntamudzanikana. Nami nimufungwiiya muđyango usoni yenu na ntaku adzeyeweza kuufunga.

<sup>9</sup>Tasikiani! Kuna wantu weokudzihanani wantu wa Muungu na hali huku ni wantu wa Shaatani. Hao nawahendeza wadzewamugwiye maguuni, nao wanahambuya kwamba mimi nimutsaka.

<sup>10</sup>Na kwa kwamba nywinywi muiđisa dza niviyomuamuru, nami namuchinga ne đina idzeyokudza kuwađema wantu wonse weo lumwenguni.

<sup>11</sup>Mimi nyakudzani si hađa kae! Kigijeni muno hikiđe mwichonacho ili muntu atsekudzamupfoka tubvo đyenu.

<sup>12</sup>Kula adzeyeshinda, namuhendeza kuwa nguzo kuzimuni mwa Hekalu ya Muungu jwangu na wala nkawezi kuiyawa kawii meshi. Nami dzuu yakwe nakwora sari đya huyu Muungu jwangu, nae anawa muntu jwa mudzi mupfya wa Muungu yani Yerusalemi mpya idzeyoyawa mbinguni kwa Muungu. Na pia nakwora sari đyangu ipfya dzuu yakwe.

<sup>13</sup>Eye na masikio, nasikiye hivi vya huyu Ruhu evyokuyambiani matsanganiko.’ “

<sup>14</sup>Yesu kagija kunena nami kanyamba, “Kwa huyu malaika jwa tsanganiko ɗya Laodekia, mworeye umwambe, ‘Huyu eyenahanwa Amina, eye shaahiɗi muhikizika jwe hachi na ambaye kula kintu kiumbwa kuchiiya na kwakwe, kamba hivi:

<sup>15</sup>Mimi niyamanya mahendo yenu yonse. Ntamukwaa mpepfo wala ntamukwaa moho. Mukwakuwa mpepfo ni heri muwe mpepfo na mukwakuwa moho ni heri muwe moho!

<sup>16</sup>Ela kwa kwamba nywinywi mwaa kavumbugo ɓasi, ntamukwaa mpepfo wala ntamukwaa moho, mimi nijwakumuhapfika!

<sup>17</sup>Aɗi nywinywi mwakudzionani kwamba mu majabva muna kula kintu, na ntamu ɗuri wa kiɗechonse! Ela ntamudzi kwamba nywinywi mu wantu mwiwo ɗinani na mwiwo ɗei wa mwiso. Na ntamudzi kwamba mu masikini, mu ntumbu matso na mwaa vivi!

<sup>18</sup>Ɗubva nyakumushaurini muguye kwangu dhahaɓu idheresejweyo na moho, mupate kuwa majabva ɗugha. Na guyani mavwazi meupe ya kuvwaa kuyawa kwangu, mupate kvinga aeɓu yenu. Guyani na ɗawa ya matso kuyawa kwangu ya kungiza humu matsoni mwenu, mupate kuona.

<sup>19</sup>Kula nimutsakiye, mimi namukanya na kumuadhiɓu. Ɗubva hendani hiɗu mupfyehuze mama.

<sup>20</sup>Ƨayowani! Mimi nisumama muɗyangoni nyakubigani hoɗi. Huyuɗe adzeyeisikia sauti yangu na akinifungwiiya muɗyango, nanjia mwakwe naɗya pfamodza nae, nae anaɗya pfamodza nami.

<sup>21</sup>Na kula adzeyeshinda, namumpa kukaa pfamodza nami kwa kiti changu cha kihaju dza hiviɗe vyangu nishindiyevyo nikikaa pfamodza na Baba kwa kitiche cha kihaju.

<sup>22</sup>Eye na masikio, nasikiye hivi vya huyu Ruhu evyokuyambiani matsanganiko.’ ”

#### **Upfenuo wa Yohana 4**

<sup>1</sup>Ɔaɗa ya hayo, niona nzozu ingine. Kudzayowa niona muɗyango upfenukiyeo hukuɗe mbinguni. Na hiɗe sauti iyokuwa dza sauti ya ɗarumbeta, niyoisikia ikinena nami ɗura inyamba, “Nzoo huku dzuu nikuyange haya ya kwamba ni haɗi yahendeke huko usoni.”

<sup>2</sup>Ɔwikira niwa Ruhuni, na kudzayowa, niona kiti cha kihaju mbinguni kikajwecho ni muntu.

<sup>3</sup>Huyu akaiye hapfa kitini ekingara dza mawe ya thamani ya yasipa na kanelia. Na hichi kitiche cha kihaju kiwa kizunguukwa ni uha wiwoukingara dza iwe ɗya thamani ɗya zumaraɗi.

<sup>4</sup>Na pia hichi kiti kiwa kizunguukwa ni viti vingine miyongo miwii na vine vya kihaju. Hivi viti viwa vikajwa ni wazee miyongo miwii na wane wavwaiyeo nguo nyeupe pee na viyemba vya dhahaḅu.

<sup>5</sup>Kuyawa hapfa pfa hichi kiti cha kihaju kubiga mpepfe na maḅaḅaḅu. Na usoni ya hichi kiti kwiwa matsotso mafungahe yeyoyakiwaka. Haya yewa ni hizi ruhu mfungahe za Muungu.

<sup>6</sup>Hapfa usoni pfa hichi kiti pfewa dza ḅahari ya kiyoo iyoikingara dza hiḅi dzuwa. Hichi kiti kiwa kizunguukwa ni viumbe vine, chicho chikiwa kahikahi. Hivi viumbe viwa na matso kula pfantu usoni na mongoni.

<sup>7</sup>Kiumbe cha ḅura kiwa dza nsimba. Cha pfii kiwa dza ngombe ndume. Cha hahu kiwa na uso dza wa mwanaaḅamu na kiumbe chane kiwa dza chalikoko eyekuguukani.

<sup>8</sup>Hivi viumbe vyoone, kula kimodza kiwa na maḅawa mahandahu. Na haya maḅawa yao, yewa na matso kula pfantu hangu dzuu mumpaka nsi. Hivi viumbe vikikwimba siku na musikahi pfasipfo kunyamaa. Vikikwimba vikyamba, “Mudheru, mudheru, mudheru, ni ḅwana Muungu mwenye nguvu zonse. Jeje ewapfo, yupfo na ndiye adzeyekudza.”

<sup>9</sup>Na kula pfa hiviḅe viumbe vyoone vipfonamushaḅa na kumukuzya na kumuyaviza ḅuḅa huyu akaiye hapfa pfa hichi kiti cha kihaju, eyenaishi maishi,

<sup>10</sup>hawaḅe wazee miyongo miwii na wane wekimugwiya na kumuyomba. Wekivuya viyemba vyao usoni yakwe na kwamba,

<sup>11</sup>“ḅwana jwehu na Muungu jwehu, wewe unamala kushaḅwa na kukuzwa na kuhilwa. Koro wewe kuumba kula kintu, na kula kintu uumbiyecho kiwa na chakuishini kwa kutsaka kwako wewe.”

## Upfenuo wa Yohana 5

<sup>1</sup>Kisa niona hu mukono kuyume wa huyu akaiye kwa hichi kiti cha kihaju ugija chuo. Hichi chuo kiwa choregwa nze na kuzimu na kiwa kifungwa na mihuri mifungahe.

<sup>2</sup>Niona na malaika mwenye nguvu, akilalabva akyamba, “Ni ga eye na hachi ya kuivunza hi mihuri akifunguye hichi chuo?”

<sup>3</sup>Ela ntakwiwa na yuḅejwonse mbinguni, lumwenguni ambu kuyawa kwa lumwengu jwa wafu, eyekuwa na hachi ya kuchifunguya hichi chuo akiyowe.

<sup>4</sup>Nami kudzaona hivyo, ninjia kuiyani na tsungu muno, koro ntakwiwa na haḅa mumodza eyekuwa na hachi ya kuchifunguya hichi chuo achisome.

<sup>5</sup>Ela mumodza jwa hawaḅe wazee miyongo miwii na wane kanyamba, “Yatsa kuiya! Huyu eyenahanwa Nsimba jwa kyeeti cha Yuḅa, eye kiḅukuḅuku cha haju

Daudi kashinda! Ndookomu jeje anaweza kuivunza hi mihuri akifunguye hichi chuo.”

<sup>6</sup>Kisa niona Mwana Mbuzi asumamiye hafufi na hiki kiti cha kihaju na akizunguukwa ni hivi viumbe vyoone na hawa wazee. Huyu Mwana Mbuzi kakaa dza kwamba ewa katsinzwa. Na ewa na mpembe mfungahe na matso mafungahe, ambayo ni hizi ruhu mfungahe za Muungu zizohumwa lumwengu yuzima.

<sup>7</sup>Huyu Mwana Mbuzi kenda kachihwaa hichi chuo kuyawa kwa hu mukono kuyume wa huyu akaiye hapfa pfa hichi kiti cha kihaju.

<sup>8</sup>Epfokihwaa, hiviđe viumbe vyoone pfamodza na hawađe wazee miyongo miwii na wane wamugwiya maguuni. Kula mumodza jwao ewa na kinuḃi na ḃaakuli ya dhahaḃu. Haya maḃaakuli yewa yadzaa vumba ḃipu ambaḃyo ni mayombo ya wadheru wa Muungu.

<sup>9</sup>Wamwimbia wiya mupfya wakyamba, “Wewe unamala kuchihwaa hichi chuo, uivunze hi mihuri yakwe. Koro wewe kuyagwa, na kwa mwaziwo, kumukombowea wantu Muungu. Wewe kumukombowea wantu, wa kuyawa kula nsi na kyeeti na lugha.

<sup>10</sup>Kuwahendeza wawe wantu wa Uhaju wa Muungu na wakohani wa kumuhumikia Muungu jwehu. Nao wanajuḃawala lumwengu.”

<sup>11</sup>Nikidzanikihea matso kawii, nisikia sauti za malaika wenji na wenji wasioḃalika waringiyeo hiki kiti cha kihaju, na hivi viumbe vyoone na hawa wazee.

<sup>12</sup>Hawa malaika wekikwimba na sauti nkuu wakyamba, “Huyu Mwana Mbuzi ayagijwe, anamala kushadwa kwa dzambo ḃya uwezowe mukuu, ujabvawe, mvidhyoye na nguvuze. Jeje anamala kukuzwa na kuhilwa.”

<sup>13</sup>Kisa nisikia viumbe vyonse, vivyo mbinguni dzuu na lumwenguni na nsii ya gaga ḃya lumwengu na madzini kuzimu, vikikwimba wiya. Vikwimba vyamba, “Huyu akaiye dzuu ya kiti cha kihaju, pfamodza na huyu Mwana Mbuzi, nawashadwe na kukuzwa, na kuhilwa na kuwa na nguvu maishi na maishi.”

<sup>14</sup>Na hiviđe viumbe vyoone vyamba, “Amina.” Na hawađe wazee miyongo miwii na wane wamugwiya Muungu na huyu Mwana Mbuzi kuwayomba.

## Upfenuo wa Yohana 6

<sup>1</sup>Kisa nimuona huyu Mwana Mbuzi akiuvunza hu muhuri wa ḃura kahi ya hiđe mihuri myofungahe. Na nisikia kiumbe kimodza kahi ya hiviđe viumbe vyoone kikinena na sauti nkuu dza ḃaḃaḃu, kikyamba, “Nzoo huku!”

<sup>2</sup>Nami nikidzanikihea matso, niona farasi dzeupe. Na huyu aḃipfaiye ewa kagija uha na ewa kabigwa kiyemba cha kihaju. Jeje ewa ni mushindi na kayawa kwenda akaheke na wangine zaiḃi.

<sup>3</sup>Huyu Mwana Mbuzi epfouvunza hu muhuri wa pfii, nikisikia hiki kiumbe cha pfii kikyamba, “Nzoo huku!”

<sup>4</sup>Na pfapfo kutupuka farasi dya ranji ya moho. Huyu adipfaiye ewa kapfegwa yupfanga yuku na uwezo wa kujumuya viha lumwenguni, ili awahendeze wantu wayagane wao na wao.

<sup>5</sup>Huyu Mwana Mbuzi epfouvunza hu muhuri wa hahu, nikisikia hiki kiumbe cha hahu kikyamba, “Nzoo huku!” Na pfapfo kudzayowa, niona farasi dzeusi. Huyu adipfaiye ewa kagija mizani mukononi.

<sup>6</sup>Kisa nisikia dza sauti iyoikiyawa kahi ya hiviḁe viumbe vyoone, ikyamba, “Mufuto mumodza wa nganu kwa maipfo ya kiḁaruwa cha nsiku nzima! Na mifuto mihahu ya muhama kwa maipfo ya kiḁaruwa cha nsiku nzima. Ela haya mafuha ya mizeituni na hi mvinyo, sivinange!”

<sup>7</sup>Huyu Mwana Mbuzi epfouvunza hu muhuri wa ne, nikisikia hiki kiumbe chane kikyamba, “Nzoo huku!”

<sup>8</sup>Na pfapfo kudzayowa, niona farasi dya ranji ya ivuivu. Na huyu adipfaiye ekihanwa Kufwa, na Lumwengu jwa Wafu jwikimuuḁa na nyuma. Wao wewa wapfegwa mamulaka ya kuyaga roḁo ya wantu wa huju lumwengu kwa njia ya viha, nzaa, vipfufu na binensa.

<sup>9</sup>Huyu Mwana Mbuzi epfouvunza hu muhuri wa tsano, niona madhabahu. Na hapfa nsi ya haya madhabahu, niona ruhu za hawa wayagijweo kwa dzambo dya chuuwo cha Muungu na ushuhuda wao.

<sup>10</sup>Wekinena na sauti nkuu wakyamba, “E Bwana Mwenye nguvu, wewe u Mudheru na u Muhikizika! Unaina haḁa ari kuipfa halo kwa kuwahukumu awa wantu wa lumwengu wahuyagiyeo?”

<sup>11</sup>Kisa kula mumodza jwao kapfegwa nkanzu nyeupe pee. Na wambigwa wasohe kwa muḁa kachuchu, mumpaka hi hesaḁu ya hawa wandugu zao na wahumisi wenzao wadzeoyagwa dzao itimiye.

<sup>12</sup>Kisa huyu Mwana Mbuzi kavunza hu muhuri wa handahu. Na nikidzanikihea matso, niona kugunga muhehemo mukuu wa nsi. Hiḁi dzuwa ḁihenda kiza na ḁigala dzeusi si, dza sinzi. Hu mwezi uperuka ranji ya moho dza mwazi.

<sup>13</sup>Na hizi nyoha zigwa lumwenguni dza hiviḁe vya kiyuwa kivyonaharachaa kwipfonabiga vuḁo.

<sup>14</sup>Hizi mbingu zikutsa-kutsa dza karaḁasi zinujwa. Kula murima na kula kilulu vyaara na hapfaḁe vipfokuwa.

<sup>15</sup>Kisa mahaju ya lumwengu, wakuu wa sirikali, wakuu wa maḁyeshi, majabva na wantu wa maana maana wangine pfamodza na wantu wangine wonse, hangu wahumwa na weo huru, wadzifitsa mampangoni na myambani huku mirimani.

<sup>16</sup>Wayambia hi mirima ne myamba, “Hugwiyeni muhufitse, hutseonwa ni huyu akaiye hapfa pfa hichi kiti cha kihaju na muhuchinge na ngoro ya huyu Mwana Mbuzi.

<sup>17</sup>Koro nsiku yao ya kuhuhukumu ifika. Ni ga adzeyepfona?”

## Upfenuo wa Yohana 7

<sup>1</sup>Baada ya hayo, niona nzozi ingine. Niona malaika wane wasumamiyeo mpebe zoone za huju lumwengu. Wazigija hizi mpepfo zoone za huju lumwengu ili zitsebige nsi guba, baharini ambu mihini.

<sup>2</sup>Kisa niona malaika yungine ayawiye muyao dzuwa. Ewa katsukuya muhuri wa Muungu eye moja. Kawakelelea hawa hawa malaika woone weopfegwa uwezo wa kuinanga hi nsi ne bahari, kawamba,

<sup>3</sup>“Namutseinanga nguzi hi nsi wala hi bahari ambu hi mihi, mumpaka wahumisi wonse wa huyu Muungu jwehu huwabige muhuri humu vidhangoni.”

<sup>4</sup>Kisa nisikia hesabu ya hawa hawa wabigijweo muhuri wa Muungu. Wewa ni wantu gana na miyongo mine na wane elefu, kuyawa kwa vyeeti vyonse vya Isiraeli.

<sup>5</sup>Na kula kyeeti kwiwa wantu elefu kumi na mbii wabigijweo muhuri. Kyeeti cha Yuda kwiwa wantu 12,000, kyeeti cha Rubeni wantu 12,000, na kyeeti cha Gadi wantu 12,000.

<sup>6</sup>Kyeeti cha Aseri kwiwa wantu 12,000, kyeeti cha Nafutali wantu 12,000, na kyeeti cha Manase wantu 12,000.

<sup>7</sup>Kyeeti cha Simioni kwiwa wantu 12,000, kyeeti cha Lawi wantu 12,000, na kyeeti cha Isakari wantu 12,000.

<sup>8</sup>Kyeeti cha Zabuloni kwiwa wantu 12,000, kyeeti cha Yusufu wantu 12,000, na kyeeti cha Benyamini wantu 12,000.

<sup>9</sup>Baada ya hayo, niona tuu nkuu na nkuu ya wantu isiyoatalika. Wewa ni wantu wa kuyawa kula nsi, na kula kyeeti na kula lugha. Wewa wasumama usoni ya hiki kiti cha kihaju na usoni ya huyu Mwana Mbuzi. Wewa wavwaa mavwazi meupe na wagija mahambi ya mintende mikononi mwao.

<sup>10</sup>Nao wekinena na sauti nkuu wakyamba, “Muungu jwehu eyenakaa kwa hichi kiti cha kihaju, pfamodza na huyu Mwana Mbuzi, ndiwo weo na uwezo wa kupfonya wantu.”

<sup>11</sup>Na hawa malaika wonse weosumama kukizunguuka hiki kiti pfamodza na hawa wazee na hivide viumbe vyoone, wamugwiya Muungu kumuyomba.

<sup>12</sup>Wamba, “Amina. Muungu jwehu anamala kushadwa kwa dzambo dya uwezowe mukuu, mvidhyoye na nguvuze. Jeje anamala kukuzwa na kuyavizwa duu na kuhilwa maishi na maishi. Amina.”

<sup>13</sup>Kisa mumodza jwa hawaḁe wazee miyongo miwii na wane kaniuza kanyamba, “Awa wantu wavwaiyeo mavwazi meupe kuwamanya? Wayawa ku?”

<sup>14</sup>Mimi nimwambukuya nimwamba, “Sidzi ḁwana. Ndiwe umanyie.” Nae kanyamba, “Hawa ni hawaḁe wayawiyeyo kwa hiḁe ḁina nkuu. Wao wayafuya mavwazi yao na mwazi wa huyu Mwana Mbuzi, na yahenda meupe pee.

<sup>15</sup>Ndiyo maana wasumamiyeyo usoni ye kiti cha kihaju cha Muungu, wakimuhumikia siku na musikahi Hekaluni mwakwe. Nae jeje akaiye kwa hiki kiti cha kihaju anawa pfamodza nao na kuwachinga.

<sup>16</sup>Nao ntawawezi kusikia nzaa wala nchiu kawii meshi. Ntawawezi kubigwa ni dzuwa kawii wala kutsomwa ni moho wa hiḁi dzuwa.

<sup>17</sup>Koro huyu Mwana Mbuzi eyenakaa kahikahi ya hiki kiti cha kihaju, anawa ndiye huyu muḁunga jwao. Nae anawapfiika kuntu kwa matsana ya madzi ya mutsangani kuzimu yeyonapfa wantu maisha. Nae Muungu anawafuta mitsozi yao yonse.”

## **Upfenuo wa Yohana 8**

<sup>1</sup>Kisa huyu Mwana Mbuzi kauvunza hu muhuri wa fungahe. Epfouvunza, hukude mbinguni vyamba mya kwa hafufi nusu saa nzima!

<sup>2</sup>Niwaona hawaḁe malaika wakuu wofungahe, weonasumama usoni kwa Muungu, wakipfegwa ḁarumbeta mfungahe.

<sup>3</sup>Kisa kudza malaika yungine, kadzakasumama hapfa pfepfo haya madhabahu. Ewa kagija ḁaakuli ya dhahaḁu ya kufukizia vumba. Na kapfegwa vumba dzinji ḁya kutsanganya na mayombo ya wadheru wa Muungu wonse, ili amuyaviye Muungu hapfa pfa haya madhabahu ya dhahaḁu yeyo usoni ya hichi kiti cha kihaju.

<sup>4</sup>Na hu mosi wa hiḁi vumba pfamodza na haya mayombo ya wantu wa Muungu, vyenda dzuu mumpaka hapfaḁe pfa Muungu epfokuwa.

<sup>5</sup>Kisa huyu malaika kahwaa makaa ya moho hapfaḁe madhabahuni, kayangiza humu mwa hi ḁaakuli ya kufukizia vumba na kaifaḁula lumwenguni. Na kugunga maḁaḁaḁu, mpepfe na muhehemo mukuu wa nsi.

<sup>6</sup>Hawa malaika wafungahe weokuwa na hizi ḁarumbeta zomfungahe, wadziweka ḁayari kuzibiga.

<sup>7</sup>Malaika jwa ḁura kaibiga hi ḁarumbeta yakwe na kugwa mvuya ya mawe na moho itsanganyikiyeyo na mwazi. Hi mvuya igwa lumwenguni, na sehemu modza ya hahu ya huju lumwengu ipfya. Na hi mihi na mani yonse ya hiyo hiyo sehemu vipfya.

<sup>8</sup>Kisa malaika jwa pfii epfoibiga hi tarumbeta yakwe, kufatulwa kintu dza murima mukuu wiwoukiwaka moho. Ugwa baharini, na sehemu modza ya hahu ya hi bahari ihalawa mwazi.

<sup>9</sup>Sehemu modza ya hahu ya hivi viumbe vyonse vya humu baharini vifwa. Na sehemu modza ya hahu ya hivi vyombo vyonse vivyokuwa humu baharini vinangwa-nangwa.

<sup>10</sup>Kisa malaika jwa hahu nae kabiga tarumbeta yakwe. Kugwa nyoha nkuu kuyawa yuwinguni iyoikiwaka dza tsotso. Igwiya sehemu modza ya hahu ya matsana na sehemu zingine zonse ziizo na madzi.

<sup>11</sup>Hi nyoha ikihanigwa "Tsongu wa Muharagesa." Na sehemu modza ya hahu ya haya madzi yagala tsungu. Wantu wenji wafwa kwa dzambo dya kunwa haya madzi yeyokuwa tsungu.

<sup>12</sup>Kisa malaika jwane nae kabiga hi tarumbeta yakwe. Sehemu modza ya hahu ya hidi dzuwa, mwezi na nyoha vipata bigo na ntavikuyangaa kawii. Sehemu modza ya hahu ya hu muyanga wa nasiku na wa musikahi waara.

<sup>13</sup>Kisa nikidzanikihea matso, niona chalikoko kakuguukani humu angani dzuu. Na nimusikia akinena na sauti nkuu akyamba, "Waa dinani, waa dinani, waa dinani! Saa ya hawa malaika wohahu wasaiyeo wadzepfzibiga hizi tarumbeta zao, wantu weokuishini lumwenguni wanawa dinani!"

## Upfenuo wa Yohana 9

<sup>1</sup>Kisa huyu malaika jwa tsano kabiga hi tarumbeta yakwe. Na nikidzanikihea matso, niona nyoha igwiyeyo kuyawa mbinguni. Hi nyoha iwa ipfegwa yufunguo jwa hidi simo disidyo mwisu.

<sup>2</sup>Na hi nyoha ipfodifunguya hidi simo, kuyawa luutano dya mosi dza mosi wiwoukiyawa ntanuni. Wiwa mosi muziho chima cha kwamba hidi dzuwa na hidi anga vifungiiya kiza cha go!

<sup>3</sup>Humu mosini kuyawa maghere na yahama humu nsini. Na haya maghere yapfegwa uwezo wa kuuma wantu dza ninge.

<sup>4</sup>Yambigwa yatseedya mani, mihi ambu mumea udewonse. Ela ni yawaadhibu hawađe wantu wonse wasio na hu muhuri wa Muungu vidhangoni mwao.

<sup>5</sup>Haya maghere yewa yapfegwa ruhusa ya kuwangiza waragha hawa wantu kwa myezi mitsano, ela watsewayaga. Hu tsungu wa huku kuuma kwao wiwa dza tsungu wa ninge epfonauma muntu.

<sup>6</sup>Hizo hizo nsiku za hu waragha, wantu wanalacha kufwa ela kufwa kunawadarama. Hata wakitamani kufwa ntawawezi kufwa.



<sup>7</sup>Haya maghere yewa yakaa dza mafarasi yatayarishijweyo kwenda vihani. Humu vitswani yakaa dza kwamba yabigwa viyemba vya dhahaḅu na haya maso yao yewa dza maso ya wanaadamu.

<sup>8</sup>Hizi nywii zao ziwa ndeya dza nywii za wake. Na magego yao yewa dza magego ya nsimba.

<sup>9</sup>Hizi ḅagwi zao zikaa dza kwamba zivingwa na nguo za chuma. Hizi mbawa zao zikwakupfungani zikivuma dza magari menji ya kunuhwa ni mafarasi yeyokwendani vihani.

<sup>10</sup>Haya maghere yewa na michia iyonauma dza ninge. Na hi sumu ya kumuhendeza muntu awaraghe kwa myezi mitsano iwa yaa humu michiani.

<sup>11</sup>Haju jwao ni huyu malaika eyenaḁisumamia hiḁi simo ḁisidyō mwiso. Sariḁye kwa Kieburania ekihanwa “Abadoni,” na kwa Kiyunani ekihanwa “Apolioni.” Na maanaye ni “Munanzi.”

<sup>12</sup>Hiḁi bigo ḁya ḁura sasa ḁisakusia. Kusaa haya mabigo yangine mowii.

<sup>13</sup>Kisa huyu malaika jwa handahu kabiga hi ṭarumbeta yakwe. Nami nisikia sauti iyawiyeyo kuyawa kwa hizide mpembe zoone za haya madhabahu ya dhahaḅu yeyo usoni kwa Muungu.

<sup>14</sup>Hi sauti imwamba huyu malaika jwa handahu eyekuwa na hi ṭarumbeta, “Wafunguye hawaḁe malaika woone weofungwa tsana nkuu ya Efurati.”

<sup>15</sup>ḁubva hawaḁe malaika woone wafungujwa. Wewa wawekwa ṭayari kwa dzambo ḁye hi nsiku ili wayage sehemu modza ya hahu ya wanaadamu wonse.

<sup>16</sup>Na kwiwa ḁyeshi ḁya wapfaa mafarasi. Nisikia kwamba hesaḅu ya hiḁi ḁyeshi iwa inafika milioni magana mawii.

<sup>17</sup>Na hivi ndivyo nioneyevyo haya mafarasi na hawa wapfaa mafarasi humu nzozi: Humu ḅagwini wewa wawwaa nguo za chuma zizokuwa na ranji ya moho, ranji ya nili na ranji ya kitweyo. Hivi vitswa vya haya mafarasi viwa dza vitswa vya nsimba. Na haya manwa yao yekiyawa moho, mosi na nsoho zizo dza mosi wa ḅaruḁi.

<sup>18</sup>Sehemu modza ya hahu ya wanaadamu wonse iyagwa ni haya mabigo mazuka mohahu yo moho, mosi na ḅaruḁi, yeyoyakiyawa manwani mwa hayaḁe mafarasi.

<sup>19</sup>Hizi nguvu za haya mafarasi ziwa zaa humu manwani na michiani mwao. Hi michia yao iwa dza nyoka za singo zizonauma wantu.

<sup>20</sup>Hawa wanaadamu wapfoneyeo na haya mabigo, amaale wadziza kupfyehuza mama. Ishinu wagija kuyomba mashaṭani na masanamu wayaelekanyiyeo na dhahaḅu, fwedha, shaḅa, mawe na mihi. Na hali haya masanamu yewa ntayawezi kuona, wala kusikia ambu kwenenda.

<sup>21</sup>Na wala ntawakupfyehuzza mama wayatse uyaji wao, tsawi, ubari na wivi wao.

## Upfenuo wa Yohana 10

<sup>1</sup>Kisa niona malaika yungine mwenye nguvu akwakusukani kuyawa mbinguni. Ewa kavwaa wingu, na dzuu ya hiki kitswache kukaa uha. Hu uso wakwe wikiyangaa dza hiđi dzuwa na maguuye yewa dza nguzo za moho.

<sup>2</sup>Kasumama, na mukononi mwakwe ewa kagija kadzuo kekopfenujwa. Kuguuđye đya mukono kuyume điwa điranga baharini na đya mukono tsonso điwa điranga gubani.

<sup>3</sup>Na kahana na sauti nkuu dza hiviđe vya nsimba evyonanguruma. Epfohana, kuhika miđitimo ya mađabađu mafungahe.

<sup>4</sup>Hayade mađabađu yepfohika, nikitsaka kwora hiviđe yaneneyevyo. Ela nisikia sauti kuyawa mbinguni ikinyamba, "Haya yanenejweyo ni haya mađabađu ni siri, nkudzoyore!"

<sup>5</sup>Kisa huyude malaika niyemuona akisumama kuguu modza baharini na kuguu modza gubani, kaunwiiya mbinguni dzuu mukono wakwe wa kuyume kuyapfa.

<sup>6</sup>Kayapfa kwa sari đya huyu eyenaishi maishi na maishi, aumbiye mbingu na nsi, bahari, na kula kiumbe chicho kuzimu ya hivi hivi vyonse. Kamba, "Wakati wa kuinda usiya!"

<sup>7</sup>Huyu malaika jwa fungahe akibiga hi tarumbeta yakwe, Muungu anađimiza hu mupangowe wiwokuwa siri. Anađimiza dza viviđe evyowambia wahumisiwe, ambao ni hawa manabii."

<sup>8</sup>Kisa niisikia kawii hiđe sauti ya kuyawa mbinguni ikinena nami ikinyamba, "Enda ukakahwae hakađe kadzuo kapfenwiiwoko, keko mukononi mwa huyu malaika asumamiye kuguu modza đikiwa baharini na kuguu modza đikiwa gubani."

<sup>9</sup>Đubva nami nimwendea huyu malaika na nimwamba animpe hakađe kadzuo. Nae kanyamba, "Kahwae ukadye. Humu kanwani kanakutsamia tsamu dza uchi, ela humu humboni kunawa ni tsungu muhupfu."

<sup>10</sup>Nami nikahwaa haka kadzuo kuyawa kwa huyu malaika na nikađya. Humu kanwani kewa tsamu dza uchi, ela nipfokamia, humu humboni kwiwa ni tsungu muhupfu.

<sup>11</sup>Kisa nyambigwa, "Ni hađi uyavye unabii kawii wa haya yadzeyohendeka kwa wantu wenji wa nsi garagara, vyeeti garagara, lugha garagara na hađa kwa mahaju."

## Upfenuo wa Yohana 11

